ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba - Tarehe 29 Septemba, 2019

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, swali la mwanzo leo nimeombwa, kwa hivyo, litakuwa swali Nam.74 la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sababu ya dharura ambayo Mhe. Waziri, anayo.

Nam. 74

Kuendelezwa kwa Viwanda Zanzibar

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya viwanda ni sekta muhimu kwa ukuaji wa uchumi na kukuza ajira kwa vijana.

a) Je, Zanzibar vipo viwanda vingapi hadi sasa ambavyo vishaanza uzalishaji na ambavyo havijaanza uzalishaji.

b) Je, viwanda hivyo vinatoa ajira ngapi kwa vijana.

c) Je, Sheria na Sera yetu ya Uendelezaji wa Viwanda vya Kati na Vidogo kweli iko rafiki na kuwavutia wawekezaji.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 74 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sensa ya viwanda vya mwaka 2012:

a) Jumla ya viwanda 2,201 vinaendelea na uzalishaji Zanzibar. Kati ya idadi hiyo, viwanda 235 vimeajiri wafanyakazi 10 au zaidi kwa kila

kiwanda na viwanda 1,966 ni vidogo vidogo vilivyoajiri watu wasiozidi tisa kila kimoja.

b) Jumla ya watu zaidi ya 10,600 wameajiriwa katika sekta ya viwanda iliyo rasmi, Zanzibar.

c) Sera ya Maendeleo ya viwanda vya mwaka 1969 inafanyiwa mapitio ili iwe rafiki zaidi na iendane na mahitaji ya sasa ya kuwavutia wawekezaji.

Mhe. Yussuf Hassan Idd: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, wizara inashirikiana vipi na *ZIPA* ili watafute wawekezaji wa viwanda wakubwa kuliko kuwa na utitiri wa viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viawnda na Masoko: Mhe. Spika, Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko tumepewa jukumu la kutayarisha mazingira mazuri kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Wajibu wetu tunakuwa tunatakiwa tutie vile vivutio halafu tuwakabidhi *ZIPA* wafanyie kazi. Sasa kwa kipindi hiki sambamba na kupitia Sera ya Maendeleo ya Viwanda tunajipanga sasa hivi kuweka mikakati ya viwanda na kuorodhesha viwanda vile ambavyo vikubwa na vile ambavyo kwa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. *ZIPA* jukumu lake wanakwenda na sisi pia tunatoka kwenda kuwashajihisha wafanyabiashara wawekezaji waliokuwa wakubwa. Kwa hivyo, kazi hiyo tumepewa kazi ya jukumu hilo na tunaifanyia kazi kwa ajili ya kuwavutia wafanyabiashara wawekezaji wakubwa. Lakini sehemu kubwa nyengine inafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, tunafahamu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza viwanda ilitenga maeneo mbali mbali kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, lakini vile vile shughuli nyengine za kiuchumi. Lakini tumeona katika maeneo yale mpaka sasa hivi hakujakuwa na harakati kubwa za ujenzi wa viwanda na kuna baadhi ya maeneo hasa maeneo ya Mpendae ambako kuliwekwa maeneo makubwa, lakini sasa hivi maeneo yale yameonekana yameimarika kimakaazi zaidi ya wananchi kuliko ujenzi wa viwanda.

Sasa je, serikali kwa sasa hivi kuna mpango maalum waliouweka kwa ajili ya kutenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na kuacha utaratibu

uliokuweko sasa hivi kwamba kuna viwanda vimejengwa kati kati ya maeneo ya makaazi ya watu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli huko nyuma kuligawiwa maeneo maalumu kwa ajili ya kuwekeza viwanda kwa mfano maeneo huru yaliyokuweko na pia maeneo mengine ya viwanda vidogo vidogo. Ni kweli kwa bahati mbaya kwa mfano eneo la Mpendae/Mombasa limeendelezwa sasa hivi kujengwa nyumba za wakaazi, lakini mwelekeo wa wizara yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Tume ya Mipango kuweka maeneo maalum kwa ajili ya kuweka Sekta ya Viwanda. Kwa hiyo, kama nilivyosema tumo katika kupitisha, kumalizia kufanya *review* ya Sera ya viwanda ndani ya sera hiyo tutapendekeza na sisi tumeshaanza kuzungumza na Waziri wa Ardhi kuona kwamba maeneo maalum yanawekwa kwa ajili ya viwanda na kuweza kuyatekeleza hayo kuwarahisishia pia wawekezaji ili waweze kufanya kazi zao bila ya usumbufu. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri, amejibu swali la msingi na la nyongeza linalohusu viwanda, kuna Kiwanda cha Soda ambacho serikali iliingia ubia na muwekezaji pale akifanya kazi kwa muda mrefu sana. Lakini sasa kiwanda kile ile dhamira ya serikali imepotea baada ya kuzalisha pale sasa hivi wanazalisha Tanzania Bara na kuleta bidhaa ile na pale kufanya *store*.

Nini utaratibu wa serikali katika kuhakikisha kiwanda kile kinaendelea lakini kisifanywe *store* kama utaratibu uliyopo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli Kiwanda cha Soda kilibinafsishwa, lakini kwa matarajio kwamba kitaendelea kuwa juu ya Kiwanda cha Soda. Lakini matatizo hayo tunayo kwa viwanda vyote ambavyo vimebinafsishwa, nakumbuka Kiwanda cha Sigara, Kiwanda cha Viatu na kadhalika. Sasa katika mazungumzo tuliokuwa tumefanya kimkakati kuangalia kama tunaweza kurudisha kiwanda kile kikarudia tena kuzalisha soda, tatio kubwa liliopo sio tu Kiwanda cha Soda kile pale lakini viwanda vyote vya soda, juisi na kadhalika hapa Zanzibar vinapata matatizo kwa sababu ushindani wa bidhaa kutoka nje umekuwa mkubwa.

Mhe. Spika, hii inatokana, kwa mfano kama soda za vikopo zinaingizwa kwa njia ya magendo (njia ya kutolipa ushuru unaotakiwa), matokeo yake hawawezi kushindana na soda za nje. Jambo hili tunalifanyia kazi kuona kwamba sheria kali zinachukuliwa na viwango sahihi vya kodi vinawekwa kwa bidhaa yoyote

ambayo hapa ndani ya nchi tunazalisha ili viwanda vyetu vya ndani viweze kupata kwenda vizuri, bila ya hivyo Kiwanda cha Soda na viwanda vyengine vile vile havitoweza kwenda vizuri kwa sababu ya ushindani ambao sio rasmi au ushindani uliokuwa sio sawa kwa viwanda vyetu vya ndani na viwanda vya nje.

Nam. 187

Mgao wa Zanzibar kutoka Msaada wa Serikali ya Marekani

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata msaada wa Shilingi 895 Bilioni, kutoka Serikali ya Marekani kwa ajili ya shughuli mbali mbali za maendeleo.

Mhe. Waziri, kwa kuwa fedha hizi ni za Muungano. Je, Zanzibar imepata kiasi gani katika fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 187 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa ipatewe fedha na Marekani kutekeleza miradi mbali mbali chini ya ufadhili wa Miradi ya *MCC Compact II*. Hata hivyo, fedha hizo hazikuwahi kutolewa kutokana na Bodi ya *MCC* kutoidhinisha fedha hizo. Kama tunakumbuka mwezi Disemba, 2015 bodi hiyo ili-*suspend* msaada huo kwa Tanzania. Lakini ilipofika mwezi wa Machi, 2015 *statement* ilitolewa ya kwamba *MCC* imesitisha ufadhili wake kwa Tanzania.

Mhe. Spika, kama ilivyokuwa kwa miradi kupitia ufadhili wa *Compact I*, Zanzibar nayo ilikuwa inufaike kupitia mradi wa kujenga uwezo wa Shirika letu la Umeme *ZECO*, lakini vile vile kusaidia masuala ya usambazaji umeme na kusaidia ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya nishati ya umeme. Kwa vile *Compact II* haikuwepo, kwa hivyo, pia fedha hizo kwa upoande wa Zanzibar hazikuwepo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri katika majibu yake sahihi ambayo yako fasaha

kabisa. Lakini pamoja na kukosa misaada hii ambayo kwa bahati mbaya imekatishwa kwa mambo wanayoyajua wenyewe wahisani wetu. Je, kwa kuwa kuna fedha nyengine zinajitokeza katika maeneo mengine Serikali yetu ya Zanzibar inafaidika vipi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, katika misaada mingine Zanzibar imekuwa ikipata *share* yake kama utaratibu ulivyo. Ziko njia tatu ambazo nchi yetu huwa inapata misaada kutoka nje ikiwa mikopo au ruzuku na njia ya kwanza ni *general budget support*, misaada ya kibajeti ambayo mgao wa Zanzibar unakuwa ni asilimia 4.5. Kwa hivyo, hizo zikitolewa Zanzibar inapata *share* yake.

Vile vile, kuna ufadhili wa miradi kwa maana ya *direct project funding*, sasa hii inategemea mradi uliyoibuliwa kama mradi huo umeibuliwa kwa Zanzibar basi ufadhili huo unakuja moja kwa moja kwa Zanzibar.

Njia ya tatu ni Mfuko Maalum kwa maana ya *basket funding*, lakini huu ni kwa ile miradi mikubwa ambayo inachukua wafadhili wengi, nayo hiyo vile vile Zanzibar imekuwa ikipata misaada hiyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi ningeomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mimi ningeomba kujua kwamba, kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano tunapata misaada mingi kupitia kwako na baadae kupata ile asilimia inayopaswa kupewa sisi Zanzibar. Ni *procedure* gani zinatumika wakati fedha zinapoletwa za wazamini mpaka kuzipata sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni *procedure* gani zinatumika baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mpaka zile pesa kuzipata sisi Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali, utaratibu uko wazi ni kwa misaada ya kibajeti fedha zinazotolewa na wafadhili zinapitia Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *share* yetu inaletwa kwenye Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni 4.5%. Sasa huo ni utaratibu mmoja.

Utaratibu mwengine ni ufadhili wa miradi, *project funding*. Ufadhili huu aghalabu sisi tunaanza kuibua mradi wetu, lakini vile vile kwa upande wa Jamhuri ya Muungano nao wanaibua mradi wao, tunapoibua miradi ikiwa ni mikopo au misaada Serikali ya Jamhuri ya Muungano hasa kwa mikopo ndiyo

inayodhamini mikopo hiyo na inapodhaminiwa kunakuweko na *project agreement* au *financing agreement* inayosainiwa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na huyo mfadhili. Lakini baadae kunakuweko na *all landing agreement* ambayo hiyo tunasaini baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri na ufafanuzi ambao wa kuridhisha kabisa, mimi nina swali dogo la nyongeza. Ni miradi ipi ilipangwa katika hii *project* ya kwenye *funding* ya *MCC Compact II*, ni miradi ipi iliyokuwemo ambayo Serikali ya Marekani imeondoa hizo fedha. Kwa mnasaba huo huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipangaje kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hii miradi bado inaendelea baada ya kukosa ufadhili huu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, kwa *MCC Compact I* miradi iliyofadhiliwa ni mmoja wa *Submarine cable*, lakini vile vile kuimarisha kituo cha umeme Mtoni. *MCC Compact II* ilikuwa tupate jumla ya *US$* 40 milioni ambayo ni sawa na shilingi 80 milioni kwa ajili hiyo hiyo ya kusaidia kujenga uwezo wa *ZECO,* lakini vile vile kusaidia *distribution* ya *ZECO*. Lakini na tatu kusaidia sekta binafsi kushiriki katika sekta ya nishati ya umeme.

Nam. 144

Maswali ya Papo kwa Papo

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Mhe. Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mhe. Waziri Mkuu wa sasa Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa wamejenga heshima kubwa sana kwa wananchi wa Tanzania katika uongozi wao Bungeni kwa kujibu maswali ya hapo kwa hapo ndani ya Bunge.

Je, ni lini Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar atajibu maswali ya papo kwa papo Barazani angalau mara moja kwa mwezi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli katika Mikutano ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kila siku ya Alhamis wakati wa kipindi cha maswalina majibu, Mhe. Waziri Mkuu amepangiwa muda wa dakika 30 wa kujibu maswali ya papo kwa papo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mhe. Spika, utaratibu huu umeanza mnamo mwaka 2008 katika Bunge la Tisa la Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uliasisiwa na Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Kayanza Mizengo Peter Pinda na sasa unaendelezwa na Waziri Mkuu aliyepo madarakani Mhe. Kassim Majaliwa.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza utaratibu huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililazimika kubadilisha Kanuni zake ili utaratibu huo uanze kwa mujibu wa Kanuni zilizopangwa na kukubali na Wabunge juu ya kumuwezesha Mhe. Waziri Mkuu kujibu maswala haya.

Mhe. Spika, katika vikao vyetu vya Baraza la Wawakilishi bado tunaendelea na mfumo wetu ambao Waheshimiwa Mawaziri hujibu maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na bado tunaamini kwamba masuala hayo yanajibiwa kwa ufasaha bila ya kuacha shaka yoyote. Hadi sasa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haikuwa na mpango wa kuanzisha utaratibu wa maswali ya papo kwa papo. Hata hivyo, serikali inaweza kulitafakari shauri hili.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Mawaziri ambao kuwa Waheshimiwa Wawakilishi wamekosa kupata matamko ya serikali wakati linapotokea jambo la dharura na kwa kuwa kifungu cha 42 fasiri ya (1-9) ya Baraza la Wawakilishi kinakataa kupeleka hoja ya dharura nyingi kwa mara moja.

(a) Je. serikali iko tayari kubadilisha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 42 ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wawakilishi walete hoja za dharura mara kwa mara.(*Makofi*)

(b) Mhe. Waziri, imeonekana Makamu wa Rais anakosa nguvu au anakosa meno ya kuwaazibu baadhi ya wateule wa Rais ambao ni watendaji katika serikali hii. Je, na leo tunabadilisha Katiba katika *order paper* yetu tunaona. Serikali iko tayari kubadilisha Katiba ili kumpa nafasi Makamu wa pili wa Rais awe na nguvu ya kikatiba ya kuwaadhibi watendaji wakorofi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu mabadiliko ya kanuni ni mamlaka ambayo Baraza lako tukufu inayo.

Kwa hiyo, ni uamuzi wa Wajumbe wenyewe kuamua ni kanuni gani wanapenda ibadilishwe kwa mujibu wa makubaliano ya pamoja. Kwa hiyo, serikali haina pingamizi pale inapoona Wajumbe wanaona kuna haja ya kufanya mabadiliko ya kanuni.

Mhe. Spika, kuhusu Makamu wa Pili wa Rais kuwa hana nguvu za kikatiba na meno. Mhe. Spika, katiba yetu ukiitizama imempa nguvu kubwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kifungu cha 39 (7) ukisoma yeye ndie mshauri Mkuu wa Rais na ndie kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza hili. Kwa kuwa anakuwa mshauri Mkuu, naamini kabisa kwa lolote linaloweza kutokea na kumshauri Rais na Rais akiliona jambo hili linafaa anakubaliana naye na hasa hasa katika kupambana na watendaji wabadhirifu, ama wazembe ni imani yangu kabisa Mhe. Makamu wa Pili anao uwezo wa kusimamisha mtu kazi kwa muda na wakati huo huo akenda kushauriana na Rais ili mtu huyo kumsimamisha kazi.

Kwa hiyo, naamini katiba yetu inaweka nafasi kubwa sana, maana licha ya kuwa Mshauri Mkuu, lakini pia Mkuu wa shughuli za serikali hapa Barazani na hata katika kuteuwa Mawaziri katika kifungu 42(2) Mhe. Rais, anashauriana na Makamu wa Pili wa Rais katika kuchangua Mawaziri. Kwa hivyo, hapana shaka yoyote ikiwa wanashauriana kuchagua viongozi wakubwa kama hao katika serikali ana uwezo mkubwa sana wa kumshauri Rais jambo anaona linafaa na lenye maslahi ya nchi.

Mhe.Jabu Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nilikuwa nataka kumtoa wasi wasi tu kwanza afanye semina na Mawaziri wake na Manaibu Mawaziri kama anavyojibu maswali humu wapate kuwa na uzoefu zaidi afanye semina hiyo...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, nenda kwenye swali, kwa nini unatupa maelezo?

Mhe. Jabu Hashim Ayoub: Mhe. Spika, mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri, asiogope kujibu maswala ya papo kwa papo, hapo mbele pengine yatamjengea uwezo kwa nafasi aliokuwa nayo na akiweko mbele. Ulipokuwa ukijibu swali ulisema ushauri huu mtauchukuwa kazi kama serikali.

(a) Kwa nini usiwaachie Baraza ushauri huu baadae ukauchukuwa wewe kama Bunge lilivyo kule wameuchukuwa wenyewe na wakaufanyia kazi?

(b) Mheshimiwa, wewe ndie msimamizi Mkuu wa Serikali katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa mara ya pili mfululizo hii kanuni hizi zinakwenda zikarudi, kwa nini hazifanywi marekebisho ikafika pahali tukajua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa mara nyingi Mhe. Jaku Hashim, husema kwa haraka na hukiacha mbali hichi kipaza sauti inakuwa tabu kumuelewa. Lakini wacha nijaribu kama ndivyo nilivyomfahamu.

Kwanza ningependa aelewe mie sie Mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi, Mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mimi ni Waziri wa Nchi, nafanya kazi katika afisi yake, yeye ndie mwenye mamlaka ya mambo yote haya. Kwa hiyo, na kwa sababu maswala yanauliza serikali, sio mimi wa kutoa maamuzi kwenye mambo ya msingi ya serikali. Mambo ya msingi ya serikali lazima yarudi serikalini yakapimwe yaonekane faida na hasara zake.

Suala la papo kwa papo ukilitizama sana Mhe. Spika, ukilitiza sana ni la kisiasa zaidi, si la kimaendeleo katika nchi. Kwa sababu swala linapoulizwa wizara husika watendaji wanapata muda wa kutosha kwenda kulifanyia kazi na kuleta majibu yasiyo shaka. Mwanaadamu ni mwanaadamu hakuna mwanaadamu alietimia mia kwa mia, unapomuuliza swala la papo kwa papo akajibu kinyume na utaratibu na imeshawahi kutokea kwenye Bunge la Jamhuri la Muungano inaleta madhara makubwa katika nchi.

Kwa hiyo, sisi kwa upande wetu bado tunaona umuhimu wa kuheshimu yale mambo ambayo hayajatuletea madhara, unapokuwa na jambo zuri basi liendelezeni liwe zuri zaidi, si vizuri kulitia mtihani na kuliharibu. Lakini kama nilivyosema bado tutalichukuwa likatafakariwe ndani ya serikali na serikali ndiyo yenye uwamuzi wa mwisho kuhusu jambo hili.

Kuhusu maswala ya kanuni, Mhe. Spika, bado kanuni za Wajumbe na bado kanuni kwa kiasi kikubwa zinashughulikia ndani ya Baraza letu hili na uamuzi wa Baraza hili ambaye Mhe. Spika, ndiye msimamizi siku zote utaheshimiwa. Kwa hiyo, mimi wakati wowote nitakapokabidhiwa kusoma kanuni nitazisoma hapa na kuziwasilisha kama ambavyo mumezitaka zifanywe.

Lakini kwa sababu kulikuwa na ushauri wa maana sana kwa kuwa Mhe. Spika, aliona tufanye semina kwanza tuzipitie vizuri zile kanuni zetu, ndio maana tukaakhirisha na kikoa kinachokuja kanuni hizi zitaletwa mbele yenu ili ziweze kutekelezwa kama mnavyoona inafaa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Waziri, ukiacha maswala ya papo kwa papo ya kisiasa, lakini kuna ahadi nyingi za serikali zinaahidiwa na bado

utekelezaji wake ni mdogo. Je, huoni ukiweka maswala haya ya papo kwa papo yataweza kutatua mzozo huu na tukapata ufumbuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, bado kuna utaratibu mzuri uliowekwa na serikali katika kuhakikisha kwamba ahadi zinazotolewa na viongozi wetu wakuu zinatekelezwa na ni majuzi tu hapa Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alieleza kwamba, muda wa serikali wa kuwepo kwenye madaraka ni miaka mitano. Kwa hiyo, alitoa ahadi kwamba kila ahadi ya viongozi wetu wakuu itatekelezwa kama walivyozitamka na kuna utaratibu wa kiserikali na kiutawala kwamba, katika kila kiwilaya kuna mratibu wa shughuli za serikali ambaye hufatilia na kupokea ahadi zinazotolewa na viongozi wetu wakuu.

Kwa hiyo, utaratibu huu unasaidia sana kujua ahadi hizo. Lakini Mhe.Mwakilishi, huwezi kuwa na kikwazo cha aina yoyote wakati una ahadi katika jimbo lako usimwandikie rasmi Mhe. Makamu wa Pili. Kwa kumuuliza swala la papo kwa papo bado nasema tena haitosaidia sana kutatua tatizo kama utaratibu ambao uko sasa.

Nam. 1

Tija iliyopatikana kwa ziara ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mwezi Aprili, 2016, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ alifanya ziara mbali mbali ya kukagua masoko. Ziara hiyo inategemewa kuleta tija katika kuweka usafi wa masoko yetu ikiwemo soko la Mombasa, Soko la Kuku la Darajani pamoja na Mwanakwerekwe.

a) Kwa kuwa soko la Kuku Darajani linakabiliwa na mazingira machafu, Je, lini matatizo haya yatapatiwa ufumbuzi.

b) Soko la Mombasa pia linakabiliwa na tatizo la maji ya mvua kufurika wakati mvua zikinyesha na kuwa kero kubwa kwa wananchi, Serikali imechukua hatua gani za kuondoa tatizo hilo pamoja na pesa zinazokusanywa pale.

c) Je, wananchi watarajie faida gani zitakazopatikana baada ya ziara hiyo hasa kwa kuzingatia imekuja wakati nchi ikiwa na tatizo la

kipindupindu na kuathiri watu kadhaa kutokana na suala la usafi na Kanuni za Afya kutosimamiwa ipasavyo na watendaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ- Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Namba lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba mnamo mwezi wa Aprili 2016, nilifanya ziara ua kukagua masoko. Ziara hiyo inategemewa kuleta tija katika kuweka usafi wa masoko yetu ikiwemo soko la Mombasa, Soko kuu Darajani na Mwanakwerekwe.

Mhe. Spika, Ofisi yangu kupitia Baraza la Manispaa inaona umuhimu wa kuyapatia ufumbuzi matatizo ya soko la kuku Darajani na kuhakikisha linakuwa na mazingira mazuri ya kufanyia biashara kwa kulifanyia ukarabati mkubwa utakaofanywa katika kipindi hiki cha mwaka 2016 - 2017, michoro na kibali cha ujenzi kinatarajia kukamilika hivi karibuni.

b) Mhe. Spika, Katika soko la Mombasa, Baraza la Manispaa mjini na Baraza la Manispaa la Magharibi "B" yanaelewa tatizo la maji ya mvua liliopo ndani ya soko hilo. Hivyo, kwa kuanzia Baraza la Manispaa limeweka vigae vya zege katika sehemu za mnada wa ndizi, sehemu za njia na minada ili kuhakikisha maji ya mvua hayatuwami. Aidha, maeneo ya nje ya soko yaliyokuwa yakituama maji kipindi cha mvua yameshughulikiwa kwa kuwekwa kifusi.

Aidha, wafanyabiashara waliopo nje wameamriwa kuingia ndani ya soko ili kupunguza uchafuzi wa mandhari ya soko. Uendelezaji wa kuweka vigae maalum vya zege ndani ya soko unaendelea.

c) Mhe. Spika, Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kujua changamoto za usafi wa mazingira katika maeneo ya masoko, kuelemisha jamii juu ya umuhimu wa kuweka mazingira safi na kuheshimu Sheria na Kanuni za usafi wa mji ili kuweza kukabiliana na matatizo ya maradhi ya mripuko. Faida kubwa iliyopatikana ni pamoja na utayari wa wafanyabiashara na wananchi kusafisha maeneo yao ya biashara na maeneo yaliyowazunguka kwa usafishaji wa mitaro ya maji ya mvua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Mhe. Spika, nani mwenye wajibu wa kusimamia usafi wa afya katika masoko baina ya mfanyabishara na serikali.

(b) Mhe. Spika, kwa nini masoko yetu yatoe huduma katika mazingira machafu wakati kuna watu wanalipwa mishahara na stahiki zao. Ni sababu gani anaweza kueleza na nikuombe tu utakapofanya ziara kipindi chengine ukanialika na mimi tukashirikiana ili nikakuone maeneo mengine Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ:-

(a) Mhe. Spika, wajibu wa kuweka usafisi katika masomo yetu, kwanza ni kwa yule mfanyabiashara mwenyewe kutunza mazingira yake katika eneo lile ambalo anafanyia biashara ili awaridhishe wateja wake.Wajibu wa Baraza la Manispaa kuhakikisha kwamba huo usafi unaimarishwa kwa kusafisha masoko na kuyaweka katika mandhari nzuri.

(b) Mimi sina tatizo na kukualika Mhe. Jaku Hashim, kufatana na mimi katika ziara. Ila nitakuomba siku nitakayofanya ziara kama utakuwepo nchini basi nitakualika. Sina tatizo hata kidogo. (*Makofi*)

Mhe.Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri, kwa kujitahidi sana katika mazingira haya.

Lakini kitu ambacho nakiona Mhe. Waziri, amekuzungumza kwamba, wale wafanyabiashara wadogo wadogo wanahamishwa nje na wanahamia ndani. Lakini ukienda ndani kwenye masoko yale utakuta mtu ana tangawizi mbili na vitu gani viwili anaviweka pale na wakati huo huo unamkuta mtu mmoja ambaye anakusanya pesa anakusanya kwa yule mtu ambae ana tangawizi mbili, ana keroti mbili, sasa suala langu lipo hapa.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kupanga mipangilio ambayo ya kisasa tukaachana na matatizo yale ambayo mtu mle ndani ana tangawizi mbili mbili.

(b) Serikali haioni kwamba kuchukuwa pesa yake yule mtu ambaye ana tangawizi mbili na baadae watu wale kwa sababu mazingira yale yanahatarisha afya na kila kitu. Lakini ni kupalilia watu wale kuongezeka na baada ya kuongezeka watu wale wanatimuliwa. Hawaoni watu wale kama wanakuwa wanawaonea kwa sababu wanachukuwa pesa yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ: Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waelewe kwamba, unapoamua kufanya biashara na kuyatumia maeneo ya Mabaraza ya Miji au Halmashauri au Manispaa;iwe ni masomo, iwe ni maeneo mengine yaliyotengwa rasmi katika kufanya biashara huko lazima uchangie kwa maana ya kulipa ada ili vyombo hivi ziweze kuetekeza majukumu yake ipasavyo.

Hata hivyo, kwa hiyo, inazingatia biashara gani unaifanya kama unafanya biashara ndogo ya thamani ndogo unatozwa kidogo, kama unafanya biashara kubwa unatozwa kikubwa. Hata hivyo, serikali ina mpango madhubuti sana wa kuweza kuwajengea mazingira mazuri wafanyabiashara wadogo wadogo ili waweze kufanya biashara zao na waweze kukuza biashara zao kupitia mifuko mbali mbali ambayo serikali imeiweka.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, pamoja na mkakati uliowekwa kupitia Wizara ya Afya na Tawala za Mikoa juu ya kuangamiza gonjwa la kipindupindu Zanzibar. Lakini katika masoko yetu bado kuna mpango wa wafanyabiashara wale kutandika magunia chini wanauza matunda na pale panabakia maji maji inakuwa ni sababu moja ya kusababisha maradhi katika vyakula vile.

Je, serikali inatoa tamko gani juu ya uzuiaji wa wafanyabiashara wadogo wadogo kutumia magunia sehemu za nje ili wawe na vibaraza vizuri kwa ajili ya shughuli zao za biashara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Jang'ombe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza tunapokea pongezi Wizara ya Afya na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara za SMZ kwa mashirikiano na wananchi kulitokeza gonjwa la kipindupindu. Mheshimiwa, Serikali haipendi hata kidogo. Serikali kupitia taasisi zake; Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, kwanza kusegana na wananchi wetu wale ambao wanajifanyia biashara kinyume na yale maeneo ambayo yamepangwa na Serikali.

Kwa hivyo, sisi tungependa zaidi wafanyabiashara wadogo wadogo wakafanya biashara kwenye maeneo maalum *slabs* zile (vibaraza) ambavyo vimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo. Na kila tunapojaribu kuchukua hatua ya kutaka kuwaondosha watu hao, niseme Mhe. Spika, baadhi ya Wajumbe wako, Baraza hili hili la Wawakilishi wanatuona kwamba tunawaonea wafanyabiashara hao.

Sasa sisi tunalinda afya za wananchi wetu. Kwa hivyo, tunaliomba Baraza hili Tukufu na Wawakilishi wote kama hili jambo Mhe. Abdalla Maulid Diwani, analiona siyo sawa na sisi Serikali tunaliona si sawa, tunapofanya zoezi la kuwaondosha wafanyabiashara hawa Baraza lako Tukufu na Wajumbe wake waiunge Serikali na wala wasituone kwamba tunawaonea wafanyabiashara hao. (*Makofi*)

Nam. 4

Uuzaji wa Samaki Katika Eneo la Kambi ya KMKM - MSUKA

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa usalama katika Kambi za vikosi vya ulinzi ni suala muhimu ambalo Serikali inapaswa kulipa uzito wa hali ya juu. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi bahari imekula sehemu kubwa ya ardhi kwenye diko la Msuka ambapo kumekuwa na shughuli za uuzaji wa samaki mbele ya kambi ya KMKM. Na kwa kuwa shughuli hizo za uuzaji wa samaki zimekuwa zikifanywa kutokana na kutokamilika ujenzi mpya wa soko la Msuka ambalo ujenzi wake hadi hivi sasa umefikia asilimia 90 kukamilika kwake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulikamilisha soko la Msuka ili wavuvi wa soko hilo waweze kuondoka katika maeneo ya kambi na kufanya shughuli zao sokoni hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Namba 4 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa hivi sasa uuzaji wa samaki katika diko la Msuka unafanyika katika eneo la Karibu na Kambi ya KMKM kutokana na sehemu ya diko hilo kuliwa na maji ya bahari kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Shughuli hizi za uuzaji wa samaki zinafanyika eneo hilo baada ya kutokamilika kwa ujenzi wa soko katika diko la Msuka.

Mhe. Spika, kwa kuwa ujenzi wa Soko hilo unagharamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kazi hiyo inatarajiwa kuendelea na kukamilika mara tu baada ya kuingizwa fedha hizo na Kamati kuidhinisha matumizi yake ili kuwaondoshea usumbufu wananchi na kuimarisha utunzaji wa mazingira.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, mimi ninashukuru kwa jibu zuri sana la Mhe. Waziri. Nilikuwa na swali (a), (b) na (c), lakini nimeyafuta nimeacha kitoto kimoja kidogo.

Kwa kuwa nimemuomba Mhe,Waziri aende kujionea mwenyewe hali halisi iliopo hapo ya uchafuzi wa mazingira uliosababishwa na mabadiliko hayo ya tabianchi. Sasa mimi naomba aniambie ni lini atafanya ziara hiyo ya kwenda kujionea hali halisi ya mabadiliko yaliyotokea kwa ajili ya kuinusuru kambi hiyo. Lini atafanya ziara hiyo naomba aniambie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza ninataka nimthibitishie kabla Baraza kwenye kipindi cha Baraza lililopita nilifanya ziara na kujionea mwenyewe hali halisi ya uchafuzi wa mazingira katika eneo hilo kutokana na tabianchi. Hata hivyo, ninataka nimuhakikishie kwamba kabla ya Baraza lijalo la Wawakilishi kati ya mwezi wa Disemba au Januari, nitakwenda ziara na yeye nitamualika ili tujue namna gani tunaweza tukalishughulikia jambo hilo. (*Makofi*)

Lakini kwa taarifa ya Baraza lako Tukufu Kikosi cha KMKM kinao mpango madhubuti wa kuweza kununua mawe na kwenda kuyaweka katika maeneo yale ambayo yameharibika kutokana na uchafuzi wa mazingira uliotokana na tabianchi.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nipate swali moja la kumuuliza Mhe. Waziri.

Kwa sababu soko la Kengeja lipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ni lini soko hilo litajengwa hapo Kengeja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Moh'd Mgaza Jecha, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano. Na katika kipindi hichi cha miaka mitano Baraza la Mji la Mkoani litaweka katika mipango yake ya kumalizia soko hilo kwa mujibu wa hali ya fedha itakavyopatikana. Lakini ndani ya kipindi cha miaka mitano tutahakikisha

kwamba hilo soko linajengwa ili Ilani ya Chama cha Mapinduzi iweze kutekelezeka. (*Makofi*)

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa vile malalamiko ya masoko yamekuwa ni mengi katika nchi yetu Unguja na Pemba, lakini Micheweni upo ujenzi wa soko ambao takriban umechukua muda mrefu na haujakamilika na Mhe. Waziri, ambaye mwenye dhamana ya kama ya kwako aliyepita aliweza kuweka ahadi eneo lile kwa kutaka kusaidia mifuko ya saruji kwa kiwango ambacho kilitajwa na kwa sasa yeye hayupo hayupo kwenye majukumu.

Naomba majibu ya Serikali juu ya hatua hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maluum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Shamata, swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ahadi aliyoweka Waziri aliyepita ni ahadi ya Serikali. Kwa hivyo, kama hiyo ahadi tutaifuatilia na Serikali tutaweza kuitekeleza. (*Makofi*)

Nam. 83

Ujenzi wa Hospitali Mpya Bungi

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Serikali imepanga kujenga hospitali mpya Binguni kuweza kuwasadia wananchi hasa wa Mkoa Kusini kupata matibabu ya afya.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haifanyi bidii ya makusudi kuanza mchakato wa kuwaelimisha wananchi wa maeneo ya karibu katika fursa za kazi hasa wa maeneo ya Tunguu, Jumbi, Binguni, Mtakuja na Dunga ili na wao wawe katika mstari wa mbele katika kufaidika na hizo ajira.

(b) Ni mkakati gani serikali inaweza kutekeleza katika hizi ajira wakati wa ujenzi unapofanyika kuhakikisha kuwa watu wa maeneo ya Jimbo la Tunguu wanafaidika na hizi ajira.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa na afya njema na wazima katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Simai Mohamed Said, swali lake Nam. 83 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Afya ina mpango maalum wa kujenga hospitali kubwa ya rufaa huko Binguni na jitihada kubwa hivi sasa inafanywa ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo pamoja na mazungumzo mbali mbali na wafadhili ambao yanaendelea.

b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi ya kwamba,pindipo matayarisho ya ujenzi yakikamilika, Serikali itawaarifu wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja hususan maeneo ya Tunguu, Jumbi, Binguni, Mtakujana na Dunga kutoa mashirikiano yao na pia tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote wa Mkoa wa Kusini wakati huo kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa za ajira ambazo zitakazojitokeza kwenye ujenzi huo utapoanza.

Mhe. Spika, napenda kuweka wazi kabisa kwamba Wizara haiwezi kutoa ahadi za moja kwa moja kuhusiana na ajira, kwani ajira zote zinatolewa na mamlaka husika kama Sheria ya Utumishi inavyojieleza. Aidha, upatikanaji wa ajira kwa wananchi utategemea pia na makubaliano yatakayowekwa baina ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na mkandarasi atakayepatikana. Hata hivyo, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wake wa maeneo hayo wanapatiwa ajira kuzingatia fursa zilizopo na masharti hayo yatazingatiwa katika mkataba utakaosaniwa na mkandarasi atakayechaguliwa.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa majibu ambayo aliyotoa ni katika majibu mazuri niliyosikia hapa kwenye maswali mengi niliyouliza, kwa hivyo, ninampongeza sana.

Nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza Mhe. Spika. Swali langu ni kwamba kama alivyotaja kuwa Serikali itahakikisha wananchi hawa watafaidika katika mradi huu mkubwa wa hospitali itakaojengwa. Swali ni kwamba wakati zabuni zinapotolewa hizi za ma-*contractors* wanakuwepo na wale *main engineers*, *subconsultants*, watu wa fundi wa umeme na wengineo.

a) Je, Wizara yake haioni umuhimu katika kutaka hii zabuni kuhakikisha kwamba watakuwa na kifungu kidogo kuhakikisha kuwa katika zile kazi ndogo ndogo zitakazojitokeza kwenye hilo eneo wananchi wangu hasa katika maeneo niliyotaja Dunga, Binguni, Mtakuja, Jumbi na Tunguu wanafaidika na hizo ajira wakati zabuni zinapotolewa.

b) Lakini pia katika mradi huu utakapokwenda katika mazingira hayo utakapojengwa kujengwa hiyo hospitali, hili eneo linalojengwa hospitali ni eneo ambalo linatumika kwa mambo ya kilimo. Swali ni kwamba katika kulinda mazingira na uchafuzi utakaotokana hasa masuala ya sindano, Madawa pengine na mambo mengine ambayo yanayotumika kwenye hospitali. Je, ananihakikishia kwamba uchafuzi wa mazingira na katika mpango mzima wa kujengwa hospitali hiyo atalilinda lile eneo kama lilivyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa naomba nimshukuru sana kwa pongezi zake na pongezi hizi pia tunaendelea kuzipokea kama Wizara ya Afya.

a) Mhe. Spika, ni kweli kabisa kifungu kidogo kinakuwemo mara nyingi katika mkataba wa mkandarasi. Na mfano mzuri ni katika mkataba uliotiwa saini katika Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba, kifungu kidogo hicho kipo na kimezingatia wenyeji wa maeneo ya pale ambao walipewa kazi ndogo ndogo pamoja na akinamama kazi za maji na mambo mengine kama hayo. Kwa hivyo, kifungu hicho kinakuwepo mara nyingi sana katika mikataba ambayo tunasaini na mkandarasi.

b) Lakini kuhusu hili eneo la pili, tayari eneo hili limezingatiwa. Tunaelewa kwamba lile eneo ni la kilimo zaidi, tunaelewa kwamba eneo lile lina rutba kubwa ni *green*. Hili limezingatiwa zaidi kwenye *feasibility study* na katika ramani. Pale katika ramani ukiangalia ya Binguni kubwa ambayo na hospitali imetayarishwa ndani imetiwa mpaka ziwa. Kwa hivyo, kuna *green area*, kuna *lake side* humo humo ndani ya hospitali ili wagonjwa nao wapate kuvutika, kwa sababu ni sehemu ya tiba kuwa na picha zote za kijani. Kwa hivyo, eneo la mazingira limezingatiwa na eneo la kupandisha miti na kuweka eneo kuwa zuri na la kuvutia, pia nalo limezingatiwa katika *feasibility study*.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, nichukue fursa kumpa pongezi

kubwa sana yeye na Naibu Waziri wake kwa kufanya kazi kwa jitihada kubwa sana. (*Makofi*)

Kwa sababu kuwa Hospitali ya Binguni inakaribia kujengwa, lakini tulipokea barua mbali mbali ikiwemo Jimbo la Mpendae kujenga hospitali ya Wilaya. Je, ninataka kuuliza swali lile limefikia wapi mpaka sasa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ninashukuru sana kwa kuleta swali kwa sababu anazidi kukumbushia. Ni kweli mpango huo upo. Upo kwa hapo Mpendae pia upo pale Mbuzini ambayo ni ahadi ambayo imetolewa na Mhe. Rais, mwenyewe. Hivi sasa tunajaribu kukamilisha maeneo makuu ambayo tunayo Hospitali ya Abdalla Mzee pamoja na mradi wa *ORIO* ambao pale Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na ule mradi wa Norway wa hospitali ile ya watoto *extension* ya Mnazi Mmoja.

Tukishakamilisha huko basi hatua zitakazofuata ni kuelekea Mbuzini na hiyo kuipandisha hadhi hospitali ya Wilaya. Bado tunaendelea kufanya mazungumzo na hivi karibuni tu tutafanya ziara katika maeneo yote hayo mawili: Mbuzini pamoja na Mpendae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri, jambo dogo.

Ninamshukuru sana Mhe.Waziri, kwamba anajitahidi kuendeleza mahospitali na kujenga mahospitali mapya. Hasa hospitali kubwa ya kisasa ambayo ipo Mkoani Pemba. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuuliza Mhe. Waziri kwamba, muda mwingi anapiga kelele kuwa wafanyakazi hawatoshi. Sasa hivi hospitali ile inahitaji wafanyakazi wengi.

(a) .Je, amejiandaaje angalau kupata wafanyakazi waliokuwa wameshapata uzoefu wa miezi sita ndiyo wakaingia kwenye hospitali ile ukiachia wanaotoka Vyuoni *fresh*.

(b) Lakini ana uhakika gani ya kwamba Hospitali ya Mkoani haitokuwa na usumbufu na wafanyakazi ambayo ni hospitali mpya ya kisasa inayotakiwa ioneshe mfano.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwanza ninamshukuru sana kwa swali zuri alilioliuliza. Mhe. Spika, hivi sasa tupo katika hatua za mwisho kabisa za kupata kibali cha Serikali za ajira takriban mia nne hamsini jumla yake. Kwa sababu kuna mradi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, kuna mradi *ORIO* na kuna mradi wa Norway.

Katika hicho kibali kitakachopatikana matangazo yatatolewa kwa ajili ya ajira ambayo nafasi nyingi zitakuwa nyingi zitakuwa ni za kiwango hicho kinachotakiwa. Maana *MD, Doctor of Medecine* na manesi na wengi ni wataalamu, yaani *skill labour*. Kwa hivyo, mara tu tutakapokamilisha tunaamini kwamba wafanyakazi watapatikana wazoezi.

b) Kuna mpango pia ndani ya Wizara ambao umeandaliwa kuwachukulia wale wazoefu wachache kuwaleta pale Hospitali ya Abdalla Mzee na hao wengine watakaochukuliwa wataweza kujaza nafasi zao.

Kwa hivyo, naomba nimtoe hofu kabisa kwamba Hospitali ya Abdalla Mzee itakapofunguliwa rasmi na sasa hivi hatua ya makabidhiano zinaendelea, itakapofunguliwa rasmi itakuwa *In shaa Allah*, hakuna uhaba wa wafanyakazi na vifaa vilivyokuwepo pale vya kisasa kabisa.

Lakini Mhe. Spika, naomba nitoe fursa hiyo hiyo tumeshaamua kama Wizara mara hii tutawaalika Wawakilishi pamoja na wewe Mhe. Spika, ukiwaongoza kuja kule Pemba katika ufunguzi rasmi utakaofanyika wa Hospitali Abdalla Mzee.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Nam. 137

Kupiga Marufuku Uingizwaji na Matumizi ya Pempasi

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Ali Khamis Bakari) - Aliuliza:-

Suala la pempasi limeonekana kuwa kadhia kubwa kwa nchi na wananchi pamoja na mazingira licha ya kuwa ni biashara kubwa ambayo inaingiza pesa nyingi, Serikali pamoja na wafanya biashara.

Ni chanzo kikubwa cha maradhi ya kipindupindu kwani pempasi hizi hurembewa ovyo katika mitaa ikiwa ina kinyesi.Na inaonekana kuwa zinachangia uharibifu wa mazingira na kuwafanya watu wawe wavivu wa kutunza na kuwatunza watoto.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na pempasi.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar, swali lake ambalo limeulizwa na Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kuwa ueneaji wa pempasi mitaani pamoja na kwenye majaa mbali mbali ni kero na linachangia moja kwa moja na sehemu kubwa wa uchafuzi wa mazingira ambao pia unapelekea kuleta miripuko ya maradhi ya kuharisha na kipindupindu hasa ukitilia maanani kuwa kinyesi cha watoto wadogo kina uwezekano mkubwa katika kuchangia maradhi ya kipindupindu.

Mhe. Spika, suala hili la kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na pempasi si la Wizara ya Afya peke yake kama inavyosemekana mara nyingi, bali ni suala letu sote na linahitaji mashirikiano makubwa sana. Kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwamba, jambo hili tunashirikiana na wao kwa karibu sana na ndiyo maana tukafanikiwa kuwa na hali hii, maana hali ilikuwa mbaya sana huko tunakotokea ya kipindupindu. Kwa hivyo, tunachokiomba sisi Mhe. Spika, kwa upande wetu serikali sisi tunaendelea kushirikiana na taasisi mbali mbali, ikiwemo Mabaraza ya Manispaa pamoja na Halmashauri. Lakini tunaomba sana kwamba elimu kubwa zaidi inahitaji bado kuendelea kutolewa katika kutupa hizi pempasi na elimu hiyo ni jukumu letu sote pamoja na wawakilishi.

Mhe. Spika, vyombo vya habari navyo pamoja na ile michezo ya kuigiza, imekuwa ikitusaidia sana na sehemu kubwa sana katika kutoa elimu kwa jamii. Naomba tuvishukuru sana vyombo vya habari kwa kutusaidia kutoe elimu hiyo. Aidha, elimu zaidi inahitajika kutolewa kwa jamii na kuwekwa mazingira mazuri ya uhifadhi wa pempasi hizo baada ya kutumika. Kwa hivyo, naomba sana hili suala liwe na mashirikiano baina yetu sote, kwa upande wa serikali inatimiza wajibu wake, lakini na kwa upande wa wananchi nao lazima na wao watimize majukumu yao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sauti zenu zinanifika huku sasa hivi, mngepunguza kidogo. Baada ya hapo naomba sasa nimuone tena Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, kwa swali la nyongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika historia ya nchi yetu maradhi ya kipindupindu yalichukua muda mrefu sana hapa Zanzibar, ambapo kwa asilimia kubwa wananchi wote wa Zanzibar kwa Unguja na Pemba tulishtuka. Lakini kwa kuwa chanzo kikubwa inasemekana ni uchafu wa mazingira yetu, lakini pia usalama mdogo wa hizi pempasi inavyosemekana.

Je, Mhe. Waziri, mara baada ya kutokea maradhi haya na katika tafiti zao walizofanya na kwa kuwa maradhi haya yalienea nchi nzima kwenye maeneo mbali mbali ambayo hayajapata kutokea, wamethibitisha vipi ni kitu gani hasa kilichosababisha mpaka mripuko huo uka mkubwa na wa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika uchunguzi wetu mkuu uliofanyika wakati wa mripuko huo wa mwisho, kila mripuko umekuja na uchunguzi wake na kila mripuko umekuja na sababu zake. Katika uchunguzi huo ile ripoti hatuitumii sisi tu, lakini mpaka Umoja wa Mataifa wanakuwa wanaihitaji, lazima ripoti ile iwasilishwe Umoja wa Mataifa, kwa sababu Zanzibar yakiendelea maradhi yale yanakuwa *declared* kama *cholera zone*, ikishakuwa *declared cholera zone*, hata utalii unakuwa unapungua. Kama ilivyokuwa huko nyuma siku za maleria. Sasa hivi tuna *less than 1%*, kwa hivyo, ndio maana utalii wetu umeongezeka. Kwa hivyo, ikiwa *declared cholera zone* inakuwa ni tatizo, ndio maana ripoti hiyo ilibidi iwasilishwe.

Mhe. Spika, katika uchunguzi uliofanyika zimegundulika sababu tatu kuu. Nasikitika kusema kwamba sababu ya kwanza kabisa ilikuwa ni ujenzi holela na kuziba njia za maji. Watu wengi hawafahamu ujenzi holela na kuziba njia kuu za maji ya mvua yanapopita wanakwenda kwenye kipindupindu. Unapozuwia njia kuu ya maji kupita, maji yale ya mvua huzoa majaa yale pamoja na zile pempasi, ikawa kile kinyesi kinachukuliwa na kinasambazwa kwa eneo kubwa sana, ambalo kile kinyesi kinaweza kutokezea pengine huko Magogoni kikafika mpaka kwenye ziwa lile la Mwanakwerekwe pale sokoni.

Kwa hivyo, hiyo ndio sababu kuu ya mwanzo kabisa na timu hiyo ilikuwa sio sisi tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni timu ambayo ilikuwa sisi pamoja na wataalamu kutoka Umoja wa Mataifa Shirika la Afya Ulimwenguni. Kwa hivyo, sababu kuu ya mwanzo ilikuwa ni maji ya mvua hayapati kwenda na ndio yanasababisha, na ndio maana maradhi haya mara nyingi huwa wakati wa mvua yanapanda zaidi.

Lakini sababu kuu ya pili, ilikuwa nyumba takriban 44 katika ukanda ule, sisi tunaita ukanda wa hatari, ambao unaanzia Darajabovu unakwenda zake mpaka Bububu, unakuja mpaka Fuoni na Jimbo la Mhe. Ali Suleiman Ali, limo pia katika ukanda huo. Sababu kuu ya pili, ilikuwa nyumba 44 hazina vyoo kabisa, yaani vile vyoo vya kuchimba, na yote hayo yametokana na kwamba watu walivamia maeneo kujenga bila ya vibali na ndio maana hakukua na nafasi ya vyoo. Kwa hivyo, hiyo ilikuwa ni sababu kuu ya pili.

Sababu kuu ya tatu, ilikuwa ni haya majaa yasiyorasmi, kwa sababu jaa rasmi huwa unawekewa kontena na taka zote pale hutupwa, ni yale majaa ambayo wananchi wanaona kiwanja kitupu basi wanaanzisha tu jaa pale. Hizo ndio zilikuwa sababu kuu tatu, na ndio maana tukazifanyia kazi. Lakini nyengine zilizofuata ni hiyo pamoja na vyakula, kuweka makabati, usafi na siku hizi mnawaona wauzaji wanavyaa makoti mazuri meupe na kadhalika. Hiyo ilikuwa ni kwa sababu kile kipindupindu kisiendelee, ndio ikabidi tuzuwie upande huo ili kile kipindupindu kisiendelee zaidi, kwa sababu mripuko ulikuwa mkubwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, majibu yamekuwa marefu sana ingawa ni mazuri sana, kwa hivyo, ningeshawishika tuendelee. Katibu.

Nam. 23

Kutofanya Kazi kwa Visima Vipya vya Maji

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na nchi ya Ras al Khaimah imechimba visima viwili katika Shehia ya Misufini (Bumbwini). Hata hivyo, ni muda mrefu sasa visima hivyo bado havijaanza kufanya kazi, jambo ambalo limewafanya wananchi wa shehia hiyo kuendelea kupata usumbufu kutokanana tatizo la upatikanaji wa maji katika shehia hiyo.

(a) Ni sababu gani zilizopelekea visima hivyo kutokamilika na kuanza kutumika.

(b) Wizara yako imechukua hatua gani za haraka za kuhakikisha kuwa visima hivyo vinaanza kufanya kazi ili kupunguza tatizo sugu la maji katika shehia hiyo.

(c) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu, Je, ni lini hasa visima hivi vitaanza kufanya kazi rasmi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 23 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Naomba ifahamike kwamba Mradi wa Uchimbaji wa Visima unaofadhiliwa na Ras al Khaimah, imefanyakazi ya uchimbaji visima, ununuzi wa *pumps* na ujenzi wa matangi sita tu kwa visima hivyo. Kazi zilizobakia za ulazaji wa mabomba yaliyobakia, upelekaji wa umeme, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu na nyenginezo, ambazo zinakamilisha mradi hadi kumfikia mwananchi kupata maji, zinalazimika kuendelezwa na kufanywa na serikali kwa kushirikiana na uongozi wa majimbo.

(b) Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji tayari imeshafanya makisio ya kazi hizo kwa visima vyote vilivyochimbwa na Ras al Khaimah ambavyo bado havijaanza kutumika. Aidha, jumla ya visima 12 kwa Unguja na Pemba tayari vimekwisha endelezwa kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kushirikiana na uongozi wa majimbo husika. Visima hivyo ni Kinduni, Makunduchi, Uwelezo, Mwanakwerekwe, Chumbuni kwa Unguja na Chambani, Mahuduthi, Mtambile, Mfikiwa, Mkanyageni, Chuguni Wingwi na Kwachangawe kwa Pemba, ambalo tayari zinahudumia wananchi.

Kwa upande mwengine visima saba, ambavyo ni Bambi, Uroa, Welezo na Michungwa Miwili kwa upande wa Unguja, na Finya Mbuzini, Kengeja na Ngwachani kwa Pemba, kazi za uendelezaji wake zinaendelea vizuri.

Aidha, napenda nichukuwe fursa hii kuupongeza uongozi wa majimbo ambao umefanya jitihada ya kuviendeleza visima katika majimbo haya. Lakini pia nichukuwe fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi, waliobakia na wao kusaidia jitihada za serikali, kwa kuviendeleza visima hivyo, kama ambavyo wenzetu hawa wamefanya, ili kuona kwa pamoja tunawaondolea shida inayowakabili wananchi wetu wakiwemo wananchi wa Shehia ya Misufini Bumbwini, ili kusaidia hali ya upatikanaji wa huduma ya maji.

(c) Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, visima vilivyochimbwa na Ras al Khaimah ambavyo bado havijaendelezwa vikiwemo vya Shehia ya Misufini, vitaendelezwa kwa kadri uwezo wa serikali utakavyoruhusu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa vile serikali imepata fedha nyingi kutoka India kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hii ya maji.

(a) Je, kwa nini fedha hizi zisielekezwe kumalizia visima hivi vilivyochimbwa na Ras al Khaimah, tukishirikiana na watumishi wa majimbo ili kuwaondoshea wananchi kero hii ya maji.

(b) Kuna tetesi kuwa hivi visima vilivyochimbwa na Ras al Khaimah, mashimo haya yalikuwa kwenye utafiti wa kutafuta mafuta, badala yake walivyokua hawakupata mafuta, basi mashimo haya wakayawacha. Je, ni nini kauli ya serikali juu ya uvumi huo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

(a) Mhe. Spika, sio kweli kwamba tumepata na tunaendelea kupata fedha, lakini fedha zozote ambazo zinakuja, basi zinakuja kwa masharti yake maalum. Sasa fedha hizi ambazo tumezisikia zinakuja, zimefanyiwa *feasibility study* ya wapi ziende zikatumika.

Lakini hata hivyo, ushauri mzuri tunauchukua na tutazinga kwa kadri yali itakavyokua inaruhusu kufanya maamuzi.

(b) Linasema, Je, visima hivi vimefanya utafiti kwa ajili ya mafuta, sio kweli. Hii ni misaada maalum kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi naipongeza sana serikali kwa jitihada zake inazofanya siku hadi siku, ili kuhakikisha kero la maji linaondoka katika kero la nchi yetu.

Jambo moja ambalo tunashuhudia kwamba mradi huu mkubwa uliotoka Ras al Khaimah wa kuchimbiwa visima kadha, ambapo ni mwelekeo mmoja wa kuhakikisha kwamba tatizo la maji linaondoka katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kuchimba maji ni rahisi, lakini kusambaza maji ndio shida. Je, kwa kuwa wafadhili walikuja kwa nia njema ya kusaidia visima hivi, wachimbe halafu wasambaze. Mawazo yangu, kwa nini wizara ilitulia na isiwaambie kwamba kuchimba maji ni njia moja na kusambaza maji ni njia ya pili. Hivyo hawaoni kwamba tatizo hili linatupa gharama kubwa sana la kusambaza, yaani kuchimba ni rahisi kuliko kusambaza. Ndio hadi leo visima hivyo havijasambazwa maji na mimi ni mmoja wapo katika visima vyangu vya Jimbo langu la Kijitoupele, kutoka Tomondo Uzi pamoja na hapa Taveta ambapo visima vimekaa vinatizama macho havijafanyakazi yoyote hadi leo wananchi wanapata shida.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kwamba anayekusaidia anaangalia naye uwezo wake wa kukusaidia. Wewe unayesaidiwa huwezi kumlazimisha kuwa ili unisaidie ni lazima unikamilishie hivi. *Something is better than nothing.* (*Makofi*)

Mhe. Spika, hapo palipobakia, aidha, tukipata mtu wa kutusaidia au sisi wenyewe tutaendeleza ili kuhakikisha kwamba tunaikamilisha hii kazi, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji kila kukicha wanapata misaada, lakini bado tatizo la maji linaongezeka, hususan maskuli wanafunzi wanapata dhiki ya maji sana.

Je, ni lini mtawaondoshea dhiki ya maji wanafunzi maskulini kwa adha hii inayowakabili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna usumbufu wa upatikanaji wa maji kwa baadhi ya maeneo na hasa baadhi ya maskuli. Lakini tuone kwamba mahitaji ya maji kila siku yanaongezeka, kwa sababu idadi ya watu kila siku inakuwa, licha ya misaada ambayo tunaipata na ambayo mnaisikia, lakini pia kuna kazi za msingi ambazo zinafanyika zikiwa na lengo la kusaidia ama kutatua utatuzi huo. Kwanza tunafanya shughuli za kuondoa miundombinu ya zamani, maeneo mengi miundombinu yake kabla ya wengi wetu sisi hatujazaliwa.

Kwa hivyo, tusione kwamba linachukuliwa na linafanyiwa mambo ambayo hayahusiki. Lakini niseme kwamba tushirikiane sote kwa pamoja tutafika, ahsante sana.

Nam. 97

Upungufu wa kiwango cha Dawa ya Kinga katika Maji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Shirika la Afya Duniani limesema kiwango cha dawa ya kinga kinachowekwa kwenye maji, katika kukabiliana na maradhi ya milipuko kinawekwa kiwango cha chini, kinyume na matumizi yake na kusababisha kila mara kujitokeza maradhi ya kipindupindu

(a) Kwa nini Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inashindwa kuweka kiwango cha dawa ya kinga kwa kuzingatiwa viwango vinavyotakiwa.

(b) Je, ni hatua gani *ZAWA* inachukua juu ya vyanzo vya maji kuchafuliwa na taka maji na taka ngumu katika kulinda vyanzo vyake vya maji.

(c) Kama *ZAWA* inaweka dawa ya kinga katika maji kabla ya kuwafikishia wananchi, kwa nini wananchi hao hao wanatakiwa kuyachemsha maji kabla ya kuyatumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika,

(a) Mhe. Spika, serikali kwa kupitia Mamlaka ya Maji, haijashindwa kuweka kiwango cha dawa ya kinga kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa. Kiwango kinachowekwa katika maji cha wastani wa 0.2 hadi 0.6, ni muafaka kwa ajili ya matumizi ya binadamu. ZAWA inajitahidi kuweka dawa katika vianzio vyake, kwa kupitia matangi kama ya Saateni, Welezo, Kinuni na Dole ambavyo ndivyo vinavyotiririsha majihayo kwenda kwa watumiaji.

Maji yanayotoka katika visima moja kwa moja, huwa hayawekwi dawa, kwa sababu visima virefu havitegemewi kuchafuka. Hata hivyo, *ZAWA* inafanya uchunguzi na ukaguzi wa visima hivyo mara kwa mara, ili kugundua kama kuna vimelea vyovyote vinavyoweza kusababisha maradhi.

Pia, kunakuwa na wimbi kubwa la vianzio binafsi ambavyo vimechimbwa kinyume cha utaratibu na maeneo ambayo hayako salama, na ambayo

hupelekea kuchanganyika na maji ya karo au mtandao wa maji machafu. Hata hivyo, Mamlaka ya Maji inajitahidi kutoa matangazo, kwa kuwataka wananchi wenye visima binafsi kuja kwenye Mamlaka ya Maji ili kupata dawa ya kutibu maji katika visima hivyo. Lakini hata hivyo, wengi wao huwa hawajitokezi kama inavyopasa kufuata wito huo.

(b) Mamkala ya Maji inafanyakazi kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali, ikiwemo Wizara ya Afya, Baraza la Manispaa, Ofisi za Wilaya, Taasisi za Mazingira, Wizara ya Kilimo, katika kuvilinda na kuvihifadhi vianzio hivyo kutokana na kuchafuliwa na maji taka na maji ngumu.

Aidha, Mamlaka ya Maji inaendelea na utoaji wa taaluma kwa wananchi, kwa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wananchi juu ya ulinzi na utunzaji wa vyanzo vya maji.

(c) Mhe. Spika, kuhusu suala la kuchemsha maji ni jambo la msingi, kama nilivyotangulia kusema kwamba sio wananchi wote wanatumia huduma ya maji inayotolewa na serikali kwa kupitia Mamlaka ya Maji. Kumekuwa na wimbi kubwa la vianzio binafsi, hasa visima, ambavyo vimechimbwa bila ya kufuata taratibu zilizowekwa na vimeunganishwa na mitandao ya maji ya visima katika mtandao wa serikali. Pia, viko katika maeneo ambayo hayako salama, ambayo hupelekea kuchanganyika na maji ya karo au mtandao wa maji machafu, hali ambayo hupelekea kusambazwa maji yenye vimelea na maradhi ya miripuko kama matumbo ya kuharisha na kipindupindu. Hivyo,kwa usalama zaidi huwa inashauriwa kuchemsha maji kabla ya kuyatumia, ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutojibu swali la msingi, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, alisema *ZAWA* haijashindwa. Mimi mwenyewe nimeshuhudia kwa kuifanya kazi hiyo jimbo kwa muda mrefu, na chanzo kikubwa ni maji kuwa machafu.Hata Mhe. Mohammed Aboud, nilimuuliza Ilani ya Chama cha Mapinduzi haijafika Michamvi hadi leo hii kwa vitendo, lakini kwa mdomo imefika.

Lakini kuna waathirika wengi wameathirika na chanzo cha maji na wizara unayoisimamia haijatoa elimu yoyote. Tunawashukuru Masheha na Ofisi za Wilaya kwa kugawa dawa hizo, lakini wizara yako haikuchukua jitihada zozote kwa wizara hiyo. Swali ni kwamba, na waswahili wanasema; 'usipoziba ufa utajenga ukuta'.

(a) Je, ni lini mtachukua tahadhari hii hasa kwa wananchi wa vijijini ambao wanaathirika sana na kipindupundu. Hilo la mwanzo.

(b) Viwango vya dawa vya *WHO* vya Umoja wa Mataifa, kwa ini hamvizingatii na mnatia dawa kidogo, bila ya kuzingatia kiwango hiki cha *WHO*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, ni kwamba tunashirikiana na taasisi mbali mbali. Kama alivyotaja Masheha, Masheha ni viongozi wa Wilaya, na *ZAWA* huwa inatoa taarifa na Masheha wanakuja kuchukua dawa pale kwenye *ZAWA* kwa ajili ya kuwafikishia wananchi wetu.

Mhe. Spika, ninachoomba kama kuna tatizo hilo basi tuletewe ili tulifanyie kazi kwa pamoja. Zaidi nikuombe Mhe. Mwakilishi, usafi ni muhimu, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya, wakati mwengine pia inachangia kupelekea maradhi hayo katika maeneo yetu. Lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba asilimia 0.2 ama 0.6 ndio kiwango wastani kwa kutibu maji, lakini inapokuwa imetokezea haja labda maji yamechafuka zaidi inaongezwa mpaka 0.9, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuongezea jibu la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Muwakilishi, alitaja habari ya ilani kwenye jibu lake la nyongeza, nataka niendelee kumhakikishia kwamba Serikali yetu inatekeleza vizuri sana ilani, na katika utekelezaji huo ndio maana Mheshimiwa, akawemo humu ndani bila ya hivyo asingekuwepo hapa kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unaofanywa na Serikali.

Lakini hata hivyo lazima tuelewe Mhe. Spika, kwamba kutekelezwa kwa ilani sio Serikali peke yake na Mhe.Mwakilishi, ana wajibu wake katika kukamilisha utekelezaji katika jimbo lake, kwa hivyo, pale anapoyafanya ya wananchi huo ni wajibu wake na asikatae wajibu katika kutekeleza jukumu lake la kukamilisha ilani yetu kwa pamoja. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa, siitaki hoja yako.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifutavyo.

Kwa kuwa amekiri kiwango kinachotiwa maji cha *chlorine* katika maji haya ili kuweka sawa ni 0.2 mpaka 0.6 na kwa sababu hiyo hiyo maabara yako iliyoko Saateni inaonyesha haina vifaa bora na haiko safi kwa utaratibu mzuri wa kuwahudumia wananchi.

a) Je, ni mpango gani uliokuwepo wa Serikali wa kuitengeneza maabara ile na kuipa vifaa bora ili kuweza kufanya kazi zake kwa umakini zaidi.

b) Mhe. Waziri, kwa sababu tu moja ya Wizara zako zitembelee kwa nguvu, je, ni lini au mara ngapi umetemebelea maabara ile ili kuona uhalisia wa kazi zao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Kwanza kiwango cha dawa kinachotiwa 0.2 hadi 0.6 ni kiwango muwafaka kwa ajili ya matumizi ya watu, kwa hivyo, naomba hilo alijue.

Lakini la pili, maabara iliyokuwepo Saateni ni maabara iliyo kamili, ni maabara yenye vifaa vya kisasa na inafanya kazi zake ipasavyo, mimi binafsi pamoja na Naibu Waziri, tumeshatembelea Maabara hiyo kama mara mbili, lakini bado utaratibu wa kutembelea maabara hiyo utaendelea kuwepo kwa sababu ni taasisi ambayo imo ndani ya miongoni mwa Wizara yangu.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini kwa kuwa mbali na kuwekwa kiwango cha kutosha cha dawa, lakini vile vile matatizo ya miundombinu ambayo husababisha mabomba mengine kupasuka na kuingiza maji machafu yakiwemo pia na kinyesi, yamesababisha maji ya katika maeneo ya jimbo langu katika maeneo ya Kisimamajongoo maarufu mkondo wa Nungwi wananchi kupatamaji ambayo yana kinyesi.

Je, Wizara ina mpango gani kuhakikisha ili kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama katika maeneo hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Kwanza inapotokezea hali kama hiyo tunaomba taarifa za haraka na sahihi zitufikie,

kwa sababu wakati mwengine mbali ya une-*nature* wake, lakini pia wahujumu wanafanya hivyo, kipindi fulani tumeshuhudi mpaka *oil* pia imewekwa. Sasa ikitokezea hali kama hiyo tupeyane taarifa haraka ili tiba ifuatwe. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, naomba pia nitoe taarifa ya ziada kwa ajili ya jibu la Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, kwamba sasa hivi kuna mradi wa *CHAISA* ambao unabadilisha miundombinu ya zamani katika eneo hili la mjini, kwa sababu tumeona wakati ule ilikuwa miundombinu ile iliyokuwa ya *ASBESTO* ikitumika ambayo sasa hivi inapasuka sana na ndio maana ikanokena tatizo limetokea kubwa. Lakini Serikali iko katika jitihada ya kufanya hiyo kazi na ndio hiyo miradi ambayo mnasema mnaiona, lakini kwamba *component* ya kubadilisha miundombinu ipo na *JICA* sasa hivi wanafanya kazi na tayari wanaendelea vizuri.

Nam. 131

Juhudi za Kuunganisha Kilimo na Utalii

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Wananchi wamekuwa wakilima sana ukulima wa mbogamboga, lakini wamekuwa na matatizo mengi yanayotokana na ukosefu wa elimu, na pembejeo, dawa, mbolea na hata soko kwa wale wanaofanikiwa kupata kwa wingi mazao hayo.

a) Wizara yako inajipangaje katika kutatua matatizo hayo.

b) Ni juhudi gani zimefaywa ili kuwaunganisha wakulima hao na sekta ya utalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 131 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaendelea na jitihada za kutoa huduma za elimu kwa wakulima kupitia maeneo yao na kuongeza idadi ya mashamba darasa pamoja na kuwatumia wakulima waliohitimu katika skuli za wakulima. Aidha, kupitia wafanyabiashara wanaouza pembejeo za kilimo kutoa huduma hiyo kwa wakati.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Taasisi zinazojihusisha na kilimo cha mboga ikiwemo *TAHA, UWAMIWMA* na *VSO* kupitia mradi wa *CASH* ambao kwa pamoja wanajihusisha na uuzaji na usambazaji bidhaa za mazao ya mbogamboga.

Mhe. Spika, aidha, Wizara imo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa kituo cha usarifu wa mazao kilichopo Kizimbani ili kuongeza thamani ya mazao hayo na hasa ule wakati wa mazao yanapokuwa mengi. Wizara pia kupitia prgramu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini *MIVARF* inawajengea uwezo wakulima sambamba na kutoa elimu ya soko na kukutanishwa na wanunuzi hususan soko la utalii.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali hii iliyopo madarakani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein, imeazimia kuhakikisha kwamba inatokemeza umasikini, inalinda masoko, inasaidia wafanya biashara na kulinda maslahi yao.

a) Je. Mhe.Waziri, anaweza kunambia bei ya nyanya katika soko la Mwanakwerekwe leo kilo ni shilingi ngapi.

b) Katika mkutano wetu hapa wa bajeti Mhe. Waziri, alikiri kwamba tayari kuna ramani za soko litakalojengwa katika eneo la Kaebona na akakiri kwamba hizo ramani ziko tayari. Kwa nini mpaka leo hizo ramani hazijafika katika Halmashauri ya Wilaya ya kati ili tuweze kuanza kazi na sisi ndio wawakilishi na Wabunge tuanze kuwachangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi:

a) Kuhusu bei ya nyanya kwa leo siwezi kukupatia jawabu sahihi kwa hapa, kwa hivyo, nitaomba nikuletee kwa maandishi.

b) Kuhusu ramani za Jengo la Kaebona za soko, ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ndio inayohusika na masuala ya masoko, kwa hivyo, kama ni ramani sisi tutaziwasilisha kwake yeye, halafu yeye ataziwasilisha huko kwako wewe, ahsante sana.

Mhe. Bihindi Khamis Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri, kwenye suali lako mama umezungumzia kuhusu mashamba darasa, nakuuliza mashamba darasa ni mangapi Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo, Malisili na Uvuvi: Mashamba Darasa yake naomba nikuletee kwa maandishi pia. kwa sababu umetaka ya jumla Unguja na Pemba.

Mhe. Spika: Kwa mujibu wa wakati tumeshamaliza maswali, lakini kanuni zinaniruhusu tumalize hili swala la mwisho.

Nam. 106

Matengenezo ya Barabara za Vijijini

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na changamozo kubwa zinazoikabili barabara zilizopo katika Shehia za Jimbo la Ziwani, zikiwemo Shehia ya Ndagoni hasa kwa vile ndio roho ya Pemba kutokana na kuwa ndio njia ya Umeme kutoka Tanga, Michungwani na Birikau. Na kwa kuwa miradi mingi ya barabara imekuwa ikielekezwa maeneo mengine na kuzisahau Shehia hizo.

Je, ni lini Serikali itazifanyia matengenezo barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi, swali lake Nam.106 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Wizara inazifahamu barabara hizo ambazo ni pamoja na barabara ya Wesha – Mkumbuu na tayari Wizara imeshafanya matengenezo kwa barabra hiyo kwa kiwango cha kifusi na hivi sasa barabara hiyo angalau inapitika vizuri. Aidha, Wizara iliifanyia matengenezo barabara ya Kijangwani - Birikau yenye 1.0 *km* kwa kiwango cha lami kwa *romix* katika hatua za majaribio. Hata hivyo, Wizara itazingatia matengenezo ya barabara hizo.

Mhe. Spika, barabara ya Mchangakwale - Pembeni yenye urefu wa 2.3 *km* nayo pia imefanyiwa matengenezo *Sport Improvement*.

Lakini napenda kumhakikishia Mhe. Muwakilishi kwamba, katika ziara yetu pamoja na yeye tulizikagua barabara hizi na tukaona kuna sehemu ambazo zimeharibika, aidha kwa mvua na naahidi kwamba zile sehemu korofi tutazifanyia matengenezo ili zile barabara ziweze kupitika kwa urahisi zaidi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri, pamoja na ziara tuliyoifanya na pamoja na barabara ya Ndagoni kwamba imetiwa fusi, lakini hivi sasa imechimka na ikinyesha mvua ni kwamba wanapata usumbufu wananchi, na ukiangalia kwamba Ndagoni ndio kwenye roho ya Pemba kutokana na umeme uliotoka Tanga.

Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba ipo haja ya kuitengeneza kwa kiwango cha lami barabara hile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Sote tulikuwa mashuhuda wakati Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, alivyowasilisha bajeti yake. Alisema kwamba kuna barabara tofauti ambazo kwa Unguja na Pemba zimeshafanyiwa uchambuzi yakinifu wa mazingira na miongoni mwa barabara zilizofanyiwa uchambuzi yakinifu wa mazingira ni barabara hii ya Wesha/Ndagoni hadi Mkumbuu.

Kwa hivyo, ile barabara tutaijenga kwa awamu lami na tutaanza na kilomita nne, kwa hivyo, tunamuomba awe na subra si kwa babaraba hiyo tu ya Ziwani bali barabara nyingi ambazo Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, aliziainisha katika bajeti yake ambazo kwa Pemba zinapita kilomita 55.9 na Unguja vile vile kama kilomita 75 basi tunamuahidi kwamba, sisi Serikali tutatengeneza kwa ukamilifu ahadi tulizozitoa kwa wananchi kupitia Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015/2020.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri, kwa kuwa tunajua kwamba barabara ya kijini nayo ipo kwenye ilani, lakini mpaka muda huu tunaona kwamba ile barabara imeshatengenezwa kwa kiwango cha fusi kwa muda mkubwa, lakini bado kiwango cha lami haijafikia na tunajua kwamba endapo imeshatengenezwa kwa kiwango cha fusi maharibiko yanaweza yakatokea.

a) Je, unatwambia vipi kuhusu barabara hii.

b) Lakini pia hapo hapo kwenye barabara ya Kijini, kuna barabara ambayo inatoka Kijini kuelekea mpaka Mwembe Kiduka, yaani Fukuchani. Je, unawaambia nini wananchi hawa wa maeneo haya kutoka Fukuchani kwenda Kijini Kigongoni, ili kuweza kupata ile barabara angalau japo kwa kiwango cha fusi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama tunavyojua sisi katika Wizara yetu tulitaja barabara ambazo tutazipa kipaumbele, zipo barabara ambazo zina kilomita 52 ambazo ziko Mkowa wa Kaskazini, nyengine Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini napenda kumhakikishia kwamba kuna barabara kule ambayo tutaijenga kwa lami katika ahadi zetu tulizotoa barabara ya Matemwe/Mbuyuni, barabara ya Kijini hivi sasa tuna utaratibu wa kutaka kuishughulikia ambapo tuna mfadhili ambaye anaijenga ile barabara.

Kwa hivyo, tunamuomba atupe muda kama vile barabara zake za ndani nilivyotoa ahadi hapa kwamba sisi Serikali tunajua kwamba kuna barabara muhimu, lakini kama nilivyosema awamu kwa awamu na uwezo utakapoturuhusu basi barabara zile tutazijenga, na zile ambazo zina umuhimu wa kuzijenga kwa lami namhakikishia kwamba tutazijenga kwa lami, atupe subira tu, ziko barabara nyingi sana na sisi tumeweka ahadi kwamba mtandao wote wa barabara tunataka tuhakikishe kwamba unapitika wakati wote bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Mimi nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri kwamba, yeye ndio mwenye dhamana ya barabara zote za Zanzibar na usalama wake, sasa nilikuwa nasema barabara za Pemba hasa zile zinazojengwa na *UUB* ni kwamba ni barabara ambazo zinakuwa nyembamba sana na hata sehemu za kona zinashindwa hata kupanuliwa ili kupunguza ajali katika sehemu zile.

a) Je, kuna ugumu gani wa kujenga barabara japo nyembamba na hata zile zilizokwishajengwa katika sehemu za kona zikaongezewa ili angalau kupunguza ajali hasa kwa eneo la Pemba kwa kona nyingi ambazo zinasababisha ajali.

b) Kwa nini barabara za *UUB* zikijengwa haziwekwi alama za barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Barabara tunapojenga tunaangalia viwango vya ile barabara, barabara *trunk road* tunajenga upana usiopungua mita 15 ndio hifadhi ya barabara, barabara za ndani zinategemea vile vile na mazingira, mazingira ya Pemba sote tunajua kwamba ni mazingira ya milima, kuna barabara mfano juzi aliuliza Mhe. Bahati, barabara yake kule ya Mwambe, barabara zile unakuta tumezijenga lakini mpaka sasa hivi hukuti ajali yoyote kwa sababu kila sehemu ambako kuna milima hatari au *cross* tunajenga wenyewe tunaita '*by pass'*. Zile *by pass* maana yake kwamba mtu anayetoka kule mwenzake anampisha anakaa pembeni ili apate kupita.

Sasa kutokana na mazingira na vile vile kwa ufinyu wa bajeti ambazo sisi *UUB* ni Idara ya Utengenezaji na Utunzaji wa Barabara, sasa sisi tunavyofanya kwamba zile barabara ambazo za ndani ambazo si barabara za *trunk road* zile tunazijenga kwa mazingira ya barabara husika.

Kuhusu haya masuala uliyosema, mimi nataka kumhakikishia Mhe. Suleiman, kwamba *UUB* wana wataalam wazuri, tatizo tuna uhaba wa vifaa, vile vile, kama unavyojua sisi Wizara yetu tunajitahidi kadri tunavyoweza kuwahakikishia barabara zote zile tunazijenga katika kiwango kinachotakiwa na hilo ni jambo ambalo tunalizingatia siku zote kuhakikisha barabara zinapata kudumu, kwa hivyo na mimi namwambia sana Mhe. Suleiman, barabara zile tunajenga kwa mujibu wa mazingira husika.

Kwa hivyo, asiseme kwamba barabara zile ni ndogo, sisi umuhimu wetu ni kurahisisha usafiri kwa wananchi na vipando, kwa hivyo, ni barabara nzuri naomba pia apongeze juhudi tunazozichukua Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Swali lake kuhusiana na alama za barabarani hujamjibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyosema alama za barabarani zinategenea na mazingira husika, barabara tunazojenga sisi tunaweka alama, lakini alama zenyewe kuna baadhi ya wakati wananchi wanaziondosha, barabara nyingi sisi tunawapa wakandarasi kuzijenga. Wakandarasi wanaweka alama na yeye ni shuhuda barabara zote za Mkoa wa Kaskazini zilizojengwa na *MCT*, barabara za Kusini Pemba barabara ambazo kusema la kweli kwa muda mrefu bado hazijajengwa na wakandarasi, lakini tumesema kuanzia sasa hivi barabara zote zinazojengwa ziwekwe alama ili kuepusha ajali na vile vile kupunguza watu kwenda kwa mwendo wa kazi zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mpaka hapo tutakuwa tumemaliza kipindi cha maswali, nina tangazo moja tu, mnatangaziwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba, lile Tamasha la Kidudu *Fashion Week* litafanyika siku ya Jumapili tarehe 9/10/2016 saa 1.30 usiku katika ukumbi wa *Grand Palace Hotel* Malindi. Waheshimiwa tunaombwa kuchangia Tamasha hilo kwa kununua kadi ya *VIP* kwa shilingi thalathini elfu na kadi hizo zinapatikana hapo masjala, Baraza la Wawakilishi.

Baada ya matangazo hayo waheshimiwa, sasa tunaingia kwenye utaratibu, nitamwita Katibu ili tuingie kwenye utaratibu wa hoja za Serikali, lakini naomba sasa kiti kije kichukuliwe na Mhe. Naibu Spika, ili tuweze kuendelea. Karibu Mhe. Naibu Spika.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha mbele ya Baraza hili Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya 11 Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza marekebisho katika baadhi ya vifungu katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, marekebisho ambayo yataweka masharti bora ya Katiba na kuiwezesha Katiba hiyo kuweza kukidhi haja ya kwenda sambamba na mahitaji ya wakati tulionao.

Mhe. Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar imeandikwa mwaka 1984 na inaendelea kutumika hadi hivi sasa. Katiba hiyo imeshafanyiwa marekebisho mara 10 marekebisho yote hayo yalilenga kuweka masharti bora na kuiwezesha Katiba kukidhi na kuanzishwa kwake hasa kuzingatia kwamba Katiba ndio msingi mkuu wa sheria zote za nchi.

Miongoni mwa marekebisho yaliyofanya katika Katiba ya mwaka 1984 ni mabadiliko ya 10 yaliyofanywa mwaka 2010. Dhamira Kuu ya mabadiliko ya mwaka 2010 ilikuwa ni kuiwezesha Katiba kuweza kwenda sambamba na

mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa uliokusudiwa kuanzishwa Zanzibar wakati huo.

Aidha, Katiba ya Zanzibar ilifanyiwa marekebisho mengine mwaka 2002, 1995, 1992, 1991, 1990, 1989, 1985. Katika marekebisho mwaka 1992 na 2002 Katiba ilifanyiwa marekebisho mara 2 katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kawaida kufanya marekebisho ya sheria kila inapohitajika kufanya hivyo. Marekebisho hayo hufanywa baada ya mapitio ya sheria husika na kuona kuwa sheria hiyo ina kasoro, hivyo, inahitaji kufanya marekebisho ili ziweze kukidhi haja na kuanzishwa kwake kutekelezwa kwa ufanisi.

Kwa kuwa Katiba ndio sheria mama nayo inafuata utaratibu wa marekebisho kama zilivyo sheria nyengine. Kiutaratibu mabadiliko ya sheria ni lazima yafanywe na chombo chenye mamlaka ya kufanya hivyo ambacho ni chombo cha Kutunga Sheria Baraza la Wawakilishi kwa hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, hivyo, mswada huu umewasilishwa ili kuweza kukamilisha utaratibu wa kuifanyia marekebisho Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Naibu Spika, mswada wa Marekebisho ya Sheria inayopendekezwa utasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, hivyo, itakuwa ni sehemu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umegawika katika sehemu kuu 2 kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza, Utangulizi, sehemu hii itazungumzia jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria hii pamoja na kueleza kwamba sheria hii itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Sehemu hii ina vifungu viwili vifuatavyo:-

Kwanza, sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2016 na itaanza kutumika kuanzia 6 Aprili, 2016. Sheria hii itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo katika sheria itajulikana kama Katiba.

Sehemu ya Pili, Marekebisho ya vifungu mbali mbali. Sehemu hii nayo ina vifungu 2.

Tatu, Kifungu cha 66 cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi yaliyopo baina ya maneno vyama vya siasa na iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani.

Nne, Kifungu cha 79(2) cha Katiba kinafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno kifungu cha 62(3) yaliyopo baina ya maneno bila ya kujali masharti ya na cha Katiba na kuweka badala yake maneno ya kifungu cha 78(4).

Mhe. Naibu Spika, marekebisho ya vifungu mbali mbali ya Katiba iliyopendekezwa kwenye kifungu cha 3 yanakusudia kuweka masharti yanayolingana na kifungu cha 119 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambacho kinatoa fursa ya uteuzi pale ambapo hatakuwepo Kiongozi wa Shughuli za Upinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi, masharti ya kifungu cha 66 cha Katiba kilivyo sasa hakitoi uwezo wa Mamlaka ya Mhe. Rais kufanya uteuzi kwa kuwa masharti ya kifungu kinalazimisha kushauriana ama na Kiongozi wa Upinzani au Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi, ili kutoa fursa hiyo pana ya uteuzi kwa kushirikisha Vyama vya Siasa pale ambapo Kiongozi wa Upinzani hatokuwepo, mswada unapendekeza kufuta maneno yenye uwakilishi ndani ya Baraza kufutwa na maneno hayo kutatoa uwezo wa Mhe. Rais kufanya uteuzi wa kushauriana na vyama vya siasa bila ya kujali uwakilishi wa vyama hivyo ndani ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Kifungu cha 4 cha mswada kinapendekeza marekebisho ya uandishi ambapo kifungu cha 79(2) cha Katiba kinafanya rejea kwenye kifungu cha 62(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo kifungu hicho hakipo. Kwa msingi huo na ili kuondoa shaka ambayo inaweza kujengeka ni vyema kifungu hicho kikafanyiwa marekebisho kwa kuondoa utata uliopo na kufuta maneno ya kifungu 62(3) na kuweka badala yake kifungu 78(4) ambacho ndio rejea sahihi inayokubalika.

Mhe. Naibu Spika, kufanyika marekebisho yanayopendekezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kupitia mswada huu, kutaiwezesha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kutekelezeka kwa ufanisi kwani kitatoa fursa kwa mamlaka ya uteuzi kufanya uteuzi wa Wawakilishi wa Kuteuliwa hata pale ambapo hapatakuwa na Kiongozi wa Shughuli za Upinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi. Masharti ya kifungu cha 66 kama kilivyo sasa hakitoi uwezo wa Mamlaka ya Mhe. Rais kufanya uteuzi pasi kushauriana na kiongozi wa upinzani. Hivyo, kuondoshwa kwa kasoro hiyo kutarahisisha utekelezaji wa Katiba hiyo. Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa marekebisho ya sheria hii unatarajiwa kuchukua muda mfupi kwani mara tu taratibu ya kupitisha sheria

hii itakapokamilika matumizi yake yaanza rasmi kuwa sheria hii itakuwa ni sehemu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala kwa ushauri wao na maelekezo yao. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu na Ofisi yake kwa mashirikiano yao katika kuandaa mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako Tukufu liridhie na kukubali mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 kama ilivyopendekezwa na mswada huu ili marekebisho hayo yaweze kuwa sehemu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mtu wa mwanzo ambaye nitamwita atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, halafu baadae atafuata Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala, ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kutujaalia neema ya kuwa hai na kukutana kwa mara nyengine tena mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu na watu wake, ikiwemo kupitisha miswada ya sheria mbali mbali ukiwemo na mswada huu ulio mbele yetu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi na Moja ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe.Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuwasilisha maoni kwa niaba ya kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada nilioutaja hapo juu.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa na kwa niaba ya Kamati naomba kuishukuru Seriakali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuona umuhimu wa kuleta Mswada huu muhimu mbele ya Baraza lako tukufu ili uweze kujadiliwa, kupitishwa na kuweza kutumika kwa lengo lililokusudiwa la kuwa na Katiba madhubuti itakayoweza kutumika katika uendeshaji wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wangu wa Kamati kwa michango na ushauri wao muhimu walioutoa wakati tulipokua tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo mawazo na ushauri wao umewezesha leo hii kuwa hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako kwa ajili ya kupata ridhaa ya Wajumbe na hatimae kupitishwa kwa ajili ya kufikia lengo lililokusudiwa na Serikali kwa maslahi ya nchi yetu na wanachi wetu kwa aujumla.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

1.	Mhe: Machano Othman Said	-	Mwenyekiti
2.	Mhe: Mwanatatu Mbarak Khamis	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe: Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
4.	Mhe: Saada Ramadhan Mwendwa	-	Mjumbe
5.	Mhe: Shamata Shaame Khamis	-	Mjumbe
6.	Mhe: Mihayo Juma N'hunga	-	Mjumbe
7.	Mhe: Nadir Abdulatif Yussuf	-	Mjumbe
8.	Mhe: Ali Khamis Bakar	-	Mjumbe
9.	Ndg: Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
10.	Ndg: Ali Alawy Ali	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Baada ya utangulizi huo sasa kwa niaba ya kamati, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na Mswada uliopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuona haja ya kukifanyia marekebisho Kifungu cha 66 cha Katiba ilikuondoa utata wa utekelezaji wake. Katika marekebisho hayo Serikali imependekeza kukirekebisha kifungu hicho kwa kuifanyia marekebisho *paragraph* ya pili ya kifungu hiki ili Rais aweze kushauriana na vyama vya siasa bila ya kujali uwepo wa Kiongozi wa Upinzani Barazani au Uwakilishi vya vyama vya Siasa ndani ya Baraza.

Hata hivyo, kamati inashauri kifungu cha 66 cha Katiba *paragraph* ya kwanza yote ndio ibakie kama ilivyo hivi sasa katika Katiba, hivyo, *paragraph* ya pili ya kushauriana na kiongozi wa upinzani Barazani au vyama vya siasa katika uteuzi wa Wajumbe wawili ifutwe yote kwa vile hali hiyo inapunguza na hadhi ya Rais kwenye Katiba yetu. Aidha, mapendekezo ya Serikali ya kumtaka Rais ashauriane na vyama vyote vya siasa vilivyokuwa nje ya Baraza vitaleta utata zaidi kwa sababu nchi yetu hivi sasa ina vyama 22 vilivyosajiliwa nchini, kwa hivyo, itakuwa ni tabu sana.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, Kamati yetu imeona kuwa wakati umefika kwa kifungu cha 119 (1) cha Katiba ya Zanzibar kinachohusu "Tume ya Uchaguzi" nacho kubadilishwa ili kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Kamati inapendekeza kifungu hicho kufutwa na kuandikwa upya ambapo baada ya marekebisho kisomeke kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati yetu inaona kuwa kwa kifungu 119 cha Katiba ya Zanzibar kinachohusu Tume ya Uchaguzi nacho kikabadilishwa ili kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Kamati inapendekeza kifungu kufutwa na kuandikwa upya na ambapo baada ya marekebisho kisomeke kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kifungu 119(1):
Kutakua na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakua na Wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Wazanzibari ambae ataona anafaa;

(b) Wajumbe watano watakaoteuliwa na Rais na angalau wawili wawe wanawake;

(c) Mjumbe mmoja mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahkama Kuu.

Mhe. Naibu Spika, sababu kubwa za kamati yetu za kufanya marekebisho ya kifungu hiki cha 119 cha Katiba ni kwamba mazingira ya kifungu hiki yanalingana sana na kifungu cha 66 cha Katiba ambacho Serikali imeleta kufanyiwa marekebisho. Kwa mujibu wa Katiba kifungu hicho cha 119 ambacho kinahusu Tume ya Uchaguzi. Kati ya Wajumbe saba wa Tume hiyo, wajumbe wawili Mhe Rais atawachagua baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Barazani na wawili atachagaua baada ya kushaurina na Kiongozi wa Upinzani Barazani au kama hayupo ashauriane na vyama vya siasa.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inajenga hofu na hiki kifungu cha kumbana Mhe Rais kushauriana na kiongozi wa upinzani au vyama vya siasa kwa msingi ufuatao:

Kwanza, uzoefu unaonesha Wajumbe wa Tume wanaopendekezwa na Kiongozi wa upinzani au vyama vya siasa wanakua sio huru badala yake wanaenda kulinda maslahi ya vyama vyao.

Pili, iwapo hakutakua na kiongozi wa Upinzani Barazani, hivyo, kutumia vyama vya siasa kupendekeza majina ya hao wajumbe wawili lipo tatizo ambalo linaweza kutokeza hasa katika kutambua ni vyama gani vya siasa vitahusika hivi sasa. Nchi yetu ina zaidi ya vyama 22 vya siasa vyenye usajili wa kudumu na kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa ni lazima kwa kila chama kiwe na muundo wa kitaifa kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano kuwa na uwakilishi katika vyama hivyo, jambo hilo linaweza kuleta mgogoro mkubwa maana kila chama kinaweza kuvutia kwake.

Mhe. Naibu Spika, mwisho, iwapo uteuzi wa Tume yote ya Uchaguzi utakuwa chini ya mamlaka ya Rais basi dhana ya Tume huru ya Uchaguzi ndio itakua imetimia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya marekebisho hayo na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yangu. Napenda kuchukua tena fursa hii kwa kuwashukuru tena Wajumbe wangu wa Kamati kwa kunipa mashirikiano makubwa wakati tulipokua tukipitia mswada huu hadi leo kuweza kutoa maoni ya kamati mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, Mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi kwa mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa nategemea michango na mawazo yao yatasaidia zaidi katika kuuboresha mswada huu. Kamati yangu inaitaka Serikali kuipitia Katiba yote ili iweze kufanyiwa marekebisho makubwa kabla ya mwaka 2018 ili kuondoa kasoro mbali mbali ambazo zipo katika Katiba hiyo. Kamati inaelewa kwamba baadhi ya vifungu vya Katiba urekebishaji wake lazima kuwe na kura za maoni. Lakini hata hivyo tunaomba Serikali iangalie Katiba yote.

Mhe. Naibu Spika, Kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezeshesha kusimama hapa mbele yako kuchangia Mswada huu wa Sheria wa Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kuona kwamba pana haja ya kufanya marekebisho hasa nyakati tulizokuwa nazo. Mwaka 2010 katika marekebisho ya Katiba hii tunayotumia, mimi nilikuwa miongoni mwa wajumbe ambao tulishiriki katika kufanya marekebisho mbali mbali. Lakini nilikuwa mkaidi sana kwa baadhi ya mambo nikasema kwamba tuzingatie wakati tuliokuwa nao, kwa sababu kwenye mfumo wa vyama vingi hakuna chama fulani na fulani tu. Mfumo mzima wa vyama vyote vina haki madhali vimesajiliwa na madhali vinaingia katika chaguzi zetu basi na wao wana haki ya kutoa ushauri wao ili tuelekee katika mwelekeo wa umoja wetu kama tuliokuwemo katika Baraza lako hili.

Mhe. Naibu Spika, naamini wazi hakuna suala ambalo lina utata katika nchi hii kuliko fulani kujiona bora kama wale wengine. Hili ndio tatizo lilotusababisha au linaloleta adha kufanya hii Katiba isitekelezwe. Naamini mengi yanayofanywa kwenye mfumo wetu kuna mengine mazuri na mengine mabaya. Kwa hivyo, mimi niipongeze serikali kwa kuona sasa hivi umefika wakati marekebisho ya Katiba yafanywe kipindi baada ya kipindi mpaka tuhakikishe tunapata Katiba nzuri kwa wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba bila ya kumbagua huyu katoka wapi au chama gani.

Hili litatusaidia sana. Mhe. Naibu Spika, tukizingatia hilo sisi katika mazingira yetu tuliyokuwa nayo Tume yetu ya Uchaguzi ya Zanzibar, mimi naipongeza sana kwa kazi nzuri inayofanya, nawapongeza wajumbe wote waliofanya kazi nzuri kwa bidii kuhakikisha nchi yetu inakwenda katika demokrasia inayokubalika. Ingawa kuna baadhi demokrasia hii wameipinga kwa upande lakini hilo ni shauri lao, kwa sababu unapoambiwa uelekee huku katika Sheria ya demokrasia basi uelekee kule wanakotaka wengi, na vyama vingi vilielekea huko tulikotaka kwa ajili ya usalama wa nchi yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nivipongeze vyama vya siasa kwanza vyote vilivyoshiriki katika uchaguzi wa marudio, tena niwapongeze wagombea wote waliogombea kwa nafasi mbali mbali, hii ni dhahiri inaonesha demokrasia haikuvunjwa katika nchi yetu imeendelezwa na itaendelea kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu milele na milele.

Mhe. Naibu Spika, unapomsomesha mwanafunzi hutegemei wanafunzi wale wote wakawa na mwelekeo mmoja, na hakuna mwanafunzi mbaya katika mazingira ya mwalimu anayoyapata kuliko mwanafunzi fulani kujiona bora kuliko wale wengine, ah! Hawa si wadogo tu kwangu hawana kitu, hilo ni kosa. Lazima uwachukue wanafunzi wale uwaelekeze katika njia moja ya kupata faida kwa kuwasomesha na ukapata kitu kimoja cha matokeo yake. Mhe. Naibu Spika, ndio maana nasema naipongeza serikali kwa kuangalia vifungu mbali mbali ambavyo vitatupa mwelekeo mzuri katika kuiweka sheria yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, imezungumzwa katika kifungu cha 119(1) kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao.

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mhe. Rais kutoka miongoni mwa Wazanzibari ambaye ataona anafaa, hiyo ni haki ya Rais;

(b) Wajumbe watano watakaoteuliwa na Rais na angalau wawili wawe wanawake, mimi hii angalau ningeona bora iondolewe, kati ya watano, wawili wanawake tu.

Maana yake ukisoma angalau, itakuwa kama haina thamani, hayo ni mawazo yangu lakini, tuseme tu kwamba kutakuwa na wajumbe watano watateuliwa na Mhe. Rais, miongoni mwao wawili ni wanawake, hivyo, ingekaa vizuri sana na tungewapa heshima sana kinamama zetu. Lakini kama ni muandiko wa kisheria siingilii, lakini ukisema angalau itakuwa kama tumewaondolea hadhi wakati watafanya kazi nzito ya taifa kwa maslahi ya demokrasia katika nchi yetu. Kwa hivyo, niombe kwamba wajumbe watano watakaoteuliwa na Mhe. Rais, kati yao wawili watakuwa wanawake, hayo ni mawazo yangu.

Mhe. Naibu Spika, mmoja miongoni mwa wajumbe hao mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Hii pia naipongeza na ingawa haikufafanua, Majaji wote wana haki kama nilivyosema wanawake nao kwa sababu hakuna mwanamke wala mwanamme, Jaji ni Jaji tu. Kwa hivyo, yeyote nae anayefaa atatusaidia katika kuongoza goma letu hili huko mbele tunakokwenda kwa demokrasia ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, tukitaka tusitake mimi katika historia ya maisha yangu niseme tu kwamba nimeshuhudia chaguzi nyingi tokea mfumo wa chama kimoja mpaka vyama vingi. Lakini jambo kubwa ambalo linatuathiri miongoni mwetu wakati mwengine tunakuwa na papara ya kuamua mambo.

Mhe. Naibu Spika, lilipokuja wazo la kubadilisha Katiba mimi nililia katika Baraza hapa, tuna haraka ya nini, tutizame hali ya hewa inavyokwenda kwa sababu huyu tunayemfikiria kuwa ndio yeye kweli yuko katika dhahiri ya kuwa yeye. Kwa sababu tatizo lilojitokeza nilitoa hofu kuna mambo mengi yalijitokeza katika nchi yetu tukatafuta miafaka mbali mbali, tukasema afueni itaondoka, lakini ilipindwa yote ilikataliwa kata kata. Lakini baadae tukabadilisha Katiba hii kwa maslahi ya kuleta umoja na uelewano ndio huu tuliokuwa nao humu katika Baraza hivi sasa, lakini bahati mbaya wale walengwa wakuu wa vyama vyote, yaani yule aliyekuwa anategemewa ndio atasaidia zaidi basi yeye ndiye aliyepinda njia akaivunja demokrasia hiyo.

Kwa hivyo, mimi kwa upande wangu niseme tu kwamba naunga mkono marekebisho haya ya Katiba kwa ajili ya kupata mwelekeo mpya wa Tume yetu ya Uchaguzi, kwa kupata watendaji mbali mbali na vifungu mbali mbali kwa ajili ya kuiweka sawa Katiba hii hasa tukizingatia mfumo wa vyama vingi una watu wengi ambao wenye maarifa. Leo kuonesha hilo baada ya uchaguzi wa Mhe. Rais na uteuzi wake kuwaleta wajumbe wawili katika Baraza hili, Mhe. Said Soud Said na Mhe. Juma Ali Khatib, tunahakikisha kwamba dunia imetuelewa na ile raha ya Baraza unaiona, kwa sababu wazo watakalolitoa upande wa pili yeyote yule linalenga kujenga nchi sio kubomoa nchi.

Kwa hivyo, huo ni mfumo ambao naamini Mhe. Rais akijateua lolote baadae kwa ajili ya viongozi wetu watakaokuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi itakuwa na raha na itakuwa na mwelekeo mzuri, kwa sababu naamini maridhiano mazuri yatatokea bila ya matatizo. Lakini ikiwa mimi ndio mkuu wa chama fulani kama Kiongozi wa *Simba Sports Club* nikataka mchezaji huyu tu aingie huyu hiyo ni hatari, itakuwa sina demokrasia naamua ninavyotaka kimabavu kwakua kiongozi. Kumbe mkikaa vyama vingi mtapata mengi mazuri kwa ajili ya kuwaelekeza pazuri kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri, nawapongesa watendaji wake, lakini pia nalipongeza Baraza la Mapinduzi chini ya Rais wake na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona wakati umefika kufanya mageuzi haya kwa salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya hayo nitamke rasmi mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele ambao kwa asilimia mia moja wanaotaka mema katika nchi hii wananiunga mkono, kwa hiyo, naunga mkono mswada huu sina matatizo nao, naomba Waheshimiwa Wajumbe tuupe nguvu na tuuboreshe ili upite na ufanye kazi vizuri kwa

maslahi ya nchi yetu na usalama wa taifa letu. Nashukuru mheshimiwa, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kidogo nitawaomba radhi Mhe. Juma Ali Khatib, pamoja na Mhe. Said Soud Said, kwamba yamekuja majina mengine ya wajumbe *back-benchers*, kwa hiyo, nitatangulia kwanza watachangia wao halafu baadae mwisho kabisa tutawapa fursa Waheshimiwa Mawaziri, kuweza kuchangia. Kwa hiyo, naomba radhi sana kwa hilo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kama kawaida kwa sote kutujaalia uzima na afya na vile vile niwapongeza sana wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa mara nyengine tena kwa kuniamini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia machache tu kwenye suala hili na vile vile nitawaachia wenzangu wengine waendelee na wao wapate nafasi.

Kwanza ningempongeza sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara na hekima zake na kila kiongozi ana sifa zake.

Vile vile, nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, kwa kazi zake, juhudi zake na mwenendo wake mzuri katika nchi yetu. Kwa kweli hali tumeiona hasa kwenye masuala yaliyotokezea ya uchaguzi, wapo waliokubali na wapo waliokuwa hawajakubali. Lakini kwa ujumla hali halisi iliyokuwepo vyama vilivyokuwa vingi havijakubaliana na *results* za Tume ya Uchaguzi.

Vile vile, niwapongeze sana wale vyama vyote waliogombea nafasi za Rais na nafasi nyengine waliokubali matokeo nakuwa pamoja na sisi niwapongeze sana, tuko nao pamoja na tutaendelea kuwa nao pamoja siku zote. Pia, kwenye pendekezo la kwamba Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tumpe nafasi yeye za kuteua hawa wajumbe watano, hili mimi nali-*support* asilimia mia kwa mia, kwa sababu humpa nafasi yeye, hii itamuondoshea maudhi ya mambo mengine na vyama vyengine vinavyomzungusha kichwa. Tunaona dhahiri kwamba kuwepo kwa vyama vingi wakati mwengine kuvishirikisha pia ina matatizo yake. Wapo wanaomkubali watamsaidia lakini kuna wengine watakuwa wako *against* na haya maamuzi yake au na ushauri wake italeta mtafaruku katika kujadili mambo mengine. Kwa hiyo, mimi ningeomba sana na

ningewaomba wajumbe wenzangu tukampa fursa Mhe. Rais ili kama tulivyopendekeza ikiwezekana kwa kukubaliana sote tulikubali na tumpe nafasi hiyo.

Mhe.Naibu Spika, ningeenda kwenye suala la Tume ya Uchaguzi. Mimi ningependekeza sana Tume ya Uchaguzi iwe tume huru, isiyoingiliwa na iwe yenye majibu ambayo yatakayokuwa yao wenyewe yasiingiliwe na mtu, wala aziweze kushtakiwa, wala kuingiliwa na mtu yeyote duniani. Nimesema hivyo kwamba, hili litaondosha matatizo kwa sababu kama tulivyoona tume imeamua lakini kila mmoja anajaribu kupinga pinga. Lakini mimi mapendekezo yangu pamoja na mwenyekiti wangu na wajumbe wenzangu ningependekeza zaidi tume hii iwe huru na iwe na maamuzi kamili yao wenyewe na wasiwe na haki ya kushtakiwa wala kupelekwa kwenye vyombo vyovyote vile, jibu litakalotoka liwe hilo hilo kutoka tume huru.

Mhe. Naibu Spika, pia, ningependekeza sana Mhe. Rais atapoteua basi ateue watendaji waliokuwa na uhakika, wanaojiamini na wanaoweza kufanya maamuzi kama yaliyofanyika kipindi cha nyuma, sio wale ambao wataoweza kutetereka na kuogopa kwa sababu vitu hivi vinataka msimamo mkali, vinataka maamuzi mazuri na chombo hiki kitapotetereka nchi inaweza kutetereka.

Mhe. Naibu Spika, tumeona athari kubwa baadhi ya nchi ambazo zimetoa maamuzi lakini chombo kikitetereka na nchi inakwenda vyengine. Kama juzi imetokeza Gabon na mambo mengine. Lakini pia ningependekeza hivi vyama 21 vilivyokuwepo mimi kama ilivyopendekeza timu yangu kwa ufupi ya Katiba na Sheria basi Mhe. Rais awe na maamuzi ya kufanya mwenyewe ya kuteua hawa wajumbe bila ya kuzungushwa zungushwa na kushauri watu ambao wengine hawataki ushauri.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitochangia mengi lakini haya yote yaliyozungumzwa na kamati yangu, mimi naya-*support* kama mjumbe na niko pamoja nayo na nitawapongeza sana wajumbe wote wa kamati yangu 10 kwa makubaliano ya pamoja kwa kufanya kazi na kukubaliana na kuangalia hasara zilizokuwepo. Kwa sababu sisi hatutaki nchi yetu ije ipate matatizo, sisi tunataka amani, utulivu, tunataka chama chetu kiendelee. Kwanza mimi binafsi nashukuru sana kuzaliwa kwenye Chama cha Mapinduzi, na nashukuru sana Chama changu cha Mapinduzi kwamba leo nimeweza kufika hapa kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani, lazima mtu ushukuru vile vile umezaliwa kwenye Chama cha uhakika. Mimi nimezaliwa wazee wangu wako kwenye Chama hiki na mimi nitaendelea mpaka nitapofika mbele ya haki.

Mhe. Naibu Spika, tumeona hasara wale wenye vyama vyengine ambavyo havitaki maendeleo, matokeo yake ndio hawamo humu ndani. Kwa hiyo, nawapongeza sana wale waliokubali na walioshirikiana na sisi wamo Waheshimiwa Mawaziri na vyama vyengine viwili, vitatu ambavyo vimeona kwamba uhakika uliokuwa tunao sisi Chama cha Mapinduzi kwa kushirikiana kwa pamoja, kuaminiana na pia kuyaamini maamuzi ya Tume ya Uchaguzi basi leo wamefika hapa na tuko nao pamoja na tunaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naipongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa maamuzi waliofanya pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana kwa pamoja ili tujenge Taifa letu na kuepusha matatizo, vurugu na vita.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitafikia hapa na hili suala mimi kwangu mimi nalikubali kwa asilimia mia, halina tatizo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumza machache sana katika mswada huu wa marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe.Naibu Spika, mimi kwanza naishukuru sana serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu chini ya usimamizi wa Mhe. Waziri, makini, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Haroun Ali Suleiman, naamini wazi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wetu huyu tunaamini ndani ya kipindi chake cha miaka hii mitano Katiba hii ataitendea haki.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mswada wa sheria unatushauri turekebishe kifungu kimoja tu na marekebisho madogo katika kifungu chengine kilichotoholewa. Lakini na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio tunaopitisha sheria hizi, ndio tunaojadili na tunayo haki vile vile ya kutoa mapendekezo. Na naamini mapendekezo haya tutakayoyatoa basi serikali yetu itaweza kuyazingatia.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba vile vile kuongezea nyama. Kwanza naipongeza sana kamati yetu hii ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliofanya na kuweza na wao kuja kuwa na mapendekezo yao vile vile. Mimi mapendekezo ya kamati Mhe. Naibu Spika, nayaunga mkono kwa asilimia mia moja vile vile.

Lakini kama kawaida yetu baada ya kuona maoni ya kamati, sisi kama wajumbe na sisi tunaweza tukatia nyama kwa yale maeneo ambayo tunayohisi

tunaweza tukatia nyama. Sasa Mhe. Naibu Spika, na mimi pia nilikuwa naomba kupendekeza tufanye marekebisho ya kifungu cha 39, kifungu cha 40, kifungu cha 80(a), kifungu cha 119 na kifungu cha 134.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikaamua kufanya marejeo ya kufanya marekebisho ya kifungu hiki? Ukiangalia kifungu cha 66 ambacho leo hii tunaamua kukirekebisha naomba kidogo nisome ili nijenge msingi wa hoja zangu.

Kifungu cha 66 kinasema kwamba:

"Kutakuwa na Wajumbe kumi wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoelezwa na kifungu cha 68(a) na (c) cha Katiba ambao wakiteuliwa watafaa kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Isipokuwa kwamba Wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au kwa kushauriana na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani".

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema mwenzangu Mhe. Ali Suleiman Ali tulipokuwa tukifanya marekebisho ya Katiba hii tulishauri mambo mengi sana, na kwa bahati mbaya kutokana na mazingira ya wakati ule ilibidi sasa tukubaliane na yale ambayo yamekuja. Tulisema kwamba iwapo leo tutamwambia au tutampa masharti kwa mujibu wa katiba Mhe. Rais ateue katika nafasi zake 10 wajumbe wawili kutoka kambi ya upinzani waliokuwemo ndani ya Baraza. Je, ikiwa hakutokuwa na chama chochote cha siasa kilichoshinda uchaguzi isipokuwa chama kimoja tu. Je, Rais hapa ataweza kuteua nafasi hizo?

Tukaambiwa aa, maana yake maridhiano, leo matokeo yake yamerudi yale yale, yale tuliyoyashauri sasa hivi ndio yaliyokuwa hapa. Kwa maana hiyo, Rais tumempa hii katiba kuitekeleza lakini tumempa na masharti magumu sana ambayo wakati mwengine anaumiza kichwa ni namna gani ataweza kutekeleza.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mapendekezo haya ya serikali kwamba Mhe. Rais katika nafasi zake 10 basi tunakubali nafasi mbili ateue kutoka katika vyama vya upinzani, lakini vile vile kumuwekea mashindikizo kwa kushauriana na vyama vya upinzani. Wenzangu wamesema kuna vyama karibu 22, je, kama hawakukubaliana Mhe. Rais atafanya nini. Sasa mimi nadhani

ushauri wangu hivyo vyama vyote ambavyo vipo vimesajiliwa wapeleke majina yao ili sasa Mhe. Rais katika majina yale ateue majina mawili.

Mhe. Naibu Spika, tukitaka tusitake tulipofanya marekebisho haya ya katiba tuliangalia zaidi maslahi ya chama kilichokuweko madarakani na chama kimoja, hatukuangalia maslahi ya vyama vyengine. Hili tulilishauri sana, unapojenga demokrasia ili kuvilea na vyama vyengine vidogo vidogo vipate uhai, huwezi ukakitengenezea mazingira katika nafasi kile chama cha upinzani ambacho kina nguvu ukaviacha vile vyama vyengine vidogo vidogo vitakufa tena vitakufa katika kifo cha kiofisa.

Mhe. Naibu Spika, wakati umefika sasa hivi katiba hii isiimarishe vyama fulani, katiba hii iimarishe msingi wa demokrasia kuwe na *fair play*. Kwa hiyo, mimi napendekeza Mhe. Rais katika nafasi zake 10, nafasi nane ateue katika chama chake mwenyewe na nafasi mbili apelekewe mapendekezo ya majina kutoka vyama vya upinzani. Hapo ndiyo tutakuwa tumempa nafasi Mhe. Rais kwa mazingira yote kutakuwa hakuna kikwazo chochote cha kikatiba ambacho kitakachokuwa kimemfunga.

Vile vile, nataka niunganishe kifungu hiki na kifungu cha 39(a) ambacho pia nimesema ninahisi iko haja ya kukifanyia marekebisho naomba nikinukuu.

Kifungu cha 39(a) (1) kinasema kwamba:

"Endapo, ndani ya siku saba mara baada ya Rais kushika madaraka, chama kinachostahiki kutoa Makamo wa Kwanza wa Rais, kitashindwa kuwasilisha kwa Rais jina la uteuzi wa Makamo wa Kwanza wa Rais, Rais, bila ya kujali masharti ya kifungu cha 39(1) na (3) cha Katiba atawacha wazi nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na kuteua Makamo wa Pili wa Rais".

(2) "Kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Rais bila ya kujali masharti ya kifungu cha 42(2) cha Katiba, atateua Mawaziri na kuwacha wazi nafasi za uteuzi wa chama au vyama vya upinzani".

Kwanza hapa hii katiba yetu inavyosema vyengine na sisi sasa hivi tunafanya vyengine. Leo tuna Makamo wa Kwanza wa Rais hapa? Hatuna lakini je, hizo nafasi za wazi za mawaziri kutoka vyama vya upinzani hakuna kwa sababu kulikuwa hakuna chama ambacho kimeshika ile nafasi ya pili na kupata ile asilimia 10. Sasa mimi hapa ushauri wangu, ikiwa yatatokezea mazingira kama tuliyokuwanayo hivi sasa, basi nadhani Mhe. Rais awe na maamuzi yake ya kuamua ikiwa ataamua kuteua mawaziri kutoka katika vyama vya upinzani sio

chama cha upinzani, kutoka katika vyama vya upinzani basi tumuwekee labda masharti kwamba asilimia fulani labda kama ni wajumbe wawili au watatu anaweza kuwateuwa katika Baraza la Mawaziri. Lakini kwa hii katiba ilivyo sasa hivi ina maana hapa kulikuwa kuna mawaziri wanasubiriwa kutoka kambi ya upinzani ambao kwa sasa hivi hawapo.

Chengine kifungu cha 40(1) kinachosema "Endapo nafasi ya Makamo wa Kwanza au Makamo wa Pili wa Rais itakuwa wazi:

(a) Kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu..." na mambo mengine Rais atamteuwa Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais kwa kutegemea nafasi ilivyo wazi".

Sasa mimi nadhani kutokana na mazingira tuliyokuwanayo kuna uwezekano mkubwa mara nyingi ikawa nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais haipo. Sasa mimi nadhani ni vyema sasa hivi nafasi hii tukaifuta akabakia Makamo wa Pili wa Rais ambaye ataweza kufanya shughuli zake kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Rais katika shughuli zake. Kwa sababu kama sasa hivi tuna katiba ambayo imeandikwa tu, lakini haitekelezwi. Sasa mimi nadhani moja katika mapendekezo yangu nakusudia kusema kwamba hii nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwanza kwa ndani ya miaka mitano haitotekelezwa, kwa hivyo nafikiri haitokuwa na haja tena ya kurejeshwa kuwa katika hiyo nafasi.

Mhe. Naibu Spika, chengine kifungu cha 80A naomba nikinukuu:

"Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 80 cha Katiba, Baraza la Wawakilishi halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusiana na sharti lolote liliomo katika kifungu chochote kilichoainishwa katika kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mpaka kwanza mabadiliko hayo yakubaliwe na wananchi kwa Kura ya Maoni".

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu kigumu tulichokiweka kwenye Katiba ya Zanzibar ni kifungu hiki. Katika mazingira yetu ya nchi za Kiafrika sijui nchi gani kwenye katiba zao kuna vifungu vinavyolazimisha kupiga kura ya maoni katika maamuzi tofauti.

Mhe. Naibu Spika, unaposema maamuzi fulani lazima yapate kura ya maoni Mheshimiwa kura ya maoni ndio kura ya maoni, kura ya maoni wakati mwengine serikali inaweza ikaja na jambo lake wananchi wakalikataa kabisa, pale ni sawa sawa kama kuidhalilisha serikali.

Mfano mdogo kama Uingereza, tuangalieni hivi karibuni, David Cameron yule kapapatua mpaka dakika ya mwisho, lakini wananchi wakasema sisi tuondoke matokezeo yake sasa hivi hata uchumi kidogo umeanza kutetereka na mambo mengine. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwa kuwa tunayo nafasi kama Baraza la Wawakilishi ya kuleta azimio, na kwa sababu ukiangalia kifungu cha (3) kinasema:

"Bila ya kuathiri masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki,...."; kama kilivyotaja, Baraza la Wawakilishi linaweza kurekebisha bila ya kuitisha kura ya maoni pale Baraza kwa azimio maalum litakalopitishwa na kuungwa mkono na thetuthi mbili ya Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura.

Sasa nadhani iko haja Mhe. Mwanasheria Mkuu na hili atukubalie hiki kifungu cha 80A ni kifungu ambacho kinaiweka serikali katika mazingira magumu ya kufanya kazi, na sisi ni wasemaji wa wananchi, serikali ikiwekwa katika mazingira magumu ya kufanya kazi mimi nafikiri tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu. Kwa hiyo, vifungu vyote hivi ambavyo vimewekwa na katiba lazima vifanyiwe marekebisho kwa kupigiwa kura ya maoni, kifungu hiki kifutwe na ili katiba yetu iwe kama mwanzo.

Katiba hii tangu mwaka 1979 ilivyoasisiwa kulikuwa hakuna hata kifungu kimoja cha kuweka kura ya maoni, tujiulize kulitokezea nini mpaka tukaweka mazingira magumu katika eneo kama hili.

Vile vile katika kifungu cha 134. Kifungu hiki cha Katiba yetu huku imeelezwa mambo ya jumla Sura ya Kumi na Tatu, inasema: "Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yanahitaji vyenginevyo: "Baraza la Mapinduzi" linajumuisha na Baraza la Mawaziri;

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo nina maneno na ingawa kuna baadhi ya watu hawanielewi vile ninavyokusudia, sasa naomba wanisikilize vizuri ili wanifahamu kile ninachokikusudia.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni nchi ya Kimapinduzi na mpaka leo serikali yetu tunaita Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na Serikali ya Mapinduzi inatakiwa iweke msingi madhubuti kwa chama chochote kitakachoingia madarakani, msingi wa Mapinduzi uendelee kubakia.

Mhe. Naibu Spika, hakuna nchi duniani isiyokuwa na historia na ukitaka kulinda historia yako iweke kwenye Katiba. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nashauri kama ilivyokuwa huko zamani kulikuwa kuna Baraza la Mapinduzi

lakini katika Baraza hilo kuna Baraza la Mawaziri lakini humo humo kuna watu ambao sio mawaziri lakini wanakuwa ni *member* wa Baraza la Mapinduzi ambao wakiitwa MBM.

Sasa ili kulinda na kuhifadhi Mapinduzi ya Zanzibar mimi nadhani Mheshimiwa tutengeneze utaratibu kama alivyosema Mhe. Machano Othman Said Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba tunahitaji katiba hii ifanyiwe *overhaul service,* yaani ifanyiwe marekebisho makubwa ili iweko *think tank* ya Mapinduzi ambao vile vile watakuwa na nafasi ya kushiriki katika vikao vya Baraza la Mapinduzi na ikiwa Mhe. Rais anahisi kuna vikao vyangu vya shughuli tu za serikali sina haja ya kuwashirikisha wale Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi basi anaweza akakaa nao vikao vyengine vya Baraza la Mapinduzi lakini vile vile kuwe na Baraza la Mawaziri.

Mhe. Naibu Spika, sio kila kitu kinaweza kikazungumzwa kwenye Baraza la Mapinduzi ambalo kama hili tulilokuwanalo sasa hivi tuna mchanganyiko wa vyama, huwezi ukazungumza mambo ya msingi ya kulinda ule msingi wako wa asili.

Mhe. Naibu Spika, ninapozungumza hivi nataka nieleweke wazi, kuna wapinzani na kuna vyama vya upinzani, kuna watu hao hata wakiingia ndani ya serikali wanaendelea kubakia wapinzani. Sasa kama leo kuna watu hata wakiingia ndani ya Baraza la Mawaziri wanaendelea kuwa na nyoyo na fikra za upinzani halafu leo mambo gani ya Baraza la Mapinduzi utakayoweza kuyazungumza pale wakaweza kuyasaidia kuweza kufunika ile misingi.

Mhe. Naibu Spika, tusione sasa hivi kwamba tuna Wawakilishi wa vyama vya upinzani ndani ya Baraza la Mapinduzi, lakini tumeshawahi kuwa na wapinzani ndani ya Baraza la Mapinduzi. Kwa ushahidi kamili Mhe. Naibu Spika, wameshawahi kuisaliti serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi hili. Serikali imeleta bajeti yake wapinzani wakaamua kuchukua mabegi yao hao wakatoka mlango huu na sisi tunawatizama. Sasa ninapozungumza hoja hii nakuwa na msingi mzuri, hili Baraza la Mapinduzi ambalo tunataka tuliweke kwenye katiba mtu anaweza akaniuliza sasa hao *fourteen* wenyewe wameshamalizika, *fourteen* wale Mheshimiwa hawamaliziki kwa sababu Mhe. Rais kila anapoteua safu yake ya mawaziri kuna wengine anasema hawa wanaweza wakaja wakawa washauri wangu wazuri.

Hata sasa hivi Mhe. Rais anao washauri, tunayo sheria anao washauri. Kwa hiyo, wale baada ya kuwa washauri wa Rais wanaweza wakawa kama Baraza la Mapinduzi wakawa na haki ya kikatiba, haki ya kimsingi.

Mhe. Naibu Spika, sisi wakati ni wakombozi wa nchi hii hatuwezi hata siku moja tukakosa waasisi, ukienda pale Kisiwandui utawakuta wazee pale wana makoti yao, wale ndio wanaotakiwa wawe waasisi wa Mapinduzi, wale ndio Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, leo kuna watu wamehangaika na nchi hii tunawaacha nje hawana shughuli yoyote, mtu hata pesa ya kula anaikosa. Tuweke Baraza la Mapinduzi wawe ni *member* wa Baraza la Mapinduzi tena wawekewe msingi wa kikatiba hapo nadhani tutaweza kuwa na nguvu.

Vile vile, hii itasaidia kujenga heshima na nidhamu na uwajibikaji kwa Baraza la Mawaziri, kwa sababu leo Baraza la Mawaziri hata wakiwa wanafanya makosa watu ambao wanaweza kusema ni sisi tu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Lakini kama kutakuwa na Baraza la Mapinduzi lile litakuwa limo juu ya Baraza la Mawaziri wataweza kumshauri Mhe. Rais bwana huyu waziri wako aa, muondoe; yaani tunaitengenezea heshima, ile *status* yetu ya Mapinduzi. Kwa hiyo, hayo ndio madhumuni yangu, na hili naliomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu rai yangu hii aichukue.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie usione kwamba labda napenda kusema. Tukija katika michango ya jumla kwenye katiba hii kwa sababu lazima tuweke ile misingi ya kuweza kushauriana vile vile. Hata katika ile Tume ya Uchaguzi yenyewe kuna maadili safari hii yalikiukwa na ndio maana nakubaliana na yale mapendekezo ya kamati kwamba mpaka kwenye Tume ya Uchaguzi kifungu cha 119 kama sikosei lazima tufanye marekebisho, ni nchi ya mwanzo duniani Zanzibar ambayo ina katiba kama hii iliyoweka kwamba hata chama kikishinda kwa asilimia 100 basi lazima waunde Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini vile vile ndani ya tume yake ya uchaguzi kuweza kuweka wanasiasa.

Hili mimi nafikiri sio jambo zuri na kama Waswahili wanasema: "Mtu akitafunwa na nyoka akiona unyasi anashituka". Safari hii uchaguzi wa Zanzibar ulivurugika kwa sababu ndani ya Tume ya Uchaguzi watu walikuwa wanabishana kisiasa sio kwa kazi ile ambayo wametumwa.

Mhe. Naibu Spika, kuendelea kuwabakisha wanasiasa ndani ya Tume ya Uchaguzi nchi yetu hii kila siku itakuwa haiko *stability*, itakuwa haiko *stable*, kila siku tukienda kwenye uchaguzi tutakuwa tunagombana.

Mhe. Naibu Spika, leo Mwenyekiti wa Tume tunamsikia anatangaza vyengine, Wajumbe wa Tume wanatoka wanakwenda kwenye vyombo vya habari wanakwenda kuzungumza mambo kinyume na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, tunakwenda wapi, hata ile *discipline* ya Wajumbe wa Tume haimo, na safari hii sijui kwa kweli ilikuwaje. Kwa sababu moja katika jambo ambalo

Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi kabla kuanza shughuli yao wanatakiwa wale kiapo, na kiapo chao cha kulinda siri za vikao vya Tume, leo niulize wale Wajumbe wa Tume waliotoka wakaenda kwenye vyombo vya habari baada ya tamko la Mwenyekiti hawakukiuka maadili ya viapo vyao?

Sasa haya tusiwalaumu wale tujilaumu sisi tuliotunga hii katiba, kwa sababu tumewaingiza wenyewe sisi kule wanasiasa. Mimi nadhani wakati umefika ndio maana nikamuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora aitendee haki katiba hii. Katiba hii isitengeneze mazingira ya nchi kuwa kila wakati iko tepetepe, haiko *stable*. Kwa hivyo, waondolewe wanasiasa kwenye Tume ya Uchaguzi ili twende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nina mapendekezo katika marekebisho ya katiba hii. Nilikuwa namuomba Mwanasheria Mkuu kama atawahi kukubali katika kikao hiki nitashukuru sana, lakini kama itabidi haya mambo mengine atayawekea utaratibu basi huko siku za mbele nitakuwa sina tatizo sana.

Mhe. Naibu Spika, Kifungu cha 116 cha Katiba, kifungu hiki kimekula mamlaka ya Baraza la Wawakilishi.

Kifungu cha 116 cha Katiba ya Zanzibar kinasema kwamba:

"Kutakuwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi, chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya utumishi wa umma kwa Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kifungu hichi kinakiuka ile demokrasia ya Utawala Bora katika nchi yetu. Kwa sababu tunavyojua kwamba kuna misingi ambayo iliwekwa kwamba Zanzibar itakuwa ni nchi ambayo inaheshimu utawala wa sheria ambayo itakuwa inaongozwa na mihilimi mitatu; Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahakama.

Sasa kama kutakuwa kuna chombo ambacho kitakachokuwa na Mamlaka ya mwisho dhidi ya vyombo hivi vyengine ambavyo ni *Pillars of the Government*. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, iko haja kifungu hichi vile vile tukifanyie marekebisho ili sasa kulipa nafasi na Baraza la Wawakilishi kuweza kufanya mambo yake kwa utulivu.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kifungu cha 74 cha Katiba hii kimekujata wewe Mhe. Naibu Spika. Lakini vile vile ukiangalia kifungu cha 76 cha Katiba hii

kimeitaja Afisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi ambaye amepewa mamlaka kwamba yeye atakuwa Mkuu wa Utumishi wa watumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa kama Katiba tayari imeshampa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kuwa ndiye Mkuu wa watumishi wote wa Baraza la Wawakilishi, leo unaposema kwamba kuna kitu chengine ambacho kiko juu ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi katika masuala ya utumishi mimi nadhani sio haki sana, na ukiangalia maamuzi haya Mhe. Naibu Spika yanapofanyika mpaka yule Waziri anayeshughulikia na masuala ya Utumishi anakuwa anashiriki katika maamuzi yanayofanywa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sasa leo kutakuwa na chombo gani chengine ambacho kitakuwa kina nguvu zaidi kiko juu kupita ile mamlaka ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile kifungu cha 77 ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha nimekupa na muda wa ziada pia umemaliza. Kwa hiyo malizia nakupa dakika 3.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, vile vile namalizia kifungu cha 77 (2) kuna suala zima Baraza la Wawakilishi limetakiwa liunde sheria yake ambayo kutakuwa na Muundo wa utumishi yaani kuwa na ule muundo wake wa utumishi wa Baraza.

Katiba yenyewe imetupa nguvu Mhe. Naibu Spika, mpaka leo Baraza la Wawakilishi tuko hapa hatuna sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu kifungu cha 116 kimezuia uhuru wetu kama Baraza la Wawakilishi.

Kwa hiyo, naomba tuangalie kifungu cha 77(2) kifungu cha 102 na kifungu cha 122 vyombo hivi havitakiwi vitawaliwe na chombo chengine chochote. Kamisheni ya Utumishi wa Umma, kwa sababu kuna Tume ya Utumishi wa Baraza, kuna tume ya Utumishi wa Mahakama na kuna Tume ya Utumishi wa Idara Maalum. Tume hizi zimepewa nguvu ya Kikatiba hazitakiwi vile vile kutawaliwa na sheria nyengine zozote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache nataka niseme nakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii na naamini yapo mengine ambayo nimeyaacha wenzangu wataweza kuyazungumza nakushukuru sana.

Naunga mkono hoja baada ya yale ambayo niliyoyashauri kuweza kukubaliwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Ahsante sana nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu, kuniona na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Mswada wa Marekebisho ya Katiba kifungu namba 66.

Awali ya yote mimi naunga mkono marekebisho yanahitajika, kama tunasema kwamba hii ni nchi ya Kimapinduzi ili Rais wetu tumpe nguvu zaidi yale Mapinduzi aoneshe kweli. Haileti maana kama Rais tunajinasibu kuwa ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar leo hii inakuwa hana maamuzi ya kwake mwenyewe mpaka ashauriane na viongozi wa upinzani au kiongozi wa upinzani.

Kwa kweli kidogo tumemnyima fursa ya kujitanua, Rais ni mtu mkubwa sana, tumempa mamlaka katika nchi hii ione kuwa kuna sababu kwamba lazima washauriane na wapinzani au kiongozi wa upinzani. Kwa kweli kidogo hapa tunamfanya anashubaka, asishubake Rais, Rais awe huru wakati ambapo katiba hii ibadilishwe impe mamlaka Rais kuamua kuchagua watu kumi, labda kwa mapendekezo yake mwenyewe anaona kama anahitaji kuchagua nafasi basi kwa maamuzi yake mwenyewe bila kushauriana na mtu yeyote katika nguvu hiyo.

Vile vile, katika mchango wangu nafikiri nimeleta *schedule of amendment* nilitaka kwamba Baraza hili nalo vile vile lirekebishe kifungu cha 80(2), nilikuwa na maana kwa sababu kama mlivyofahamu kwamba wiki iliyopita nyuma ilikuwa hadithi mjini hapo, sababu oh mswada umekataliwa wa serikali, ile kosa mswada kwa mara ya kwanza na ndio maana yakatokezea yale. Lakini laiti kama mswada ule unasomeka kwa mara ya pili na tatu yasingekuwa yale. Kwa hiyo, ningeomba kifungu kile kisomeke naomba kunukuu:

Mswada wa Baraza la Wawakilishi kuthibitisha Katiba hii kutopitishwa kwa Baraza isipokuwa uwe umeungwa mkono kwa mara ya pili na mara ya tatu katika kusomwa kwa kura si chini ya theluthi mbili.

Mimi nina maana kwamba kisomwe mara ya tatu ndio kipitishwe, kwa sababu juzi tuliakhirisha Baraza baada ya ule mswada mwazo kuletwa tulikuwa hatuna taarifa, na ikafika saa tukaahirisha tusijadili na ikawa nje nyimbo kubwa sana. Nafikiri ingekuwa unasomwa mara mbili tatu yasingetokezea ile. Mwanzo ungewasilishwa na baadae ukaja ukasomwa na baadae na tena tukaupitisha.

Kwa hiyo, natetea mada hii kwamba nayo vile vile tubadilishe ili tuendane sambamba basi kama miswada yote ambayo inayoendeshwa na Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Nitakuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu hili liangalie kabisa kwa jicho la huruma kwa sababu lina faida yake. Juzi kidogo nje tulitikisika vyombo vya habari visivyotutakia mema wanasema manemo mengi juu ya mswada Baraza la Wawakilishi linapinga mswada kwa sababu ya ile ulivyotangulizwa mara ya kwanza. Lakini ingelikuwa laiti kuna nafasi mbili za ziada nafikiri isingetokeo hivyo.

Vile vile naunga mkono kuhusu kifungu cha 119 kubadilishwa. Ni kweli kabisa tumeona au tumejifunza kila tunapopata muda tunajifunza na matukio, safari hii tumepata matukio kama haya yaliyotokea. Kwa hiyo, Tume ya Uchaguzi kama Mjumbe aliyepita alizungumza kwamba wasiwemo wapinzani au wasiwemo watu wa chama kwa sababu kule hakwendi kuzungumzwa siasa, kunaenda kuongewa mustakabali wa nchi namna gani uchaguzi uendeshwe, sasa unapopeleka washabiki wa chama kila mtu atajivutia kwake na ndio maana ikapelekea kama sote ni mashahidi kuona Makamishna, wenyeviti na Wakurugenzi wanavutana kwa sababu wamo katika Tume ya Uchaguzi hiyo nafasi ya Ukamishna.

Kwa hiyo, sioni sababu kifungu kile kuendelea, nitakuomba sana Mheshimiwa na mwenzangu aliyepita alisema kwamba sasa hivi muda umefika kwa kurekebisha katiba yetu. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ina haja ya kurekebishwa, kuna haja ya kuiangalia upya hasa ikae kama Baraza la Mapinduzi iletwe hoja ya kuikarabati Katiba nzima ya Zanzibar hii iko tangu mwaka 1984 kwa wakati ule ilikuwa ni wakati wake. Lakini sasa hivi tunakwenda katika mwaka 2000 na kuendelea. Kwa hiyo, lazima tupate katiba inayoendana na wakati huu tuliokuwa nao wa Sayansi na Teknolojia.

Nitakuomba sana Mhe.Mwanasheria Mkuu hilo ulipendekeze na Baraza lako hili litakuwa pamoja na wewe katika kusimamia kwamba katiba hii tunaifanyia mabadiliko. Vile vile kama Mjumbe aliyepita mengi ambayo niliyokuwa niyaseme mimi Mhe. Hamza Hassan Juma kanimaliza. Kwa hiyo, sitopoteza muda sana lakini makubwa zaidi nasimamia kwenye *schedule of amendment* yangu kwamba nitakuomba sana Mhe. Mwanasheria basi tufanye marekebisho, hiyo miswada nayo isomwe mara ya tatu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niwe niongoni mwa wanaochangia kwenye mada hii ya marekebisho ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli naomba kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara zake kubwa anazozitumia kuiongoza nchi yetu.

Kwa kweli anabeba mengi, kuna watu wasiopenda maendeleo wanazungumza maovu dhidi yake, wengine wanazungumzia ufedhuli na wengine wanazungumza hata matusi. Lakini bado anastahamili na nchi inaendelea na maendeleo yanaendelea kupatikana. Asiyeyaona anajifanya kipofu, lakini maendeleo yapo na yanazidi kuendelea.

Pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, ni mwenzetu na muda wote tunaye kwenye Baraza hili na yeye pia mengi sana ameyapata; ya matusi, kukashifiwa lakini bado msimamo wake uko pale pale kuiendeleza Zanzibar kwa manufaa ya Wazanzibari. Hongera sana Mhe. Makamo wa pili wa Rais.

Pili nilipongeze Baraza la Wawakilishi la mara hii limetanua demokrasia, viko vyama vinne humu vya siasa ambavyo vinashikiri kwenye Baraza hili la Wawakilishi ni kwamba demokrasia imepanuka, asiyeona pia anajifanya kipofu.

Baraza hili limekuwa likiendelea na mijadala yake wakati mwengine inakuwa mijadala mikali lakini hamna kususiana na sijapata kuona hata Mwakilishi mmoja akatoka nje kwa kususia mada fulani iliyozungumzwa, hongera sana Baraza la Wawakilishi.

Napenda nimpongeze Mwenyekiti wa Tume maana nikiipongeza Tume itakuwa nakwenda kinyume kwa sababu kuna wengine hawastahiki pongezi walituharibia. Mwenyekiti wa Tume kwa kweli anastahili pongezi kubwa sana, huyu ni mfanyakazi jasiri anayejali sana demokrasia. Kwa kweli ingekuwa katiba inaruhusu basi *wallahi laadhim* ninasema huyu aendelee kuwa Mwenyekiti wa Tume hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Naunga mkono hoja hizi ya kubadilisha katiba, naunga mkono sana kwa asilimia mia mabadiliko haya ambayo tunakwenda nayo ya katiba hii, kwa sababu nchi yetu ni nchi ya demokrasia na demokrasia ndio msingi wa maendeleo, wananchi wetu wanataka demokrasia mambo yaende kwa usawa ili waweze kupata yale wanayoyatarajia.

Demokrasia ikiambatana na fujo hasa ikifanywa na Vyama vya Upinzani ambavyo pengine vina watu wanaowafuata basi wanaharibu demokrasia na

wanakwaza maendeleo. Kwa hivyo, mimi nashauri sana msajili aviangalie vyama vya upinzani vinavyoleta fujo.

Juzi hapa katika Jimbo langu la Mtopepo tulikuwa tunafanya hesabu za watu kwa madhumuni mazuri, kwa sababu ukijua ile hesabu ya watu utajua maji lita ngapi uwapatie kwa kiasi gani, utajua barabara zetu tuzijenge vipi, utajua mambo ya maendeleo uyafanye vipi hata chakula.

Leo anatokea mtu watu wanakaribia kumaliza makaratasi anayachukua anakimbia nayo, polisi walijaribu kufuatilia hili suala na mimi niwashauri polisi walichukulie hatua kali sana, huu si uungawa kabisa kama una lako la kufanya basi wewe nenda kwenye vyombo vinavyohusika au kaa pembeni hutaki kufanya, hivyo wanavyofanya watu kwa niaba ya wananchi basi wewe huna haki ya kukaa kwenye nchi hii kama unapo pa kwenda bora uendee.

Mimi nasema tena kwamba kwa yeyote yule ambaye haendani na maadili ya maendeleo, anapinga demokrasia basi achukuliwe hatua zinazostahiki, mahakama zipo, sheria zipo, wanasheria wapo, vitendo vya hujuma vinafanyika. Kwa hiyo, vitendo hivi viangaliwe kwa makini sana na viweze kuchukuliwa hatua ili yasitokezee yanayoweza kutokezea.

Nimekuwa nikishuhudia Baraza la Wawakilishi lililopita nilikuwa nikiangalia sana Baraza hili. Alikuwepo mtu anazungumza mpaka najiuliza huyu hatatapika, anazungumza kwa jazba kubwa sana kiasi kwamba yuko tayari kama mtu atamsogelea apigane. Haya mambo kwenye Baraza hili nimesema tangu mwanzo pale hayapo na tuzidi kuendelea kuwa imara, tuelewane, isitokee mizozo kama hii, kwa sababu kila mtu ana njia zake za kumtetea mwananchi.

Ukimtetea mwananchi kwa jazba ukapandikiza hasira, chuki, wewe utakuwa hufanyi kitu cha maana. Kwa hivyo, na mimi sitaki kuchukua muda mrefu naomba niseme tena kwamba naunga mkono mabadiliko ya katiba.

Lakini katika demokrasia hakuna mabadiliko ya haraka. Mabadiliko ya haraka haya ni ya kimapinduzi tu, inapotokea Mapinduzi nchi inapinduliwa hayo ndio mabadiliko ya haraka yanakuja. Lakini kwa nchi ya demokrasia mabadiliko yanakwenda pole pole. Kwa hiyo, twendeni na mabadiliko haya pole pole tutakwenda hadi tutafikia pale ambapo tunataka.

Baada ya kusema haya Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa leo kunipa nafasi ya mwisho kwa wachangiaji kabla ya mawaziri.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wangu wa jimbo la Welezo kwa kunichangua kwa kura nyingi kuja humu kuwatetea wana Mapinduzi wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Pili nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na serikali yote kwa jumla kwa kuleta Mswada huu wa Mabadiliko ya Katiba ambayo tutayapitisha punde.

Mhe. Naibu Spika, naomba kusema wazi wazi kwamba naiunga mkono hoja hii mia juu ya mia kabla sijaanza kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, ukweli usiopingika kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein inafanya mengi ya maendeleo ambayo hakuna hata mmoja asiyejua kama serikali ya awamu wa saba imejidhatiti kuhakikisha Wazanzibari wanaendelea. Ingawaje kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Naibu baadhi ya watu ambao wamo ndani ya serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar na wanalipwa mishahara na wanafanyiwa mambo mengi mazuri lakini bado wamekuwa ni wapinga Mapinduzi, Maendeleo na baadhi yao wamekuwa si waaminifu na ni wezi. Mhe. Naibu Spika sasa naomba kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, leo tunachangia kitu kimoja kikubwa sana katika historia ya Zanzibar, ambacho Hasssan Khamis Hafidh na mimi nikiwa Mjumbe wa Baraza hili la Tisa kikao cha tatu.

Mhe. Spika, tunabadilisha baadhi ya vifungu. Kifungu cha 66 ambacho tunakibadilisha Mhe. Naibu Spika, nitaomba nikisome.

> "Isipokuwa kwamba Wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au kwa kushauriana na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani".

Mhe. Naibu Spika, mswada huu tutaupitisha lakini mimi kama Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Welezo huwa inaniuma sana kuona

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi eti mpaka ashauriane na Kiongozi wa upinzani, ashauriane na vyama vya siasa.

Mhe. Naibu Spika, mswada tunaupitisha lakini lazima imefika wakati katiba hii tuje kuichambua upya, haya mambo kwamba Rais wetu ashauriane na vyama vya upinzani, ashaurine na vyama vya siasa hayatufai.

Uraisi si kitu kidogo, wapo wengi walioutamani, wapo wengi wanautaka, lakini hawajaupata. Urais wa Zanzibar kuna watu wanautafuta kwa miaka isiyopungua 30 lakini bado hawajaupata na Rais aliyemtaka Mwenyezi Mungu ni Dkt. Ali Mohamed Shein ndiye Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anayetoka Chama cha Mapinduzi, na ajaye mwaka 2020 pia anatoka Chama cha Mapinduzi, mpaka Kiama nchi hii itaendelea kuongozwa na Chama cha Mapinduzi. Kwani ndiyo Mwenyezi Mungu anayejua kwamba Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoweza kutoa viongozi makini, wenye kuwatakia maendeleo wananchi wa Zanzibar kila uchao. (*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika, pia Kipengele cha 119 kuhusu Tume ya Uchaguzi. Ukikiangalia pia kinasema, "Wajumbe wawili watateuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi, au iwapo hakuna Kiongozi wa Upinzani basi kwa kushauriana na Vyama vya Siasa".

Mhe. Naibu Spika, pia mimi siwafiki maneno ya kwetu shamba, Rais wa Zanzibar utakapopata Urais, wewe ni Rais. *Qur-an* imemtaja Rais, *Bible* imemtaja Rais, vitabu vyote vya dini vimemtaja Rais na vimempa uwezo Rais na ndiyo maana kuna wengi wanautamani. Ndiyo maana kuna wengi wanautaka na Mwenyezi Mungu hajawajaalia. Aliyemjaalia Mwenyezi Mungu Urais ndiyo keshamjaalia. Nyimbo moja imesema,"*Aliyepewa kapewa, Mpewa hapokonyeki*". (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninasema tena Rais wa Zanzibar hakuna haja ya kushauriana na Kiongozi wa Upinzani, hakuna haja ya kushauriana na Vyama vya Siasa, atakapokuwa Rais wa Zanzibar basi maamuzi yawe yake mwenyewe, labda akiona tu mwenyewe ni maamuzi yake, akiona inafaa aweze kuteua mtu kutoka katika Vyama vya Upinzani akiona inafaa. Lakini siyo kushauriana wala kushauriana na Vyama vya Siasa, aah. Urais siyo kitu kidogo, Urais ni kitu kikubwa na ndiyo maana umetajwa katika Msahafu, umetajwa katika vitabu vyote vya dini Mhe. Naibu Spika.

Pia Mhe. Naibu Spika, Kifungu cha 134 cha Katiba inaweka Baraza la Mapinduzi ambalo ndani yake muna Mawaziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi tangu udogo wangu nilikuwa ninasikia mapinduzi, na nilipokuja kupata fahamu yangu ya kibinadamu kusoma historia, kuwauliza wazee na kuuliza mababu, nikajua kumbe sisi Wazanzibari yaliyotuokoa ni mapinduzi matukufu ya Januari, 1964. Ushahidi wote huo upo, dunia nzima unaonesha. Sasa leo hii nchi hii mimi Hassan mtu wa kwanza ninayemchukia anayepinga mapinduzi ya Januari, 1964. Huyo ninakuwa simpendi, na ndiyo maana kauli zangu zote ndani ya Baraza hili ninayapongeza na nitayatetea, kuyalinda na kuyadumisha mapinduzi matukufu ya Januari, 1964.

Ninaamini ndiyo yaliyoniokoa mimi mkwezi na mkulima, mshamba wa Mchangani na wenzangu katika kutuletea maendeleo ya taifa hili. Siruhusiwi kusema mapinduzi oyee! lakini ningekuwa ninaruhusiwa na Baraza hili leo ningeyasema Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa unaposema kuna Baraza la Mawaziri, Katiba inaruhusu lakini ndani ya Baraza la Mawaziri kuwe na Mawaziri wengine wanatoka katika Chama cha Upinzani ambao hawathamini wala hawayatambui mapinduzi. Mimi hapa ninapata mashaka. Atakuwaje Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awemo ndani ya Baraza la Mapinduzi, awe Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi lakini nafsi yake hayatambui wala hayataki mapinduzi matukufu yaliyotuokoa. Huyo kweli anahusika kuingia katika Baraza hilo? Katiba inaruhusu lakini mimi Hassan naona ndiyo ninaposema ipo haja ya kuichambua Katiba hii upya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na Baraza hili la Tisa limejidhatiti kidhati kabisa katika kutaka kuichambua Katiba hii. Kwa sababu tunaona baadhi ya vipengele haviendani na azma na malengo ya mapinduzi matukufu ya Januari, 1964 yanakinzana nayo ambayo yamo ndani ya Katiba, waliyatia watu kinyemela kwa maslahi yao binafsi, ambayo mambo hayo wazi kabisa yanapingana na dhamira ya mapinduzi ya Januari yaliyokuja kutukomboa sisi wakulima na wakwezi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Baraza hili la Tisa limejidhatiti kuyalinda, kuyatetea na kuyadumisha mapinduzi matukufu ya Zanzibar katika kutimiza azma yake ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ni lazima Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iendane na matakwa na malengo ya mapinduzi ya Januari, 1964. Muna vipengele humu vinakinzana na malengo ya mapinduzi ya Januari, 1964. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ni lazima tuje tuichambue upya Katiba hii. Kwa leo tunaikubalia Serikali kuipitishia Kifungu hichi walichokileta kwa sababu ni Serikali yetu ya mapinduzi hatuwezi kukataa, lakini tunaiomba Serikali nayo tukae upya kuichambua Katiba hii ili iendane na malengo ya mapinduzi matukufu ya Januari, 1964.

Mhe. Naibu Spika, mwisho huwa tunafanya utafiti. Utafiti unajiuliza hivi kwa nini Zanzibar au na baadhi ya nchi za Kiafrika huwa haziendelei. Kwa Zanzibar ukifanya utafiti kwa nini inakuwa kila siku tuna mashaka, unagundua kuna mambo matatu makuu ambayo mimi kwenye baadhi ya hotuba zangu zote huwa ninayasema.

Mhe. Naibu Spika, utafiti unaonesha Rais wa Zanzibar wa Awamu wa Saba yupo kuyatekeleza kwa vitendo, kuyalinda, kuyatetea na kuyatekeleza mapinduzi matukufu ya Januari, 1964 yenye malengo ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar wakwezi na wakulima.

Lakini Namba mbili Mhe. Naibu Spika, Rais wa Zanzibar unamuona hasa kajidhatiti katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na kuwaondoshea umaskini.

Mhe. Naibu Spika, pia unamuona Rais wa Zanzibar na Serikali yake walivyojipanga katika kuwaletea maendeleo lakini baadhi ya watu wamo ndani ya Serikali hii wanalipwa.

Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuja mimi nilikuwa mtendaji wa Serikali, mshahara wangu ulikuwa mwembamba, baada ya kuja kuongezwa mshahara, mshahara ukapanda unaona *'yes',* na hivi ameahidi tena mwezi wa nne mwakani ataongeza mshahara. Ninafikiri kwa historia ya Zanzibar Rais wa Awamu ya Saba Dkt. Ali Mohamed Shein ndiye Rais pekee aliyekuja kuongeza mshahara kwa kiwango alichoongeza na kufanya marekebisho ya mshahara kwa mara mbili au tatu, bila ya kujali kwa sababu anawatakia kheri wananchi wa Zanzibar ili umaskini ututoke hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna watu Serikali inajitahidi kuyalinda mapinduzi, lakini kuna watu wanayabeza mapinduzi na wamo ndani ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Serikali inajitahidi kuleta maendeleo kwa wananchi wake lakini kuna watu bado wanajitahidi na wao kuyabomoa maendeleo na Serikali. Serikali inajitahidi kuwainulia maisha Wazanzibari wa nchi hii ili waneemeke lakini kuna watu wanaizunguka ukuti Serikali wanafanya wanavyotaka wao, wanakuwa siyo waaminifu, wengine wanakuwa wezi.

Mhe. Naibu Spika, sijui kipengele gani cha Katiba, kama ninaulizwa na mimi kirekebishwe. Hawa wapinga mapinduzi, hawa wapinga maendeleo na hawa wezi na waliokuwa si waaminifu ambao Serikalini bado wamo na tunawatafuta. Ninamuahidi Mhe. Rais kwamba Baraza hili la Tisa kama tulivyoanza tutawatafuta, tutawasema hapa wale wote wapinga maendeleo, wapinga mapinduzi na wale waliokuwa sio waaminifu, wezi tutawasema hapa hapa.

Tunampongeza Mhe. Rais kwa kuwachukulia hatua wale wote wezi, wapinga maendeleo na wapinga mapinduzi tuliowataja na yeye akawachukulia hatua. Pia tunampongeza Mhe. Waziri tulipowataja wezi wa Wizara ya Fedha ambao wanakinzana na malengo ya mapinduzi aliwachukulia hatua. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Tisa tutaendelea kuwatafuta na kuwaibua wale wote wapinga maendeleo, wale wezi na wale wapinga mapinduzi ili nchi yetu iendane sambamba na matakwa ya mapinduzi na kumsaidia Rais wetu katika kuiletea maendeleo Zanzibar yanayofaa.

Mhe. Naibu Spika, hakuna asiyejua kama umaskini ni kitu kibaya, hakuna asiyejua kama umaskini hatuutaki, lakini Serikali inajitahidi kila uchao kuhakikisha umaskini inauondosha.

Mhe. Naibu Spika, nilisema na Marehemu Mandela kasema, *"Poverty is a man-made"*. Umaskini ni kitu kinacholetwa na mwanadamu, ni sisi tunaoleta umaskini, tuna jukumu la kuuondosha.

Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba naomba sana kuunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia, lakini pia napenda kusema kama tutasema utaratibu unaofaa katika kuleta mapendekezo yetu Katiba hii tuichambue neno kwa neno, tuichambue mstari kwa mstari, tuichambue *paragraph* kwa *paragraph* ili Katiba hii iendane na malengo na matakwa ya mapinduzi matukufu ya Januari, 1964. Haiwezekani kuwe na Serikali ya Mapinduzi ndani yake muwe na Mawaziri, Katiba inaruhusu muwe na Mawaziri ambao hawatambui mapinduzi ya Januari ya 1964 yaliyokuja kumkomboa mkwezi na mkulima. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa, naomba sana kuunga mkono hoja na naomba na wenzangu wote waunge mkono hoja hii ya Serikali ili tuweze kupitisha kwa haraka iwezekanavyo.

Katiba impe nguvu Rais aweze kufanya anachoweza kufanya kwa sababu huyu ni Rais wa mapinduzi, mwenye kulinda maslahi ya wana mapinduzi wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hassan. Sasa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) na baada ya hapo atakuja Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi ninataka kusema kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tujitambue na tutambue na tuwe na historia kwa taifa letu la nchi yetu; wapi tumetoka na wapi tulipo.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu iliingia katika vuguvugu la siasa miaka ya nyuma iliyopita na misuguano, ilikuwa ni jambo baya na la aibu kwa dunia ya sasa, pale siasa ilipotufikisha pabaya tukaamua kuuwana sisi wenyewe kwa wenyewe, ndugu wa baba mmoja. (*Makofi*)

Lakini kwa bahati nzuri viongozi wa nchi yetu na Serikali yetu, Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi (*CUF*) walikaa pamoja katika kuleta muafaka. Ukaja muafaka wa kwanza ukasimamiwa na Chief Emeka Anyaoku, lakini kwa bahati mbaya haukuleta manufaa kwa taifa letu. Bado nchi yetu ikakumbwa na dhiki na mambo ya aibu ya kususiana na kutokushirikiana. Lakini Mwenyezi Mungu akajaalia Chama cha Mapinduzi na Chama cha *CUF* kikakaa pamoja na mimi ninawapongeza wakaleta muafaka. Muafaka huu ukaja ukazaa Katiba hii ambayo kuwa leo hapa tunayo.

Bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, hii Katiba wakati inatungwa, ndani ya Baraza hili wapo Waheshimiwa walishiriki katika kuitunga hii Katiba. Sasa ninachotaka kusema kwamba kwanza tukumbuke kuwa sisi tupo kwenye ulimwengu, hatupo peke yetu.

Mhe. Naibu Spika, Tanzania inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Tanzania tuliingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa 1992 na CCM iliridhia. Ninawapongeza sana viongozi wa CCM na viongozi wa Serikali. (*Makofi*)

Mimi ninakubaliana na Kifungu cha 66 kilicholetwa na Mhe. Waziri kinachosema kwamba, "Rais ashauriane na Vyama vya Siasa". Kwa sababu dunia ya sasa huwezi kufanya kitu wewe mwenyewe peke yako, vyama vyengine ukaviacha. Tukumbuke kwamba ni sisi tuliotunga Katiba hii. Kwa hivyo leo unapokuja ukasema kwamba aah! Rais aamue tu vyovyote vile haiwi. Ninampongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein.

Huku nyuma wakati anataka kuunda Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, hii tuliyonayo leo, pamoja na kwamba Katiba inasema Rais achague viongozi wawili kwenye Vyama vya Siasa vya Upinzani. Lakini Dkt. Ali Mohamed Shein ameteuwa Wajumbe watatu kutoka Vyama vya Upinzani. Kwa kweli ni jambo la kupigiwa mfano na tutamkumbuka kwa jambo jema na zuri alofanya. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, alichokifanya Rais alitwita Vyama vya Siasa pale Ikulu. Tukaenda kwa nia njema tukashauriana na Mhe. Rais, na Mhe. Rais akaenda mbali zaidi, akasema basi au akaamua badala ya kuchagua Vyama viwili, akachagua Wajumbe watatu. Wawili walitoka Chama cha CUF mpaka leo wamo; Mhe. Nassor na Mhe. Ayoub na watatu Mhe. Haji Ramadhan kutoka Chama cha SAU. Hii ni kujenga utawala. (*Makofi*)

Sasa Kifungu alichokileta Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ninakiunga mkono kwa sababu kinasema badala ya Rais kukaa na Kiongozi wa Upinzani au kukaa na Vyama vya Siasa vilivyopo ndani ya Baraza, hii Katiba sasa inasema, atashauriana na Vyama vingi vya Siasa. Unaposema sasa kama Rais ashauriane na Vyama vya Siasa, hii ndiyo kujenga demokrasia na utawala bora. Kwa sababu kuna msemaji mmoja alisema hapa kwamba huu ulimwengu sasa lazima na vyama vipewe nafasi. Kwa sababu leo unaposema kwamba Rais achukue yale mawazo ya vyama vyengine, vile vyama vinapeleka majina, halafu Rais anaangalia ni chama gani na chama gani. Ndivyo tokea kuipata Tume hii. Mimi Chama changu hakikubahatika kuingia kwenye Tume ya Uchaguzi lakini nimeridhia na nimefurahi. Hata baadhi ya vyama vyengine kwa sababu huu ndiyo ushirikishwaji wa demokrasia. Kwa hivyo ninachotaka kusema kwamba Mswada alioleta Mhe. Waziri kwa Kifungu hichi cha 66, mimi ninakiunga

mkono. Lakini tusiwe na mawazo kwamba sasa kuunda Tume ya Uchaguzi kuwa tuvunje ile misingi, lazima tukumbuke misingi ya Katiba hii ilikujaje.

Hii misingi ya Katiba ilikuja baada ya misuguano mikubwa ya kisiasa katika taifa letu kwenye nchi yetu. Sisi kazi ya Baraza la Wawakilishi au Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupime upepo wa siasa unavyokwenda. Tuangalie mustakabali wa taifa letu, tuangalie hatma ya nchi yetu. Sisi leo tupo kwenye chombo hichi lakini kesho na keshokutwa hatupo, watakuja wengine.

Kwa hivyo unaposema leo kwamba Tume ya Uchaguzi kusishirikishwe Vyama vya Siasa, mimi hili siungi mkono. Kwa sababu lipo kwenye Katiba, hatuwezi tukaichezea Katiba. Unaposema leo kwamba kusiwe na Makamo wa Kwanza wa Rais, jamani hili lipo kwenye Katiba. Twende kwenye hoja.

Kifungu cha 66 mimi ninakiunga mkono kilicholetwa na Mhe. Waziri, hatuwezi leo tukakaa hapa tukasema kwamba tufute nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tufute kusiwe na Wajumbe kutoka Vyama vya Upinzani kwenye Tume ya Uchaguzi. Jamani tupime upepo wa siasa na tumsaidie Rais kulinda amani na utulivu katika nchi yetu, tusichafue upepo wa siasa. Tukiona kama kuna jambo halileti mustakabali wa taifa, lazima tuliseme na tulitetee, tuzungumze lakini tupime na hali, tuangalie na kwamba sisi tupo katika mfumo wa vyama vingi. Vyama vingi havikuja tu hivi hivi, vilikuja kutokana na mfumo wa dunia, vilivyokuja na mfumo wa kisasa.

Dhana ya utawala bora, dhana ya mashirikiano, dhana ya umoja. Hivyo, leo unambagua mtu kwa sababu hayupo kwenye chama chako. Siyo sahihi, tubadilike, tujenge uzalendo. Umuhimu mtu unampima Mhe. Naibu Spika, kwa utu wake, kwa uzalendo wake na uaminifu wake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na watu wapo kwenye Chama cha Mapinduzi na walifika kuwa viongozi wakubwa katika taifa hili. Lakini watu wale wale leo baadae wametoka wamekwenda kwenye upinzani na wametoa changamoto kubwa sana. Sasa hebu niambie, huyu mtu alikuwa ni kada mkubwa wa Chama cha Mapinduzi, leo yupo kwenye Chama cha Upinzani na akawa mgombea wa urais wa Jamhuri wa nchi hii. Hebu tupime, je, kuna aliyetegemea kwamba lile lingetokezea. Lakini unaweza kukuta kumbe kwenye Vyama vya Upinzani kuna watu wana mawazo mazuri na kuna watu wana nia nzuri kwa taifa hili. (*Makofi*)

Sasa tusikae hapa tukasema kwamba aah! vyama visishirikishwe. Hili bwana ni taifa letu, ni nchi yetu sote! Hakuna chama chochote chenye hati miliki na taifa hili na nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, sisi Wazanzibari, sisi Watanzania ndiyo wenye hati miliki na nchi hii na taifa hili. Ifike wakati kwanza tujue ni jambo la aibu kusema kweli, kuona kuwa Mheshimiwa unategemewa kwenye jimbo, unakuja hapa unasahau kwamba nchi yetu tupo kwenye mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ifike wakati utufanyie semina elekezi. Watu wanatusikiliza, watu wanatafakari na kupima. Hapa hatupo kwenye kulumbana, hapa hatupo kwenye siasa. Tutizame hoja iliyoletwa na Mhe. Waziri, mimi ninaiunga mkono Kifungu hichi cha 66 na mimi Mhe. Naibu Spika, ninampongeza sana Mhe. Rais wetu, tumepata Rais kusema ukweli ni wa historia.

Ni Rais kwa mara ya kwanza aliongoza Dkt. Ali Mohamed Shein, Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mara ya kwanza, yeye ndiye aliyeongoza. Hatutomsahau, na kwa kweli aliongoza kwa hekma na busara kubwa, alikumbana na watu ndani ya Serikali yake wanaompinga na wasiompinga, pamoja na misuguano na figisufigisu za kisiasa, lakini Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya kazi katika kipindi cha miaka mitano kwa usahihi na kwa uadilifu mkubwa, na akailinda katiba yetu.

Kwa kweli kaonesha mfano mzuri, hebu tuige mfano wa Rais. Sasa hivi awamu yake ya pili, kuwepo sisi hapa mimi na Mhe. Said Soud na Mhe. Hamad Rashid ni yale yale kutokana na malengo na misingi mikubwa ya katiba yetu.

Katiba iliyotungwa na Baraza tukufu la Wawakilishi, wakiwemo baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamo leo humu, kwa sababu sisi imefika wakati kama wadau wa siasa tulishirikishwa katika kutoa maoni, tulishirikishwa kwenye kamati ya sheria, hata Mhe. Haji Omar Kheri pale waziri atakumbuka hilo jambo.

Kwa hivyo, lazima ifike wakati tukumbuke, tujue nini cha kuzungumza na nini cha kufanya. Mimi siwafiki kwamba tuondoe nafasi leo ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tuondowe Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, Mhe. Naibu Spika, hili mimi siliungi mkono. Naona unazungumza. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachotaka kusema Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi, kwa unyenyekevu nawaombeni kwamba tusome Katiba na sheria, yako mambo

makubwa unapotaka kuyabadilisha ni lazima uitishe kura ya maoni. Lakini viko vifungu vidogo vidogo kwa mamlaka ya Baraza la Wawakilishi tunaweza tukabadilisha, lakini vile vile tujue na hatima yetu, tusisahau tu tukataka kwamba kila kitu tukombe tuchukuwe sisi tu, lazima demokrasia ifanye kazi, demokrasia ichukue nafasi yake. Mhe. Naibu Spika, naona kuna mazungumzo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba sana tumsikilize Mhe. Mjumbe. Wengine tumechangia tumesikilizwa, kwa hivyo na yeye tumsikilize, tafadhalini sana.

Mhe. Juma Ali Khatib: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Sisi kila mjumbe anayezungumza tunakaa kimya tunasikiliza, sasa na sisi watufanyie haki. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninachokisema Mhe. Naibu Spika, sisi tumejifunza yale makosa yaliyopita kwenye nchi yetu, tulikumbwa na shetani mbaya. Mwenyezi Mungu katujaalia yule shetani mbaya kaondoka. Sisi sasa hivi tunataka serikali yetu iende mbele, tunataka amani na utulivu uendelee.

Nampongeza sana Mhe. Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa kufanya kazi nzuri, na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuleta kifungu hiki, naunga mkono sana. Lakini tusitie mambo mengine ambayo hayamo kwenye hii hoja, hayamo kwenye haya mabadiliko, itakuwa kama vile tunatonesha vidonda au vigaga. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukumbuke kwamba sisi wajibu wetu ni kuhakikisha taifa letu au nchi yetu inamaliza miaka mitano na mengine ijayo tukiwa katika hali ya amani na utulivu na mshikamano wa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii iliyoletwa na kifungu hiki namba 66. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja iliyoletwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa sababu ndio makubaliano ya Baraza la Mapinduzi. Sasa mwengine yeyote aliyeleta hoja yake ndani ya mfuko, atabakia nayo kwenye koti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kabla sijasema naomba nisome utangulizi. Wanasheria wanajua, kitu kinachoandikwa na kwa kuwa wanasheria wanaelewa hilo, 'na kwa kuwa tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na

viongozi wa Mapinduzi wakiongozwa na muasisi wa Chama cha *ASP*, na Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima kizazi baada ya kizazi, katika kupambana na ukoloni, ubepari, unyonge, uonevu na dharau na badala yake kudumisha uhuru na umoja, haki na usawa, heshima na utu'. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, maneno haya ni makubwa sana. Lakini kwa kutaka kuwaambia baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wasioelewa, kwamba mwaka 1964 Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 hadi mwaka 1984 nchi hii haina katiba.

Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 hadi mwaka 1984 Zanzibar ilikuwa inakwenda haina katiba, inakwenda ki- *decree*, basi. Hii imeanzishwa mwaka 1984 baada ya Baraza la Wawakilishi la kwanza la mwaka 1980 kutunga sheria. Sasa basi, kama kuna mwakilishi anayetaka kuirudisha Zanzibar kwenye miaka ya 1964 kachelewa, hana wakati huo tena, hawezi na hawezi kuirudisha Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya dunia, na dunia inakwenda mbele, dunia hairudi nyuma. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni vizuri sasa tukawa tayari kuheshimu katiba, na kuelewa kwamba katiba hii ya marekebisho ya 10 yalifanywa kwa sababu zipi.

Marekebisho ya 10 yalifanywa kwa sababu nyingi zilizojitokeza ikiwemo kufa kwa Wapemba wengi sana, katika tarehe 27 mwaka 2001. Wapemba walikufa wengi sana, serikali ikatangaza Wapemba 67, tunakubaliana na 67. Lakini walikufa wengi sana kwa kudai demokrasia. Sasa leo anatokea mtu anakuambia aah! maana yake vyama vingi viondoshwe, viondoshwe? *(Makofi)*

Vyama vingi viondoshwe, yaani viondoshwe vipelekwe wapi?

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Na Zanzibar imekuja, imetawala, inatawaliwa na mfumo wa vyama vingi vya demokrasia.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, naomba uzungumze na kiti.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye mada.

Mhe. Naibu Spika: Haya ahsante.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Kwa sababu tu nataka niseme hivi, huwezi leo ukawa mwakilishi ama ukawa Mkuu wa Mkoa, au ukawa Mkuu wa Wilaya, ukaja ukasema kwamba mimi nataka kifungu hiki kifutwe. Zingatia kwanza kilikuja kwa sababu zipi. Sababu zilizoleta kifungu hiki ni sababu nzito, ngumu na mbaya! Kwa sababu nyinyi mnaiona hii katiba ya Zanzibar labda mnayo mikononi mwenu tu. Lakini hii katiba ya Zanzibar iko Jumuiya ya Madola, katiba ya Zanzibar iko Umoja wa Mataifa na maelezo yote haya yamo, wewe unataka kuifuta kwa kusema nini, yaani uwende ukaseme kule Umoja wa Mataifa kama katiba ya Zanzibar tumeifuta.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanapiga hatua kila siku wanakwenda *ICC*, wanakwenda Marekani na kwengine, wakifika wanaoneshwa hii serikali ni ya Umoja wa Kitaifa, ndio. Wanaulizwa mabalozi ndio. Wewe ukitaka kuona jina langu, labda unaweza kuliona katika Gazeti la Uhuru, liko Marekani, kwamba hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Said Soud yumo, Juma Ali Khatib yumo, Hamad Rashid yumo, ndio maana ukakuta *peace in Zanzibar* imetengenezwa na nani, imetengenezwa na viongozi wakuu wa nchi hii. Akiwemo Rais Magufuli, akiwemo Mhe. Seif Ali Iddi, Dkt. Ali Mohamed Shein, wamesimamia uadilifu wa katiba hii.

Leo mnakuja hapa mna mambo yenu mfukoni, ooh! maana yake waondoshwe, Rais asikae na vyama vya siasa. Akakae na nani? Rais akakae na nani sasa. Maana hii mnampinga Rais asikae na vyama vya siasa. Kifungu namba 119 Rais akae na nani kuteuwa haya mambo. Nisikilize vizuri, akakae na nani. Wajumbe mlipokuwa mnachangia…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan kaa, naomba ukae kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe: *(Walipiga Makofi kwa wingi sana na kwa muda mrefu)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Muongozo wako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Sawa. Mhe. Said Soud naomba ukae kidogo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, natumia kanuni ya 48

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan sijakupa ruhusa ya kuzungumza. *(Makofi)*

Sasa nakupa ruhusa nyanyuka uzungumze. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kanuni ya 48 inatupa muongozo wa kuchangia mjumbe ajenge hoja. Mjumbe mpaka hivi sasa aliposimama anazungumza maneno ya watu, hajajenga hoja katika kifungu chochote cha katiba ambacho yeye anahisi pafanywe marekebisho au anaboresha.

Mhe. Naibu Spika, kama hatukwenda kwa utaratibu, basi itakuwa hapa kama tuko marikiti tunabishana na tunalumbana. Kama ana hoja basi atafute kifungu ajenge hoja zake kama tulivyofanya sisi wengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri nenda kwenye hoja inayozungumzwa hapa leo.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwa mara ya kwanza nimesema naunga mkono hoja, kifungu namba 66 kinachosema Rais

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ni mazungumzo yako ndio yanatakiwa yaende kwenye hoja.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ndio nasema naunga mkono hoja Mhe. Naibu Spika. Lakini kama niende kwenye vifungu, basi nakwenda kwenye vifungu. *(Makofi)*

Kifungu namba 66 cha katiba hii kimempa mamlaka Rais kukaa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ili aweze kuzungumzia nafasi mbili za wajumbe kutoka kambi ya upinzani. Lakini Baraza la Mapinduzi kwa sababu ndio chombo pekee chenye mamlaka katika nchi hii, kikaonelea mbali kwamba iko haja sasa kumpa Rais uwezo wa kuteuwa wajumbe anaowataka bila ya kumuita Kiongozi wa Upinzani, na hilo sisi tumekubaliana nalo, kwamba anao uwezo huo Rais wa kufanya hivyo. Kwa nini basi, Rais kwa sababu ya kupenda demokrasia na kuheshimu demokrasia ya Tanzania, nafasi hizo mbili pia anazo katika katiba hii hii, inayomfanya anapotaka kuunda Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kuwaita viongozi wa vyama vya siasa. Kati ya viongozi wa vyama vya siasa kumi walioitwa na Rais na mimi nilikuwemo. Rais akatoa maelezo yake kuhusu muundo wa Tume ya Uchaguzi.

Nina imani mwaka 2018 Tume ile itakapomaliza muda wake, Rais ataendelea kufanya yale yale ya kuita tena vyama vya siasa kama katiba hii inavyomuelekeza. Sasa napinga hoja ya mtu ambaye anasema kwamba vyama vya siasa visiitwe pale ambapo Rais anataka kuteua. Hii napinga na nitaendelea kupinga, na nitapinga tena zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu basi demokrasia katika nchi hii imekuwa na majukumu mengi, mazito na matatizo mengi yamezuka na bado watu wanaendelea kuiheshimu katiba. Kwa maana hiyo ni kwamba kifungu hiki kitakapoondoshwa, hatujui nini kitatokea katika nchi yetu ni lazima tuwe na hadhari. Kwa vyovyote vile huwezi kuwa na mtoto wako kalala ndani ya nyumba, lakini ukahesabu kwamba hayupo na ukaanza kugawa nafasi kwa watu wengine kwa sababu yeye kalala. Tunaamini kwamba mwaka 2020 huyu mtoto aliyelala anaweza kuamka, je akiamka akija kwenye katiba aje aseme irekebishwe tena, nafasi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ibakie pale pale kwa sababu hiyo ni nafasi yangu mwaka ujao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa misingi hiyo hatuwezi tukasema nafasi hii iondoshwe eti kwa sababu tu Makamo wa Kwanza wa Rais hakupatikani. Hakupatikana kwa sababu mwenyewe alikuwa kalala, na kwa kuwa kalala, basi *aliyelala usimuamshe, ukimuamsha utalala wewe*, ndio maana tukamuacha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa maana hiyo napenda kuchukua tena nafasi hii kusema kwamba, katika Katiba hii kuna vifungu kadhaa vilivyoeleza kwamba kuna mambo yanahitaji kupigiwa kura ya maoni pindi yakitakiwa kufanywa.

Sasa ninachotaka kusema hayo mpaka kufikia sisi Wazanzibari tukatia kifungu hiki ndani ya katiba yetu, kwamba yakitaka kufanyika haya tupige kura ya maoni, ilikuwa ni heshima ya viongozi wetu katika nadharia ya kuituliza nchi hii isiingie katika vurugu wala fujo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar, nampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kuwa na utaratibu wa kuweza kuifanya nchi hii iwe na amani na utulivu hadi mwaka 2020, tubadilishane tena vijiti kwa utaratibu ambao tumekubaliana nao. Lakini sio kufuta vifungu vilivyomo humu. Hivi vifungu ni vifungu tulivyoviweka na vinatukwaza, ingawaje tunataka tuingie, lakini unapoonekana kwamba wewe huna sifa ukiwekwa upande usikasirike, hii ndio ilivyo na kupokezana vijiti kwa utaratibu maalumu, hivi ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa misingi hiyo lazima Waheshimiwa Wawakilishi, tuheshimu Katiba yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama sisi tunavyoheshimu ilani ya Chama cha Mapinduzi. Bahati mbaya mimi sikuja na begi hapa, lakini mimi nimekabidhiwa ilani ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Baraza la Mapinduzi, ninaheshimu na nitaendelea kuheshimu, kwa sababu ndicho chama kinachotawala katika nchi hii. Kwa hivyo, leo akitokea mtu akasema ooh! maana yake tufute hii. Maana yake umesahau yaliyotokea, yaliyotokea ni makubwa mno katika nchi hii. Kwa maana hiyo...

Waheshimiwa Wajumbe: *(Walipiga Makofi kwa wingi sana na kwa muda mrefu)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Muongozo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja iliyoletwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Nasikia Waheshimiwa nakuja huko. Ahsante sana Mhe. Waziri. Kuhusu muongozo. Mhe. Hassan Khamis sijakutaja jina lako. Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, naomba kutumia kifungu cha 59(8)(d),

> Kifungu cha 59(8)(d), kinachosema:
>
> "Ni marufuku kwa Mhe. Mjumbe, kuzungumzia wajumbe wenzake".

Mhe. Naibu Spika, sisi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tumechaguliwa na wananchi majimboni wengine na wengine wameteuliwa, tuna haki ya kuzungumza jambo ndani ya Baraza la Wawakilishi na tuna kinga za Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, sio vyema kwa mwakilishi kumzungumzia mwakilishi mwenziwe kwamba kazungumzia jambo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, humu tuna haki na tunazungumza kwa mujibu wa Kanuni na Katiba. Kwa hivyo, naona Mheshimiwa aliyemaliza kavunja utaratibu, kwa hivyo atuombe radhi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakubaliana na Mhe. Machano Othman alivyosema. Lakini tangu hapo mwanzo wengi wetu tulitoka katika mstari vile vile. Kama mnakumbuka mlitoka katika mstari mkawa hamjadili

tena hoja ambayo imeletwa mbele, lakini mkawa mnajadili mambo mengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, maana yake watu wanasema ukimnyooshea mwenzio kidole kimoja na wewe huku vyengine vinakuelekea. Kwa hivyo, hilo mlilifanya tangu hapo awali Waheshimiwa Wajumbe. Sasa mimi kwa sababu limekuja hilo mbele ya utaratibu wa Mhe. Waziri ni kweli kwamba kuna baadhi ya maneno ambayo amezungumza ambayo sio sahihi. Kwa hivyo, nitamuomba atoe hiyo kauli, lakini hilo mlilifanya nyote. *(Makofi)*

Wengine sio nyote, wengine. Samahani sisemi nyote, lakini wengine. Nafuta maneno yangu sio nyote, wengine. Nimesema tena nafuta, sitaki kunyooshewa kidogo, nafuta. Nimesema wengine.

Sasa nitamtaka Mhe. Waziri asimame atoe kauli juu ya hilo suala ambalo amelizungumza.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru tena kwa kunipa nafasi, walau kama ningetaja jina basi ningeomba radhi, lakini kwa kuwa sikutaja jina siombi radhi. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, kifungu namba 59(8)(d), hakisemi kwamba lazima utaje jina. Naomba nikisome kifungu kilivyo. Kinasema kama ifuatavyo;

Kifungu cha 59(8)(d), kinachosema

"Ni marufuku kwa Mhe. Mjumbe,

(a) Kutumia lugha ya matusi au kashfa;
(b) Kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kucheleweshe shughuli za Baraza;
(c) Kumzungumza Mjumbe mwengine kwa nia mbaya au kumshambulia binafsi, isipokuwa kwa kutoa hoja halisi inayohusu mwenendo mahususi wa mjumbe huyo; na (d) ambalo nalitumia mimi ni;
(d) Kujiingiza katika mambo ya kuwasema Wajumbe wenzake."

Mhe. Naibu Spika: Wewe uko wapi?

Mhe. Machano Othman Said: Mimi niko kwenye kifungu cha (d), kwa sababu alisema humu kuna watu wamekuja na vikaratasi vyao mfukoni. Nani

aliyekuja hapa Barazani na vikaratasi na sote tuna haki. Kwa hivyo, natumia kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nawauliza waheshimiwa

Waheshimiwa Wajumbe: Aombe radhiii!

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hatutaki zogo hapa.

Waheshimiwa Wajumbe: Aombe radhiii

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sijampa mjumbe fursa ya kusema. Ninachokisema Waheshimiwa nataka tupige kura ili Mheshimiwa kama ipo nafasi ya kuomba radhi aombe radhi, Waheshimiwa kama wale wanaohisi kwamba Mheshimiwa kwa njia moja au nyengine katika hotuba yake amewalenga. Nasemaje, tusichukue muda mrefu kuzozana kuhusu hili, tufanye haki, Mheshimiwa wakati anazungumza pengine inawezekana kawagusa baadhi ya wajumbe, sasa ninachokisema hisia inawezekana mmoja au wawili wakahisi kwenye hisia kwamba ni hivyo, wengine hawakuhisi hivyo.

Naomba tupige kura wajumbe ambao wanahisi Mheshimiwa amelenga katika hisia za watu wengine wanyooshe mikono, mbona mko wachache sana. Mheshimiwa sasa uombe radhi.

Mhe. Said Soud Said: Mhe. Naibu Spika, kama kuna lugha ambayo imewakwaza baadhi ya wengine ningeshauri kabla sijasema lolote, wale wanaopendekeza kutaka kuleta miswada yao ya kisheria inayovuruga katiba kwanza wamuone Mwanasheria Mkuu, ili Mwanasheria Mkuu awaambie lete. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba kama Mhe. Machano anaona suala hili limemgusa yeye namuomba radhi.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tuelewane tusikilizane. Mhe. Waziri Soud naomba uombe radhi tumalize hili.

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiyekuwa na Wizara Malum): Mhe. Naibu Spika, nasemaje, ikiwa kama Mhe. Machano na wenzake waliokasirika juu ya hoja hii naomba radhi.*(Makofi)*

MUONGOZO

Mhe. Naibu Spika: kuhusu muongozo hili limekwisha lakini.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hili limekwisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mjumbe aliyepita katika maneno yake alisema kwamba Zanzibar haikuwa na katiba tangu 1964 mpaka 1984 kwa mujibu wa Katiba niliyonayo 133(a) Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1979 ilifutwa maana yake nini, maana yake kulikuwa na katiba.

Kwa maana hiyo kuweka *Hansard* sawa hapa amelipotosha Baraza, tuweke *Hansard* sawa Mhe. Naibu Spika, na hapo pia aombe radhi kwa sababu kasema kitu bila ya kukijua.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kama ulisema hivyo weka *Hansard* yako sawa, ni kuweka *hansard* sawa tu.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, katiba haiwezi kuundwa na mtu mmoja, katiba iliyokuwepo baada ya Mapinduzi kwanza hakukuwa na Katiba, katiba iliundwa na Baraza la Wawakilishi la mwaka 1980 ndio walitunga sheria na katiba, sasa kama kulikuwa na katiba ilikuwa yake yeye mfukoni huyo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hassan kaa kitako, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu tumalizie hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa jinsi ambavyo umeweza kukiongoza hichi kikao vizuri, lakini Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine tunapochangia tunasema mambo mengi, na wakati mwengine mtu anaposema inawezekana pia akateleza na ulimi.

Sasa hoja ambayo Mhe. Hassan ameisema na yeye alishaweka sawa kwamba ni kweli kabla ya katiba ya mwaka 1984 hii ambayo tunayo sasa hivi kulikuwa kuna katiba ya mwaka 1979. *(Makofi)*

Katiba hii ya mwaka 1984 ndiyo iliyokuja kufuta ile Katiba ya mwaka 1979. Sasa hoja hii Mhe. Naibu Spika, iko vizuri na imo ndani ya Katiba, niwaombe sana Waheshimiwa wajumbe tusiendeleze mjadala huu tukaufanya mrefu, kwa sababu mambo yenyewe yameelezwa ndani ya katiba yenyewe. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kutokana na muda ambao umebakia sidhani kama tutaweza kumaliza shughuli yetu hii pamoja na

kupitisha vifungu, hivyo basi ningemuomba Mhe. Waziri wa nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutengua kifungu cha muda ili tuweze kuendelea na shughuli yetu ili tuweze kufanya shughuli ambayo tunaifanya sasa hivi. Mhe. Waziri karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshelezi kufikia mwisho wa shughuli iliyo mbele yetu ya kupitisha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Hivyo, naliomba Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja sasa ningewauliza wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, lakini pili nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika suala zima la mabadiliko ya Katiba ambayo tunayapendekeza mabadiliko ya 11.

Mhe. Naibu Spika, ningependa sana kuomba tu kwamba nichukue nafasi kumshukuru sana Mhe. Machano Othman Said…

Mhe. Naibu Spika: Samahani sana Mheshimiwa wajumbe mnaotoka sasa hivi tutapitisha vifungu tunaomba sana mkimaliza tu kuswali mrudi ndani tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Mfenesini pale alipochukua nafasi ya kututanabahisha na kutukumbusha turudi katika mstari, ni utaratibu mzuri

ambapo kwa mujibu wa kanuni zetu za mwaka 2012 miongoni mwa utaratibu mzuri wa mazungumzo ni pale ambapo mmoja wetu amekwenda ama ameteleza kuona basi tunarejeshana katika mstari kwa utaratibu ule ambao tumeupanga, na utaratibu mzuri wa kukumbushana kwa mujibu wa kanuni. Ni jambo zuri na nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Machano Othman Said.

Pili Mhe. Naibu Spika, naomba nirudi katika msingi wa mabadiliko haya ambayo tunayapendekeza. Mabadiliko haya Mhe. Naibu Spika, ukiyatazama tumekuja na vifungu viwili ama ibara mbili za katiba ambazo tumekuja kwa ajili ya kufanya mabadiliko, na mabadiliko yenyewe ni kwa msingi wa kutaka kuendeleza vizuri zaidi mustakbali wa nchi yetu, katika utawala na kuwasaidia huduma wananchi tunaowaongoza.

Mhe. Naibu Spika, suala la mabadiliko ya Katiba si suala ambalo la kukurupuka, lakini si suala ambalo tunalazimika kwamba tusilifanye kila pale ambapo Serikali ama mjumbe ataona kwamba kuna haja au ulazima, naamini chombo hichi hakitosita kuchukua nafasi ya kufanya mabadiliko hayo, kwa msingi wa kusaidia maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyokumbuka na kama tunavyojua nyingi ya sheria zetu zinazotumika Zanzibar hasa hizi sheria za zamani zilikuwa ni sheria ambazo tumechukua na kutohoa kutoka katika nchi ya India, na India kwa kiasi kikubwa ni mwalimu mzuri sana katika tasnia ya sheria. Na tunapofanya kama *reference* kwa ajili ya mwalimu wetu lazima yako mambo ambayo tunapaswa tujifunze. Ukichukua mfano mzuri wa Katiba ya India ambayo naamini ni miongoni mwa katiba ndefu duniani ina vifungu takriban 390, ukitoa mwaka ambao wamepata uhuru katiba yao nadhani imeanza mwaka 1949 ama 1950.

Lakini mpaka mwaka huu katiba ya India tayari imefanyiwa mabadiliko mara 100 katika kipindi kisichozidi miaka 67, sasa katiba yetu ya Zanzibar mpaka mwaka huu takriban ni miaka 32 tumefanya mabadiliko ya 10 na hii tunayokuja nayo ni mabadiliko ya 11, kwa hivyo sidhani kama Katiba yetu tutaonekana kama vile tumefanya mabadiliko mengi kwa wakati mdogo, bila ya shaka yoyote tunafanya mabadiliko haya kwa kutambua katiba *is a dynamic is not a static*, kwa maana ya kwamba kila pale ambapo kutaonekana kuna haja ama ulazima wa kufanya mabadiliko kwa msingi wa kuendeleza maendeleo ya wananchi wetu sisi kama Serikali tutakuja na mabadiliko kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe watukubalie mabadiliko hayo ili tuendeleze mbele msingi wa maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kama sote tunavyokumbuka tokea nchi yetu ilivyoasisi mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, kwa kipindi chote Baraza hili la Wawakilishi limekuwa likijikuta kwamba ni itikadi mbili tu za siasa ndizo ambazo zinapata nafasi ya kushiriki katika chombo hichi, lakini Mwenyezi Mungu ameleta rehema zake katika Baraza hili la Tisa humu tumo viongozi, na tumo waheshimiwa Wawakilishi ambao tunatokana na Vyama vinne vya kisiasa. Jitihada hizi ni kubwa na lazima tuziunge mkono, ili kuweza kuziunga mkono jitihada hizi za kuondoa ule ukiritimba kwamba wawili mnapambana bila ya kuwa *neutralized*, ambao ni hawa wa vyama vyengine vya kisiasa. Naamini kwamba mabadiliko ambayo yanapendekezwa na Ibara hii ya 66 ni miongoni mwa chachu ya kuifanya kwamba tuondokane na mtazamo wa Baraza la Wawakilishi kwamba ni Baraza la vyama viwili vya siasa twende katika upeo sasa wa kuona kwamba tunatanua wigo na vile vyama vyengine vya siasa navyo vimepata fursa ya kuja kushiriki katika kutoa mchango wao kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mabadiliko haya yameelezwa vizuri sana, sababu na maudhui yake nayo ni moja tu, ni kutaka kumpa nafasi pana zaidi Mhe. Rais, badala ya kufungika kuona kwamba anashindwa kuwapa fursa watu wengine kuwateua kwa ajili ya kuharakiza michango yao, upeo wao, nguvu zao na harakati zao katika kujenga msingi wa kuendeleza maisha ya Wazanzibari katika nafasi za uongozi kwa kukwazika kwa sababu ya msingi wa Katiba basi tumeona ni busara kuja katika Baraza hili kuomba kufanya mabadiliko haya kwa madhumuni ya kutanua wigo na kuongeza na kuimarisha demokrasia nchini mwetu.

Matarajio yangu kwamba zipo baadhi ya nchi ambazo zimefanya mabadiliko makubwa katika katiba zao, lakini ukiangalia mantiki zinakuwa zina malengo ya kulenga watu binafsi, hazikuwa na malengo ya kulenga taasisi ama upana wa tasnia yenyewe kama vile ambavyo mabadiliko haya tunavyoyaleta mbele ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia mabadiliko mengine ya kifungu cha pili ni makosa ambayo yalikuwa yametokea katika katiba yetu na si busara kama atokee mtu anasoma kifungu ambacho kimekuwa kimenakiliwa ama kimefanywa *reference* ndani ya katiba kifungu ambacho hakipo. Sasa ni busara kuona kwamba Serikali tumeliona hilo na tumekuja kwa ajili ya kufanya masahihisho na usahihi ili kuweza kuweka kifungu halisi ambacho mtu yeyote akisoma anaweza kufanya *reference* zaidi kwa ajili ya kuweza kupata maudhui yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika mijadala hii kuna suala moja ambalo pia nalo limeulizwa. Naomba tu nichukue nafasi hii kuweza kutoa suala dogo tu linalohusiana na suala zima la kura ya maoni. Zipo nchi nyingi ambazo za Afrika katika katiba zao wameweza kuzingatia mfano mzuri ni Uganda, ukisoma kifungu 101 cha Rwanda pia nacho kinaelezea suala la *referendum*.

Pia ukitizama mfano mzuri wa mabadiliko ya Katiba ambayo wameyafanya wenzetu wa Rwanda katika nafasi ya kumuwezesha Rais kuweza kuondosha au kupunguza muda ule wa kutoka miaka saba kuja miaka mitano, wamefanya *referendum* kwa mujibu wa kifungu chao cha katiba ambalo jambo liko wazi kabisa. Wameweka utaratibu mzuri wa kuona kwamba kiasi gani katiba inaweza kulinda na madhumuni makubwa ya kufanya *referendum* ni kuona tu kwamba Katiba ile inabaki kama ni mali ya wananchi, na wananchi kwa wingi wao ndio wataamua yale mabadiliko makubwa ya maeneo mahususi ambayo yanaashiria katika kutaka kufanya hayo mabadiliko.

Pia ukiangalia katiba ya Rwanda kifungu 260 kimeeleza utaratibu mzima wa kufanya kura ya maoni katika yale mambo mahususi ambayo yameelezwa na katiba katika kulinda maslahi ya nchi. Jengine hata katika Katiba yetu ambayo tunapendekeza sote tunajua yamo mambo muhimu ambayo tumeona kwamba ili kulinda mustakabali mzuri kwa taifa letu ni busara mambo yale yaendelee kubaki kama sehemu ya kufanya mabadiliko kwa mfumo wa kura za maoni.

Mhe. Naibu Spika, niombe sana kwamba Waheshimiwa Wajumbe *concern* zao ni nyingi, na nyingi ni nzuri, za kuona kwamba ipo haja kwa Serikali kuipitia Katiba kwa mapana yake, na kuweza kuendana na matakwa au changamoto ama mabadiliko ya kidunia na mabadiliko ya nchi yetu, siamini kama Serikali itakataa mawazo hayo, na wakati muafaka ukifika Serikali itakuja kwa kuzingatia muono na maslahi ambayo sote tunayalenga ya kuimarisha na kuboresha huduma za wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niombe sana, tunafanya kazi ya siasa, kama tunafanya kazi ya siasa msingi mkubwa wa siasa ni kuwa na uvumilivu, tukiweza kuvumiliana tutaweza kusaidiana, kama hatukuweza kufanya kazi ya kuvumiliana kazi ya siasa itakuwa ngumu sana, maana msingi wa siasa ni kusema, lazima wewe useme mwenzako umpe nafasi na yeye aseme, wewe ujibu na mwenzako ajibu, mwisho wa siku mtakubaliana. Imani yangu kwamba mawazo ya Serikali tumeyaona, tumeyasema na tutaendelea kuyasema. Wenzetu walioko *backbencher* wameyasema ya kwao tumeyaona tunajadiliana mwisho wa siku tutakubaliana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema machache niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja kwa mia moja.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria iliyo mbele yetu.

Aidha, nichukue fursa hii niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, Waheshimiwa Mawaziri waliochangia hoja hii. Waheshimiwa Wajumbe walitoa hoja zao kwa mijadala ya wazi, ya kidemokrasia, ambayo imeonesha wazi upeo mkubwa na uwezo mkubwa wa kuona mbali walionao wajumbe wetu, naomba uniruhusu Mhe. Naibu Spika, niwapongeze sana kwa namna ambavyo nimeona mambo kwa kina, wameiona vyema Katiba yetu, wameona mahitaji yanayohitajika ndani ya katiba yetu, na kwa kweli ushauri wao ulikuwa wa busara sana.

Kama alivyonitangulia Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba kila kitu kina wakati wake, na mimi nataka nikubaliane naye kabisa kwamba kutokana na maelezo haya ya kina ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyasema, kwa vyovyote vile ipo haja wakati wa kufika basi yale ambayo ni muhimu kuletwa kwenye marekebisho mbele ya chombo chako hiki kitukufu ili yafanyiwe marekebisho na tuwe na Katiba iliyo bora zaidi inayojali wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe wanayafanya haya kwa msingi wa upenzi wa nchi yao, wanayafanya kwa msingi wa mapenzi ya wananchi ili tuweze kujenga maendeleo yaliyo makubwa sana katika nchi yetu. Kwa kweli sisi ndani ya Serikali tumekuwa tukifaidi sana michango yenu, imekuwa dira ya shughuli zetu mbali mbali za kuongoza nchi. Kwa hivyo niwashukuru na nazidi kuwaombea dua muendelee na misimamo hiyo ambayo kwa kweli inajenga na ni ya kizalendo ambayo matokeo yake inatusukuma mbele kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, hakuna jambo kubwa kama umoja wa nchi, maana umoja unazaa upendo, unazaa maelewano kitu ambacho kina mchango mkubwa katika kuimarisha amani na utulivu wa nchi. Kwa hivyo naamini sana haya yote ambayo tunayafanya dhamira yake ni kuwatumikia wananchi wetu na nchi yetu iendelee kuwa katika utulivu mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni makubwa ya kuleta mabadiliko haya ya marekebisho ya Katiba ya kifungu hiki ambacho kiko mbele yetu, dhamira yake kubwa ni kuondosha utata uliojitokeza. Nataka nikubaliane sana na Mhe. Hamza, alisema yako mambo waliyachangia wakati wakifanya mabadiliko ya kumi na leo akatukumbushia mengine. Ni kweli sisi kama binadamu hatuwezi kuwa na ukamilifu wa asilimia 100, kwa njia moja au nyengine yanatokea mapungufu na pale mapungufu yanapotokea basi tunarekebisha.

Rekebisho kubwa ambalo limezaa utata ni hili kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza. Leo tumeona hatuna Kiongozi wa Upinzani katika Baraza lakini kwa msingi wa umoja, kwa msingi wa kuheshimu mambo mengi ambayo tumeyazungumza huko nyuma mpaka tukafikia hapa na nchi yetu ikaendelea kuwa katika amani na utulivu, basi ni msingi huo na ni busara hizo zilizotumika katika Serikali kwa kusema kwamba Mhe. Rais atashauriana na vyama vya siasa ili kupata wale wajumbe wawili. Ilikuwa ni nia njema kabisa kutokana na matatizo yaliyojitokeza huko nyuma, ilikuwa nia njema kabisa ya kuendeleza umoja wetu. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana waheshimiwa michango yenu iko sahihi kabisa na iko juu ya mstari, lakini naomba sana tukubaliane na busara hii ya Serikali ili kuendeleza na kudumisha umoja na amani ya nchi yetu.

Ni kweli kabisa kwamba tunahitaji mabadiliko yatokee katika Katiba yetu na naamini Serikali itafanya hivyo wakati utakapofika, lakini kwa leo jambo ambalo liko mbele yetu ni kifungu hiki kimoja tunaporekebisha hiki hatuleti mabadiliko mengine yoyote ndani ya Katiba hii, kwa msingi huu tutakuwa hatujagusa eneo jengine, isipokuwa maeneo mengine yatafanyiwa kazi kwa kina na yakiletwa yaletwe na hoja zake tufanye mabadiliko kwa pamoja kwa mustakbali wa nchi yetu.

Baada ya maelezo haya machache Mhe. Naibu Spika, naomba tena kabisa niwaombe wajumbe wenzangu tuondoe utata uliopo tukipitishe kifungu hiki ili tuwe na Katiba ambayo haina utata katika kutekeleza kwake, na tutoe nafasi kwa Mhe. Rais aweze kutimiza matakwa ya kikatiba ili nchi yetu iendelee kuwa katika hali ya umoja, amani na utulivu.

Baada ya haya naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kutoa shukurani zangu kwa kunipa fursa na mimi angalau kusema machache katika hoja hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi

wa Umma na Utawala Bora ya Mabadiliko ya Vifungu viwili vya Katiba. Kifungu cha 66 na kifungu cha 79.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamezungumzwa, na mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyazungumza leo wameyazungumza kutoka ndani ya nyoyo zao jinsi gani wanaona tupate muda sasa wa kukaaa na kutafakari na kuja kufanya marekebisho mengine ya Katiba kama ambavyo waheshimiwa walivyotangulia kusema, hakuna jambo kama kushirikiana. Sisi tunaokaa huku mbele wala hatuna dhamira ya kupinga kila kitu ambacho Waheshimiwa Wawakilishi wanakuja nacho. Kwa sababu sisi tunaoshauri sisi pia ni binaadamu, inawezekana wakati mwengine unaposhauri kuna mambo pia yakakupitikia usione, lakini unapoingia ndani ya chombo hiki chenye wajumbe zaidi ya 80 basi bila shaka mambo mengi yataibuka na mengi wakati mwengine tunakubaliana na mengi yanakuwa yote ni ya msingi. Kwa hivyo niwatoe sana wasiwasi Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe kwamba si dhamira kila jambo linalokuja Serikali ipinge. Lakini pale ambapo tunasimama sisi tuna wajibu wa kutetea hoja za Serikali ambazo zimewasilishwa ndani ya Baraza hili, lakini baadae mwisho wa siku tunaamua kwa kura. Kura Mhe. Naibu Spika, ndizo zinazoamua hoja ambazo zimo ndani ya Baraza hili.

Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kama tunapofika kujadiliana tunajadiliana kwenye kujenga hoja tu, na hoja ambayo ita-*prevail* ni ile ambayo itapigiwa kura na wenyewe Waheshimiwa Wajumbe, na Waheshimiwa Wajumbe kuamua ndio demokrasia iliyomo ndani ya chombo hiki. Kwa hivyo tusije tukafika pahala Mhe. Naibu Spika, ikaonekana kama sisi tuna ukakasi wa kuzuia hoja hizi, lakini sisi tuna wajibu wa kusimamia na kutetea hoja hizi za Serikali ambazo zimeletwa ndani ya chombo hiki.

Sasa mengi yamesemwa Mhe. Naibu Spika, na mengi yamegusa vifungu na vifungu vyengine vimegusa vile ambavyo vinatakiwa marekebisho yake yafanywe, kwanza kwa kura ya maoni lakini vyengine vimezungumzwa kwa maoni ya Kamati kama navyo viingie kwenye marekebisho ya mswada huu, yaani marekebisho ya 11 ya Katiba hii. Sasa niwaombe sana Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Mhe. Abdalla Diwani kama hoja zao tumeziona lakini watuachie kwanza ili na sisi tukazitafakari vizuri, lakini baadaye tuje tujadiliane na tukubaliane. Niwaombe sana Mhe. Naibu Spika, kama hoja zao tumezisikia, wamejenga hoja zinazotokana na mawazo yao lakini wamejenga hoja zilizomo ndani ya nyoyo zao, kama wanaona sasa muelekeo uwe ni huu ambao wamekuja nao.

Mhe. Naibu Spika, lakini marekebisho ya kifungu cha 119 nayo yamepita kwenye awamu, mara ya mwanzo kabisa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi alikuwa ni Spika wa Baraza la Wawakilishi. Ukisoma Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ile *original* Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi alikuwa ni Spika wa Baraza la Wawakilishi. Lakini mazingira yaliruhusu tuanze kubadilisha muundo wa Tume ya Uchaguzi, tukabadilisha muundo mara ya kwanza, tukabadilisha muundo mara ya pili. Ilifika pahala hata muundo mzima tukautoa ndani ya Katiba tukaupeleka ndani ya sheria ya Tume ya Uchaguzi, kama sasa hata ule muundo ule wa wajumbe usiwe wa Kikatiba uachiwe sheria. Maana yake unapobadilisha Katiba inataka *two third majority* ya kila awamu ya kwanza na ya pili unaposoma, lakini tukaona tuiondoe tuipeleke kwenye sheria. Lakini baadae tukairudisha tena kwenye Katiba kusema kwamba sasa hapana tuirudishe tena kwenye Katiba.

Sasa kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, kimepita kwenye marekebisho mengi, na ndio ombi letu sisi kwa Waheshimiwa Wajumbe kama na sisi tuchukue muda tutafakari ili tukubaliane kama sasa muelekeo na muundo upi wa Tume ya Uchaguzi ambayo sasa twende nayo. Sasa kwenye hili niombe sana Kamati yangu ya Katiba, Sheria kama kwenye hili niwaombe ili marekebisho yao ambayo wamekuja nayo basi kabla hatujafika kwenye kupitisha vifungu basi hii waiondoe hoja yao ambayo wamekuja nayo ili zibaki hizi hoja ambazo zimeletwa na Serikali.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, ni hoja ambayo ameleta Mhe. Abdalla Diwani ambaye anaomba kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 80(2) cha upitishwaji wa miswada.

Naelewa hoja yake, dhamira yake ni nzuri kama anaona sasa kwa nini miswada yote mengine tunapoleta inasomwa mara tatu. Inasomwa mara ya kwanza, ambapo inakuwa haijadiliwi lakini inakuja kusomwa mara ya pili na mara ya tatu kwenye Kikao kijacho cha Baraza. Lakini hoja ya Mhe. Abdalla Diwani ni kwamba kwa nini tusifuate utaratibu huo ambao umewekwa ndani ya Kanuni ya 83(1) na 83(2).

Hoja yake ni ya msingi lakini nimkumbushe Mhe. Naibu Spika, kwanza kama angesoma Kanuni ya 77(6) kanuni yenyewe ya Baraza mbali ya kwamba tayari Kanuni ya 83(1) na (2) imeweka utaratibu wa kupitisha miswada hii kwa kusomwa mara tatu. Lakini kwenye kupitisha Mswada wa Katiba Kanuni ya 77(6) yenyewe imeweka utaratibu wa kwamba Katiba hii isomwe mara ya kwanza na mara ya pili. Lakini masharti hayo pia ni masharti ambayo yamewekwa kwenye kifungu cha 80(2) chenyewe cha kusema kama Katiba hii

unapotaka kuibadilisha, basi uibadilishe kwa kusomwa mara mbili. Mara ya kwanza na mara ya pili na kila mara unapoisoma lazima upate *two thirds majority* ya kila *reading* unayofanya.

Sasa tunapopitisha miswada mengine yote ya Katiba hatufati masharti ya kupata *two third majority,* tunaamua kwa *simple majority*. Sasa nimuombe sana ndugu yangu Mhe. Abdalla Diwani kama tusifike pahala tukataka kuishurutisha Katiba ifuate Kanuni, nimuombe sana. Kwa sababu akisoma ibara ya 4 ya Katiba, Katiba yenyewe imejieleza kama Katiba ndio sheria mama na itakuwa na nguvu juu ya sheria nyengine zote tunazozitunga. Kama sheria nyengine yoyote tunayoitunga itahitilafiana na kifungu cha Katiba basi Katiba ndio itakuwa ina nguvu. Kwa hivyo Katiba Mhe. Naibu Spika, tayari imeshajiwekea utaratibu wake.

Sasa nimuombe sana Mhe. Abdalla Diwani kwa vile kifungu cha 80(2) cha Katiba kimejiwekea utaratibu huo na ndio maana kifungu cha Kanuni cha 77(6) nacho kikaweka utaratibu ule ule ambao umewekwa wa kikatiba wa namna ya kupitisha Katiba.

Sasa utaratibu upo mzuri, utaratibu wa kupitisha miswada umewekwa, lakini utaratibu wa kupitisha Katiba pia nao umewekwa ndani ya Kanuni hiyo hiyo. Sasa nikuombe ndugu yangu Mhe. Abdalla Diwani baada ya hoja hizi nikuombe sana hoja yako ambayo umeileta nayo pia uiondoe kwa sababu ya ufafanuzi uliokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Hamza amezungumza mengi sana na kama nilivyosema yote haya aliyoyazungumza, ameyazungumza ndani ya moyo wake kama ameona sasa umefika wakati anaizindua Serikali lakini analizindua na Baraza kama tukae tufanye tafakuri ya pamoja ya jinsi gani muelekeo wa nchi yetu sasa uwe.

Mapendekezo yake ni mazuri, mapendekezo yake yanajadilika, mapendekezo yake mengine ni ya msingi kabisa. Lakini nimuombe kama haya lazima tukubaliane kwa sababu mengine haya tuliyoyafanya yamekuja baada ya *sacrifice* kubwa iliyofanywa, na ndio maana tukafanya marekebisho haya. Haikuwa rahisi kuja na marekebisho ambayo yamo leo hii ndani ya Katiba.

Sasa nimuombe sana Mhe. Hamza lazima sisi kama Serikali lakini wao kama wajumbe tuyatafakari sana mambo haya kwa pamoja, na hili tutakapokubaliana tukubaliane kwamba huo sasa ndio muelekeo wetu sote.

Sasa nimuombe sana Mhe. Hamza kama na haya ambayo wameyazungumza tumeyasikia wananchi wake wameyasikia, lakini na sisi ombi letu pia atukubalie kama atuachie ili na sisi tuyafanyie tafakuri ili tujue sasa tutayafanyia utaratibu gani wa marekebisho.

Sasa baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kuunga mkono hoja hii iliyokuwepo mbele yetu hapa kwa asilimia mia moja, lakini pia niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kama tumpitishie Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora hoja yake hii iliyopo hapa mbele bila ya mabadiliko yoyote.

Ninakuombea sana na naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu sasa waheshimiwa kwa kuwa Mwanasheria Mkuu kuna maombi, kabla ya kuendelea Mhe. Waziri wale ambao Mwanasheria amewaomba maoni yale kukubali ombi ambalo amelitoa Mwanasheria Mkuu, naomba sasa kama lipo hilo Mhe. Machano amenileta lakini sijapata kutoka kwa Mhe. Diwani wala kwa Mhe. Hamza. Sasa kama kutakuwa na jambo lolote basi naomba waliseme sasa hivi.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nimesimama hapa kwa niaba ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala kuzungumzia tamko la Serikali.

Kwa mujibu wa Kanuni kifungu 113(f) Kamati yetu inapewa mamlaka ya kuzungumzia miswada ambayo tutaipata baada ya kukabidhiwa na Mhe. Spika. Tulikabidhiwa mswada huu wa marekebisho ya 11 ya Katiba tukaujadili kwa pamoja na Mhe. *AG* na wataalamu wengine wa sheria. Lakini sisi kama Kamati tulikuwa na haki pia ya kutoa mapendekezo yetu mapya kwa mswada huu. Lakini leo bahati nzuri baada ya majadiliano na Waheshimiwa Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wameahidi kwamba Serikali baada ya kuipitia Katiba upya watafanya marekebisho makubwa ya Katiba.

Kwa hivyo sisi Kamati, mimi Mwenyekiti wao naona hakuna haja ya kulazimisha kwamba vifungu hivi vibadilishwe leo, sisi ni Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi tumesikia kauli ya Serikali, kwa hivyo mimi kwa niaba ya Kamati naondoa yale mapendekezo ya Kamati, lakini pia naomba waheshimiwa wengine walioleta mapendekezo yao tukubaliane na mapendekezo ya Serikali tuipe muda ikafanye kazi kwa uadilifu mkubwa baadaye tutaona mapendekezo ambayo yataletwa baadae.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kusema kwamba sisi tunaondoa yale mapendekezo na tunaunga mkono vile vifungu ambavyo vimeletwa na serikali kama vilivyo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa nafsi yangu nilipendekeza hili wazo tu la kurekebisha kifungu cha 80(2), lakini bila ya kumkwaza Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi nathubutu kutamka kwamba naondoa hili suala, najua kama mtangulizi wangu Mwenyekiti wa Kamati kasema kwamba serikali inajipanga kuja kufanya marekebisho nategemea na hili litakuwemo. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa upande wangu nataka niwashukuru mawaziri; Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini vile vile Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutumia utu uzima na busara kubwa, kwa sababu wao wanajua yaliyomo ndani ya mioyo yetu na ninaamini kama walivyosema Waheshimiwa Mawaziri hawa kwamba wao walileta wazo lao kama serikali, na kimsingi kama walivyotangulia wenzangu tumekubali yale ambayo waliyoyaleta, na kwa kuzingatia vile vile kwamba na sisi kwa kuwa wamesema na wao wameyachukua yale ya kwetu watakwenda kuyajadili na ninaamini watakwenda kuyafanyia kazi.

Kwa hiyo, ninaamini yale mawazo kwa sababu sisi tukitoa mawazo Mhe. Naibu Spika, kama tunavyosema, tunatoa mawazo kwa niaba ya wananchi wetu. Sasa kitu ninachokiomba serikali, lakini na sisi vyama vya siasa. Mhe. Naibu Spika, hakuna suala zito katika nchi kama Katiba, leo Katiba hizi tunazitengeneza katika mazingira magumu sana ya kuridhia alau tuwe tunaelewana. Lakini sasa isiwe kwamba leo tunatengeneza Katiba kwa kuridhiana, halafu baadae yale yale tuliyoridhiana watu wakishatoka nje wanayakiuka yale yale. Ina maana kila siku tutakuwa tuna kazi ya kumpa kazi kubwa Rais kila siku kuangalia ni maeneo gani ya kuweza kurekebisha. Sasa naomba sana tuna-*sacrifice* sana kupitisha hizi Katiba wakati mwengine bila ya kutaka, lakini unajua ndio unatengeneza nchi, sasa basi na sisi tuheshimu yale ambayo tumeweka katika misingi ya Katiba. Viongozi wetu huko tumewatengenezea nafasi leo hawamo humu ndio huo uchungu ambao tunauona.

Basi mimi baada ya hayo nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, naishukuru sana serikali basi naamini mashirikiano yetu yataendelea kuwepo na ninaamini

haya kama nilivyosema hamtoyakalia mtakwenda kuyafanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika wakati huu katika kulizungumzia jambo la kheri.

La pili Mheshimiwa nianze kwanza kwa kutoa neno la kiungwana kuwashukuru waheshimiwa watatu pamoja na wengine wote, lakini naanza na hawa watatu. Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Hamza Hassan Juma. Maana yake *AG* nilikuwa namtizama anavyozungumza nao anavyotoa taarifa, basi nilihisi sasa kabakia kuwabeba tu maana yake anawaambia katika lugha ya kuwa ni *very humble* ya kwamba wamfahamu, na *AG* huyu amepea sina wasi wasi. (*Makofi*)

Mhe. Hamza alisema neno hapa nataka nianze na hilo hilo, Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako. Alisema Maalim Haroun ni Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na tunamuomba aitendee haki Katiba yetu katika kipindi hiki.

Mhe. Hamza kama nilikutendea haki ulipokuwa darasani nikakusomesha na sijakudanganya kama *this is a book*, nilikwambia *this is a book* sijakwambia *this is a dog* na wakati ule kwa sababu ndio unajifunza. Kwa hivyo, napenda nikuhakikishie wewe pamoja na Waheshimiwa wote nakushukuruni sana na nitaitendea haki Katiba hii ili iendane na wakati wetu unavyokwenda.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niwataje wote waliochangia. Jumla ya waliochangia ni watu 17, watu 12 wamechangia kwa kusema na 5 wamechangia kwa maandishi.

1. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Machano Othman Said
2. Mhe. Ali Suleima Ali (Shihata)
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
4. Mhe. Hamza Hassan Juma
5. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi (Makoti)
6. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
7. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
8. Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Juma Ali Khatib)
9. Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Said Soud Said)

10. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
11. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali
12. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
2. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
3. Mhe. Miraji Khamis Mussa; na
4. Mhe. Waziri wa Afya

Mhe. Naibu Spika, mimi nimekuwepo kwenye Baraza hili kwa vipindi vinne sasa hivi na nawaombea wenzangu *in shaa Allah* wapate vipindi kama hivyo. Na kama kuna *maturity* ya *contribution* basi mimi nimeshuhudia katika Baraza hili, hawa wawakilishi wengi ni wapya lakini michango yao utafikiri wamekuwa Barazani kwa miaka zaidi ya minne au mitano. Kwa hivyo, mimi naanza na kuwapongeza sana tena wote nikalinganisha na ile hadithi ya mzee wangu mmoja alikuwa na tatizo, wengine wanaijua nitaisema hapa kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika. Kwa sababu kila mchangiaji anayesimama anachangia vizuri kiasi ambacho unafikiri huyu ni mzuri zaidi kuliko aliyepita, akija mwengine na yeye anachangia vizuri.

Kuna hadithi ya mtu alikuwa na tatizo la miwani haoni, akaniambia wewe Mwalimu Mkuu wa Haile Salassie wakati ule Hamza mwanafunzi wangu pale Haile Salassie, basi akaniambia nifanyie mpango nipate miwani palikuwa na madaktari wa *Lions Club* walikuwa wanakuja Mhe. Mahmoud, *Lions Club* walikuwa wanatusaidia sana katika skuli zetu na maeneo yetu kwa hivyo wananchi huwa wanakuja. Akaniambia hebu nisaidie nifanye mpango niwepo katika kupimwa macho na mimi nina matatizo, haya. Nikamfanyia mpango nikazungumza na madaktari akaingia ndani, nikampenyeza kutoka Ofisi ya Mwalimu Mkuu ambayo ilikuwa ndio ofisi yangu, basi akaingia ndani akawekwa kwenye kiti kile akawekwa ile miwani iliyokuwa na *frame* tu, akaanza kutiwa kioo cha kwanza akasema mizuri, akawekwa kioo cha pili akasema kizuri zaidi, akapewa kioo cha tatu akasema hii ndio niliyokuwa naitafuta. Ah! Nikajiuliza huyu ana matatizo ya macho kweli, nikamwambia yule daktari nikamnong'oneza hebu mpe *frame* tupu iliyokuwa haina vioo, basi akavalishwa haina vioo akasema hii ndio naondoka nayo naichukua sasa hivi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nasema haya kwa sababu sio kwamba nazungumza ndio Maalim Haroun hadithi zake tu, *no*. Mimi nimeridhika na michango ya waheshimiwa hawa, kwa kweli wanaisaidia nchi yetu na wananchi ambao wamewachagua. Kwa hivyo, naomba kama ni miezi tisa sasa hivi karibu tunachangia hivi inaelekea mheshimiwa katika miaka mitatu, minne ijayo *in shaa Allah* tukijaaliwa tutakuwa na rasilimali kubwa katika Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na michango mizuri iliyotolewa na waheshimiwa wote na mawaziri wenzangu kunisaidia, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Mwanasheria Mkuu wamenirahisishia kazi sana hii ya kufanya majumuisho.

Mimi sitaki nichukue muda mwingi lakini nisije nikageuka yule Shekhe hadithi nyengine hiyo. Kuna Shekhe mmoja alikuwa anamsomesha mtu mmoja sasa husomesha halafu humuuliza Shekhe hapa unasemaje? Hapa nilikuwa nakwambia bwana Mtume ametwambia tufanye moja, mbili, tatu basi yule mwanafunzi akamjibu nilikuwa niseme hivyo hivyo. Tukaendelea, tukaendelea akamuuliza tena Shekhe hapa unasemaje, hapa anasema Mwenyezi Mungu anatuhimiza tufanye moja, mbili, tatu yule mwanafunzi akamwambia Shekhe ilikuwa niseme hivyo hivyo, akamwambia toka umeshahitimu, wewe kila ninachosema wewe ulikuwa useme hivyo hivyo sasa unaniuliza kwa nini. Sasa na hapa sitaki mimi nigeuke huyo mwanafunzi wa kuuliza mambo nikasema na mimi nilikuwa niseme yote waliosema Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu), Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na *AG* na mimi nitasema kidogo ili nisije nikaambiwa niondoke.

Mhe. Naibu Spika, ninachohimiza mimi kimoja ambacho naanza nacho naomba sana tuendelee kushikamana tujenge umoja wetu na amani yetu katika nchi yetu. Mheshimiwa tuna kila sababu ya kuringia umoja wetu na amani yetu katika nchi yetu, na hili ndilo lilotupeleka hapa sisi sote tuliunge mkono hili. Umoja wetu ndio unaotupeleka hapa na mshikamano wetu, tumuombe Mwenyezi Mungu Mhe. Rais wetu Mungu ampe umri mrefu, ampe afya njema *in shaa Allah* ni mtu mwenye hekima na busara kubwa sana katika nchi yetu anatuongoza kwa uadilifu mkubwa sana. Kwa hivyo, sote tumuunge mkono Rais wetu kwa sababu nia yake ni nzuri katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, tunafanya marekebisho haya leo tumeshafanya kumi mengine, hili ni la kumi na moja, kwa hivyo naomba kama tulivyopendekeza iwe ni hivyo tupitisheni vifungu vyetu hivi bila ya matatizo yoyote *in shaa Allah*.

Naomba sana wenzetu maombi yenu yote ya marekebisho mlioleta naahidi lile ambalo Mhe. Hamza aliloniambia kuitendea haki Katiba, *in shaa Allah* tumeyakusanya maoni yenu yote na tumeyathamini sana na musiwe na wasi wasi jambo zuri lolote halihitaji haraka, tutakwenda nalo kwa wakati ili tuweze kufanya marekebisho hayo kila haja itapotekezea. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kutoa hoja *in shaa Allah* ili tuendelee na hatua nyengine.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja sasa niwaulize wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kidogo naomba mnisikilize ni kwamba kwa utaratibu wetu kawaida tunapopitisha vifungu huwa tunapitisha vifungu nauliza kama mnakubali mnanyoosha mikono tunaendelea. Lakini leo kutokana na kanuni za kupitisha mabadiliko ya sheria katika Katiba inabidi tuwahesabu wale ambao wamekubali pamoja na wale ambao wamekataa. Kwa hiyo, wakati tutapokuwa tunakubali na mnanyoosha mikono itabidi kidogo mkae na mikono juu ili Makatibu waweze kuwahesabu. Nafikiri nimeeleweka vizuri waheshimiwa tunaanza.

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Mhe. Mwenyekiti: Mikono juu waheshimiwa, tumeshawahesabu tayari kwa sababu tunataka kuweka *record* sio suala tu la kwamba ni wote. Sawa waheshimiwa wanaokataa, wanaokataa, tunaendelea waheshimiwa.

Kifungu 2 Kusomwa

Sehemu ya Pili

Marekebisho ya Vifungu Mbali Mbali

Kifungu 3	Marekebisho ya kifungu cha 66
Kifungu 4	Marekebisho ya kifungu cha 79

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja wanaokubaliana na hoja, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliew)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya 2016

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi na Moja ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya Tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu lakini vile vile niwashukuru sana kwa kupitisha marekebisho ya sheria hii ambayo yalikuwa ni muhimu sana kwetu sisi pamoja na taifa letu kwa ujumla.

Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa hatua ambayo mumefikia, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na kamati na watendaji wake wote pamoja na Mwanasheria Mkuu kwa kuweza kupitisha sheria hii na nimtakie kila la kheri na mafanikio katika utekelezaji mwengine ambao umekusudiwa kwa ajili ya sheria hii.

Baada ya kusema hayo machache Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao chetu hiki cha leo…

Waheshimiwa Wajumbe, mtanisamehe tuna matangazo mawili kwanza. Tangazo moja ni la timu ya ushindi wa Yanga wakutane nje, tangazo hilo limeletwa na Mhe. Jazira, poleni sana Simba.

Na tangazo la pili ni Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Serikali Mwenyekiti wao anawaomba vile vile wakutane nje tu baada ya kutoka hapa. Baada ya hayo waheshimiwa naahirisha hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni.

(Saa 7:37 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/09/2016 saa 3:00 asubuhi)